

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 13 Juni, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Tukae sasa. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tisa, Kikao cha Arobaini na Tano. Baada ya leo bado Vikao viwili tu. *(Kicheko)*

Katibu!

#### NDG. YONA KIRUMBI -KATIBU MEZANI

#### HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

na

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea kama nilivyoahidi jana, kwamba orodha yangu ni ndefu sana. Sasa nitaanza na dakika saba saba nione tunavyoenda, nadhani baada ya kama saa moja hivi inabidi turudi kwenye dakika tano

tano. Tuanze na saba saba tuone tunakwendaje, kwa hiyo kengele ni moja tu, ikilia tu maana yake dakika zako saba zimekwisha.

Tutaanza na Mheshimiwa Mariam Ditopile, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kujijalia kuwa sehemu ya Bunge hili nikihudumu kama Mbunge wa Viti Maalum, nawakilisha kundi la vijana kwa heshima ya chama changu Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kuungana na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kulongoza vyema Serikali ya Awamu ya Tano. Pia nisiwe mchoyo wa fadhila na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na msaidizi wake Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tangu Awamu ya Tano ianze hii ni bajeti ya tano, lakini tumeona ni namna gani bajeti hizi zilivyo bora, zikiweka kipaumbele kwenye maendeleo, ongezeko la mapato na nidhamu ya matumizi. Hata hivyo, wameenda mbali zaidi na kuwa wazalendo kutumia fedha zetu wenyewe kwa ajili ya miradi yetu ya maendeleo. Vilevile bajeti hizi zinaakisi mahitaji halisi ya nchi na wananchi na zikiwa zimegusa moja kwa moja mategemeo na matumaini ya wananchi hususan wanyonge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii bajeti yetu ya mwisho kabla ya Uchaguzi Mkuu, lazima tuwaeleze wananchi mambo mema na mazuri ambayo yamefanywa na Serikali yetu na pia chini ya usimamizi wa Bunge hili kwenye Uongozi wako Mheshimiwa Spika. Mimi nawakilisha vijana na ninasema katika kundi ambalo limependelewa ni vijana. Mheshimiwa Rais kazi yake ya kwanza kuitekeleza ilikuwa kutekeleza elimu msingi bila ya malipo.

Mheshimiwa Spika, tumeona *impact* ya hii, ile shilingi 20,000 ya ada na michango ilikuwa ikinyima fursa ya watoto wa wanyonge kwenda kupata elimu na mtu anaekupa elimu ndio anakupa msingi wa maendeleo. Tuliona *program* hii ilivyoanza udahili ulizidi kwa zaidi ya asilimia 105. Serikali sikuu haikuishia hapo tumeona ukarabati wa shule kongwe zaidi ya bilioni 63 zimetumika kukarabati shule zaidi ya 63 kongwe. Tunakumbuka huko nyuma elimu ya *A-level cream* kubwa ilikuwa inatoka kwenye shule za Serikali, lakini baada ya miundombinu kuwa mibaya hii sifa ilipotea. Kwa hiyo Serikali hii imeliona hilo imefanya marekebisho na shule zetu zinapendeza na elimu itapanda kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, haikuishia hapo tumeona bajeti za mikopo ya elimu ya juu zikiongezeka mwaka hadi mwaka; kwa sababu mwaka 2014/2015 ilikuwa bilioni 348.7 lakini imepanda mpaka bilioni 450 mwaka 2019/2020. Sio tu kutenga bajeti lakini mfumo wa utoaji sasa hivi ni wa haki, wale wanaopaswa kupata mikopo hii ndio wanapata, ndio maana umesikia hakuna kelele wala hakuna migomo kwenye Vyuo Vikuu, maisha yanaendelea. Hapo hapo nichomekee tumeona Mheshimiwa Waziri amesema mfumuko wa bei umekuwa chini na hii inatugusa sisi vijana. Hata kule vyuoni sisi ndio tunakaa kwenye hosteli, tunakula vyakula vyaa mama ntilie kutokana na mfumuko wa bei kuwa chini, basi hata maisha yetu kule vyuoni yamekuwa mazuri na tunaweza kupata elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, tumeona sio kila mmoja atapitia kwenye mfumo huu wa elimu mpaka vyuoni, lakini tunaenda kujenga Serikali ya Viwanda, tunahitaji mafundi mchundo ndio maana Serikali kila mwaka inaweka bajeti na utekelezaji upo wa kujenga Vyuo vya VETA kila Wilaya, jamani hakuna ya kusema sisi vijana.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye suala la ajira, kila mwaka ajira zinatolewa kwa Walimu, ajira zimetolewa kwa Madaktari tena 1,000 kwa mara moja, haijawahi kutokea. Pia tumeona Mheshimiwa Rais akitumia Vijana wa JKT katika ujenzi wa miundombinu ambao ni historia; ujenzi

wa Ukuta wa Mererani, ujenzi wa Ikulu Chamwino lakini hajaishia tu kuwatumia kwenye kujenga amewapa kipaumbele na wakimaliza *operation* hizo wanapewa ajira. Nani kama Mheshimiwa Magufuli kwa vijana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumeona kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye Wizara yake ya Kazi, Ajira na Vijana na ametuwekea mtu sahihi kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri Kijana, shupavu Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde akihangainka kuweka miradi kwa ajili ya vijana; vitalu nyumba, mizinga ya nyuki yote kutafutia vijana, lakini amekuwa mkali kwa kuwapa vijana wazawa kazi ambazo huko zamani zilikuwa zinafanywa na wageni.

Mheshimiwa Spika, tumeona vile vile kupitia Halmashauri mikopo ya asilimia nne ikitolewa huko zamani ilikuwa ni Sera lakini kupitia TAMISEMI kwenye Serikali hii ya Awamu ya Tano sasa ni sheria na kanuni zimetoka na mambo yanaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini tumeona Serikali hii imefanya makubwa kwenye madini, lakini asilimia 70 ya wanaojihusisha kwenye madini hasa wachimbaji wadogo wadogo ni vijana. Mheshimiwa Rais ametenga muda wa kuwasikiliza, lakini sio kuwasikiliza na kutatua kero zao tumepunguziwa kodi, wamewekewa masoko mazuri, kwa hiyo kwa kweli vijana sasa hivi wanatajirika na rasilimali zao. Hata marekebisho ya sheria ya rasilimali hiyo inatugusa sisi kizazi kichanga na kizazi kijacho, leo hii watu hawatoona lakini huko mbele sisi vijana na watoto wetu tutaona faida ya marekebisho ya sheria hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye miradi mikubwa ya kimkakati, mradi wa *Stiegler's gorge*, Bwawa la Nyerere, *Standard Gauge* zinatoa ajira za muda mfupi na muda mrefu na wanufaika ni Vijana, jamani. Pia tumeona Shirika la Ndege, watu wengine wehu unawashangaa kabisa, wanasesma eti ndege zinasaidia nini. Tulikuwa tuna vijana wetu wapo kwenye *Avviation Industry* wanasona u-pilot, u-cabin crew walikuwa wakafanye kazi wapi, waende wakafanye kazi emirate? Leo hii tuna vijana zaidi ya 60 ni

ma-pilot wanarusha *Bombardier*, wanarusha *Airbus*, wanarusha *Dreamliner* mpaka India. Jamani nani kama Mheshimiwa Magufuli kwa vijana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye kilimo, miradi ya umwagiliaji imezidishwa bajeti, wanufaika wakubwa ni vijana. Tozo kwenye mazao ya kimkakati korosho, zabibu kwa vijana wangu wa hapa Dodoma – Mpunguzi, zimetolewa na zinapandisha thamani ya mazao yetu. Hatukuishia hapo, nashukuru Mungu wameanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nimpongeze, kuna kundi lilikuwa nalitetea walikuwa wanadharau wachuuzi wa mazao, lakini leo hii waratambulika na tunaona vijana wazawa wanavyolindwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, Mheshimiwa Rais hakuishla hapo ameaminii vijana kwenye Serikali yake Mawaziri, Ma-*DED* na sisi tunasema Vijana kupitia Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi tunaingia pindi na Mheshimiwa Rais atapata kura za kishindo kupitia sisi vijana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile, hakika umeuwasha moto asubuhisubuhi, sasa kazi inaendelea. Naona *Chief Whiep* wa Upinzani anatoa macho anaona duuu, hizi bunduki nitaziweza hizi.

Mheshimiwa Oran Njeza atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuchangia hii hotuba ya bajeti. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa sana katika miaka hii mitano, mfano ni kwenye jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote katika nyanja zao zote, wamefanya kazi

kubwa mno, ilikuwa ni kazi ya kimapinduzi na ya kimageuzi, tunawashukuru sana tena sana. Nawashukuru pia kwa kukisafisha Chama cha Mapinduzi, sasa hivi tunatembea kifua mbele na sisi tunaotoka ile mikoa ambayo ilikuwa na Upinzani mkubwa sasa hivi nikuhakikishie Upinzani kwa kweli umekwisha. Jimbo langu la Mbeya sasa hivi CCM tunatembea kifua mbele kwa ajili ya kazi iliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimpongeze Waziri wa Fedha, mimi nipo kwenye Kamati ya Bajeti kwa kweli ushirikiano wake ni mkubwa mno. Uweledi wa Timu yake ni mkubwa mno, kwa kweli bajeti hii nilikuwa najaribu kulinganisha na bajeti nyingine za nchi zinazotuzunguka za Afrika ya Mashariki na Kati imekuwa ni bajeti ya mfano. Wakati nchi nyingi ziliogopa sana kwamba bajeti zao zizingatie kuangalia athari za *Covid 19*, balaa hili la ugonjwa wa *corona*, lakini bajeti yetu ukilangalia na ni ya ukweli kabisa, imeondoa kabisa hiyo dhana.

Mheshimiwa Spika, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri tuangalie ni maeneo gani ambayo tunaweza kupata *quick wins*, matokeo ya haraka ili tuweze kukidhi na kuhakikisha kuwa hii bajeti yetu inakamilishwa na inatekelezwa kwa ukamilifu wake. Nipende vile vile kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi alizozifanya katika Jimbo letu la Mbeya Vijiji. Kazi kubwa iliyofanyika ni kwenye miundombinu na miundombinu imesaidia sana kwenye kilimo. Jimbo la Mbeya Vijiji lilikuwa halina barabara za Vijiji za lami ukiondoa zile barabara kuu, lakini leo hii kilomita chungu nzima zinajengwa barabara za lami ambazo zinapelekwa kwenye maeneo ya uzalishaji wa kilimo. Barabara hizo nyingi zimekamilika na nyingi zinaendelea kujengwa, namwomba Waziri wa Ujenzi vile vile ajaribu kuangalia ni namna gani atakamilisha zile barabara ambazo zipo kwenye mpango kwa vile hizi ndio zitachochea utekelezaji wa hii bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, nipende kumkumbusha vile vile Waziri wa Ujenzi, tulipotembelewa na Mheshimiwa Rais

aliahidi kutengeneza barabara moja muhimu sana kwa wakulima; Barabara ya Mbalizi kwenda Chigamba, ile barabara ni barabara muhimu sana, kuna uzalishaji mkubwa, ukisikia Mbeya ndio kuna uzalishaji mkubwa wa chakula hilo eneo ndilo linalozalisha chakula kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda ningependa kugusia *quick wins* zingine ambazo ni kwenye madini. Mbeya tumebahatika kuwa na madini ya aina nyingi. Tuna madini yanaitwa *niobium*, kuna wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza kuleta viwanda ili wachakate madini hayo kutoka sehemu mbalimbali duniani na yale madini ambayo yatachimbwa hapa nchini. Kwa kweli hiyo ni fursa, namwomba Waziri wa Madini ameanza kulifanyia kazi hilo, ahakikishe hili linakuja haraka ili tuweze kupata pesa za kigeni, zisaidie katika utekelezaji wa bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye miundombinu, naomba tuangalie ni namna gani tuboreshe reli ya *TAZARA*, reli hii ni muhimu. Umuhimu wa Reli ya *TAZARA* ni kwamba inapunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima, lakini pia itatupunguzia gharama za mazao yetu yanapokwenda sokoni. Naomba hili litiliwe mkazo, tuangalie kama ilivyosomeka kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi hii reli ni muhimu sana kwenye uchumi wetu. Iende sambamba, tunapoendelea na kuboresha miradi mingine ya kimkakati hii miradi mingine tulionayo iwe ni kuyaboresha tu hatuhitaji pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye kilimo. Kilimo kinahitaji masoko, tumelima tumezalisha sana lakini tatizo tulilonalo kubwa ni masoko. Namshukuru sana Waziri wa Kilimo amekuja na mageuzi makubwa sana kwenye namna ya kuendesha masoko ya kimtandao. Alitumie sana soko letu la bidhaa kwa vile hili ni soko la Kimataifa litatusaidia sana kuhakikisha ya kuwa wakulima wetu wa pareto, kahawa, mahindi na mazao mbalimbali wanapata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwenye miradi ya maji; mradi wa maji ambayo alikuwa ametuahidi kwenye Jimbo letu kwenye Mji wa Mbalizi

umekamilika sasa hivi. Maji yanatoka sasa hivi iko kwenye hatua za usambazaji na tunamwomba Waziri wa Maji ahakkishe kuwa yale maji yasambazwe kwa wakazi wa Mbalizi pia na kwenye miji jirani kama Mji wa Songwe pamoja na Kijiji cha Ilota.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa vile vile nizungumzie kwenye upande wa Afya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, amejenga Vituo vya Afya...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mashimba Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya mwaka 2020/2021. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, mbeba maono ya nchi yetu kwa kutupa pesa za kutosha ili kutekeleza miradi mbalimbali kwenye Jimbo langu la Maswa Magharibi.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kumsaidia vema Mheshimiwa Rais kwa kazi zake. Mimi namuita mama huyu ni simba jike. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo anasimamia shughuli za Serikali hapa Bungeni, lakini pia shughuli za Serikali kule nje, mimi namuita baba huyu ni simba mwendapole ndiye anayekula nyama.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe kwa kazi nzuri ambazo unazifanya katika Bunge lako hili Tukufu na unaonekana ni mpole lakini naweza kukufananisha na nyoka yule anayeitwa kifutu, ni mpole sana lakini ukikanyaga

mkia wake ndiyo utajua ana sura ya namna gani. Hongera sana Mheshimiwa Spika, naamini ndugu zangu wa pale Kongwa watatenda yale tunayotarajia ili kipindi kijacho uendelee kuwa kiongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo sana mambo mawili kabla sijaenda kwenye hoja yangu inayohusu jimbo langu na mkoa wangu. Ukuaji wa uchumi ni hesabu ya kisayansi, siyo tu hesabu ya kawaida ya darasa la pili, mbili jumlisha mbili kwamba ni sawa na nne, haiwezi kuwa hivyo. Tunaposema uchumi wa nchi utakua kwa asilimia kumi au asilimia saba, Wachumi kuna vitu tunavyoviangalia ili uweze kufika hapo na ndiyo maana huwa tunasema uchumi utakua kwa asilimia saba halafu tunaongeza neno tunaloliita kwa Kilatini *ceteris paribus*, maana yake kuna mambo ambayo lazima yawekwe sawa ili kufikia uchumi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo siyo hesabu tu ya kusema mbili jumlisha mbili ni sawa na nne na kwa sababu hukuandika nne basi umekosa haiko namna hiyo. Hesabu ya ukuaji uchumi ni hesabu ya kisayansi, ni hesabu ya kichumi, ni hesabu ambayo inaeleweka kwa Wachumi, sasa ukifanya kama unavyofanya hesabu ya kawaida utakuwa unakosea. Wakati mwininge tunaposema uchumi unaweza ukakua kwa asilimia saba, unaweza ukakua kwa zaidi ya hapo, kwa sababu zipo nchi ambazo zimeweza kufanya hivyo na kitendo hicho kinaitwa *the great leap forward*, kwa hiyo inawezekana kabisa uchumi wa nchi yetu ukakua kupita kiwango tulichotarajia ikiwa mambo fulani *ceteris paribus yatafanyika vizuri*.

Mheshimiwa Spika, nizungumze pia kwa sababu kuna jambo jana lilitajwa hapa linalohusiana na umeme; kwamba kwenye Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati alisema tutakuwa na uzalishaji wa umeme *megawat* 4,000, hapana! Kwenye Kamati ya Bajeti tawimu tulizonazo Mheshimiwa Waziri alizozileta zinasema, mpaka 2025 uzalishaji wa umeme utakuwa umefikia megawati 3,053, lakini kufikia Februari mwaka huu uzalishaji wa umeme katika nchi yetu ulikuwa megawati 1,602.318 wakati mahitaji yetu Februari,

2020 ilikuwa ni megawati 1,151. Kwa hiyo utaona kwamba tuna umeme wa ziada mpaka sasa hivi, kwa hiyo tunapokuwa na umeme wa ziada, sasa wewe unataka tuzalishe mwingi haraka tuupeleke wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka sasa nihame niende kwenye hoja ya mkoa wangu. Tunataka kujenga nchi ya uchumi wa viwanda kuelekea uchumi wa katii. Kule kwenye Mkoa wangu wa Simiyu tuna kiwanda cha vifaa tiba ambacho mpango wake ni kuanzia mwaka 2017 na kuendelea mpaka leo, ilikuwa inatarajiwa kwamba mpaka 2018 mradi huu ungekuwa umeanza, mradi huu ungekuwa umeshawekwa jiwe la msingi na Mheshimiwa Rais lakini mpaka sasa hivi haujaanza. Sasa tatizo sijaelewa ni nini, kwa sababu wanaotoa fedha ni *NHIF*na *WCF*, wako tayari kutoa pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, *due diligence* ilishafanyika ya kwanza ikafanyika na Wizara mama na ya pili ikafanyika na Wizara ya Fedha. Mlipaji Mkuu wa Serikali alifanya *due diligence* hiyo na ikatoa matokeo mapema na ikasema mradi ni *viable*, yaani una faida unaweza ukaanzishwa, lakini nashindwa kuelewa mpaka leo mradi huu haujaanza wakati michakato yote hiyo imefanyika. Pesa zipo, *NHIF* wako tayari, *WCF* wako tayari, mikutano mbalimbali ilishafanyika, Waziri wa Ajira Mheshimiwa Mhagama, Waziri wa Afya, Waziri wa Uwekezaji, Waziri wa blashtara, wote walishashiriki na kuitisha mradi huu, lakini haujaanza/

Mheshimiwa Spika, mradi huu una faida kubwa katika nchi yetu na mkoa wetu wa Simiyu kwa sababu utatumia pamba tunayozalisha. Kwa hiyo...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, lakini naomba majibu kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri ili mradi huu uanze kuanza kwa sababu ni ahadi pia ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante.  
*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Andrew Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa asubuhi ya leo nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kusema machache na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika hii Bajeti Kuu ya Serikali. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo muda mrefu tunarejea tena kwa wenye nchi kuomba ridhaa yao tena. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kupitia wewe kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya kwa pamoja. Kwa sababu kazi ya Bunge hasa; vyama vya siasa vinapoomba ridhaa kwa wananchi ndiyo maana tunaomba sana mkituchagua tuyafanye haya na haya kwa maendeleo yetu; na ndio maana Chama cha Mapinduzi katika llani yake ya 2015 kiliwaeleza wananchi wa Tanzania kwamba mtuamini kupitia mgombea wetu Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli sasa kwamba tutayafanya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuyafanya hayo kunategemea idadi ya Wabunge wako ulionao. Ndiyo maana najisikia vizuri sana ninapoona idadi kubwa ya Wabunge wa CCM waliotokana na wananchi waliomo katika Bunge hili na kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Kazi yetu sasa imekuwa kwa kipindi cha miaka mitano kuwezesha shughuli za Serikali kupitia Bajeti yake ya kila mwaka na mipango yake inayoletwa katika miaka ya maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunarejea kuomba ridhaa ya Watanzania tena tukiwa tunatembea vifua mbele. Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ameitendea haki llani ya uchaguzi ya CCM katika maeneo yote na ndiyo maana tangu jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipowasilisha

hotuba yake, Waheshimiwa Wabunge wengi, hata ndugu zangu wa upande mwagine kule wameyasema mazuri ambayo yamefanyika katika nchi yetu kwa kipindi cha miaka mitano hii. Hongereni sana CCM, hongereni Waheshimiwa Wabunge wa CCM, hongera sana Mheshimiwa Rais Dkt. Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda ni mfupi, lakini nasema katika kipindi hiki tunaona kama tutaweza kusimamia vizuri hata mapato yetu kidogo yanayopatikana, tunaweza tukafanya vizuri sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake katika Wizara hii. Tunaona tulikoanzia 2015/2016 na leo kupitia *TRA*, kazi kubwa nzuri imefanyika kwa mapato ya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kwa maboresho ya makusanyo kutumia vifaa vya elektroniki, tunaona makusanyo yasiyo ya kodi tunafanya vizuri, kwa upande wa Halmashauri tunafanya vizuri, unaona pengo kati ya bajeti yetu, mahitaji yetu linazidi kupungua. Ila *deficit* ya bajeti itaendelea kuwepo. Hata mataifa makubwa unakuta wana *budget deficit*. Eeh! Hata hivyo, tunafanya vizuri katika kuziba hilo pengo. Nashukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kubwa zaidi ukiangalia katika kipindi cha miaka hii minne hasa 2016, 2017 mpaka mwaka huu wa fedha, unaona fedha nyingi iliyolekezwa na Serikali kwa upande wa maendeleo yetu ya ndani tumepelekea Serikali kupitia fedha za ndani, mnaona katika Hotuba ya Bajeti na Taarifa ya Kamati ya Bajeti ni pesa nyingi. Fedha za ndani zimekuwa shillingi trilioni 24.63 za ndani. Hongera sana kwa sababu wewe ndio umewezesha kupitia Bunge hili haya kufanyika. Eeh! Wanaposema wenzangu, nami nikutakie kila la kheri kwa wananchi wa Kongwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua hali ya sasa ya dunia, *Covid* hii ndiyo, lakini isitufanye sasa tuogope kufanya makubwa ambayo tunapaswa kuyafanya kwa faida ya maendeleo ya Taifa letu. Tunafahamu pesa ya wenzetu

itaendelea kupungua na itapungua hasa katika kipindi hiki, maana kila mmoja anaangalia hali yake, lakini sisi tungeelekea sasa katika maeneo ambayo yanaweza yakatusaidia kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, eneo moja ambalo nafikiri tuliangalie kwa ukaribu sana ni suala la utalii, kwa sababu tukilibeba vizuri na hali tunayoiona sasa ikabadilika, watalii wakaanza kurejea Tanzania, tukafanya vitu ambavyo ni vya ushindani, tutaweza kuinyanya kwa haraka sana hii sekta muhimu ambayo inatuletea asilimia 26 ya mapato yote ya fedha za kigeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naelewa zipo changamoto, lakini tukiiacha hii; maana utalii lazima uambatane na uhifadhi wa wanyama wetu, hasa wanyamapori. Najua tuna changamoto kidogo kwa sababu ukiangalla vitalu vyetu vya uwindaji ambavyo ndiyo vinafanya sehemu kubwa ya uhifadhi, hatujafanya vizuri sana. Napenda tuliangalie hilo kwa pamoja ili tuweze kuona namna ya kuisaidia Sekta hii ya Utalii tunapopambana na hali yetu ya sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limesemwa sana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, napenda tuangalie hali ya barabara zetu za vijijini tufanye kila linalowezekana katika mwaka ujao wa fedha, hata kama ni kufanya *reallocation*, tuhakikishe *TARURA* inawezeshwa kwa kiwango kikubwa ili barabara zetu za vijijini na madaraja yaweze kutengenezwa na barabara hizo ziweze kuitika na kubeba mazao ya wakulima wetu na kuleta tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Uvuvi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Ooh! Loh! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nawashukuru wananchi wa Bariadi walionipa heshima ya kuwa hapa Bungeni. Nawatakiwa Waheshimiwa Wabunge wote kheri na fanaka tunapoelekeea na turejee tena mwezi Novemba katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Andrew Chenge.

Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. Mheshimiwa Mchengerwa pia hayupo. Haya, hawa nawaruka. Mheshimiwa Raphael Chegeni na Mheshimiwa Willam Ngeleja, aah, afadhali, wananiokolea muda maana orodha yangu ni kubwa sana leo. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ngeleja halafu Mheshimiwa Shamsi.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwa hakika nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuipongeza Serikali na hasa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa hotuba hii nzito kabisa iliyojaa matumaini kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati tunachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini pia kwenye hotuba ya Wizara ya Katiba na Sheria, baadhi ya mambo tuliyoyazungumza kwa kina mojawapo ilikuwa ni suala la gonywa la *Corona* ambalo limeikumba dunia.

Mheshimiwa Spika, pili, tulizungumzia kuliomba Shirika la Fedha ama Benki ya Dunia, mashirika makubwa ya fedha duniani kuzingatia yale ambayo nchi tajiri duniani, zile G20 zilikuwa zimeamua kuzipa ahueni kidogo nchi zinazoendelea na nchi masikini kwa madeni ambayo zinadaiwa na zinatakiwa zilipe kila mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya mambo ambayo tulyiyazungumzia nami nilitoa mchango wangu kuhusu maeneo hayo. Katika hilo iliibua hoja ya mjadala kuhusu masuala ya tiba asili na tiba mbadala. Nasimama hapa nikiwa nazungumza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema lakini pia kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ukiwemo mwongozo wako katika kuipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo pamoja na yote ambayo imeyafanya, pia kusimama imara na kuwa thabiti katika kuhakikisha kwamba katika vita ambayo tulikuwa tunapambana nayo na sasa tunaendelea kupambana nayo ya ugonjwa wa Corona, silaha zote zitumike ikiwemo tiba asilia ama tiba mbadala. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Ummy. Bunge lako Tukufu hili pamoja na Watanzania kwa ujumla kama nchi tumesimama kwa pamoja kutumia silaha zote ambazo tunazo kuhakikisha kwamba janga hili la *Corona* tunalishinda na kwa kweli tunaona sasa matumaini kwamba tunakoelekea na tulipofikia ni pazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana nataka kusema, jambo hili kama lisingesimamiwa vizuri na Serikali chini ya Uongozi wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli, nina hakika kwamba nchi bado ingekuwa na tataruki kama ambavyo tumeona baadhi ya nchi duniani bado zinaendelea kuhangaika. Tunaipongeza sana Serikali na Mheshimiwa Rais tunampongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hayo pia tulishauri Serikali, nawe ultioa mwongozo kwamba Serikali ianze kuzungumza na Bunge lako Tukufu kuititia Kamati ya Bajeti kuhusu namna ambavyo sisi kama nchi tungeweza kunufaika na ile ahueni iliyotolewa na hizi nchi tajiri. Ni majuzi tu Shirika la Fedha Duniani limetoa kauli, taarifa kwa dunia nzima kuonyesha kwamba sisi Tanzania tumesamehewa madeni ambayo yana thamani ya dola milioni 14.3 kwa kipindi ambacho tungeweza

kuwa tunalipa kuanzia mwezi wa Sita huu hadi mwezi Oktoba.  
*(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna *potential*, kuna uwezekano kabisa wa kuongezewa ahueni hiyo au msamaha huo kama tutaendelea kufanya vizuri na kadri ambavyo Serikali inaendelea kuzungumza na haya Mashirika makubwa ya Fedha Duniani na nchi tajiri. Kwa hiyo, nilikuwa nasema pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema na kuungana na Watanzania wenzangu kuendelea kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanya. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, ahueni tunayoizungumza, wataalam wa mahesabu wanasema hii milioni dola 14.3 ni sawa na shilingi bilioni kama 33 hivi za Kitanzania. Manufaa yake ni kwamba ukitafasiri kwa shughuli za kawaida kwa mfano uzungumzie ukamilishaji wa maboma na miundombionu ambayo Watanzania wamejenga maeneo mbalimbali; ujenzi wa Zahanati; Vituo vya Afya, nyumba za Walimu, madarasa; ni maelfu ya miundombinu hii itakamilishwa kutokana na afueni tulioipata. Kwa hiyo, hongera sana Serikali, tunawapongeza sana. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kulipongeza Bunge lako Tukufu na Watanzania tukiongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi miaka miwili iliyopita tuliyoyapitisha hapa kutunga sheria rasmi kabisa ya kulazimisha Halmashauri zetu sasa ziwe na mwongozo thabiti wa kutoa makusanyo hayo ya ndani kwa 4% inayopatikana katika Halmashauri zetu ziende kwa wanawake na 4% ziende kwa vijana na 2% ziende kwa walemavu. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na mwongozo wa kisera miaka mingi na miaka miwili iliyopita tulitunga sheria mahususi kwa jambo hilo. Hilo ni jambo kubwa kutokana na vita dhidi ya umasikini. Tumejiongezea sasa fursa ya kuwaimarisha Watanzania katika mapambano dhidi ya umasikini. Jambo hili linahitaji heshima kubwa na pongezi kubwa kwa Serikali na kwa Bunge lako Tukufu. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, tumemtaja Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa mambo mengi, tumeitaja Serikali kwa mambo mengi na tumekutaja wewe kwa namna mlivyojipambanua. Hata hivyo nataka nimtambue Mheshimiwa Rais; kama Watanzania wengi wanavyokumbuka kwamba Mheshimiwa Rais pia tukimwangalia kwenye *angle* ya kimichezo amekuwa ni mhamasishaji namba moja katika kuendeleza sekta ya michezo na sanaa hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeona amezungumza na wasanii mara kadhaa kuwapongeza, kuwatia moyo na pia tumeona namna ambavyo anashiriki kuendeleza michezo Tanzania. Ndiyo maana juzi nilishangaa sana nilivyosikia baadhi yetu hapa wanazungumzia goli moja liliofungwa na timu fulani inayoitwa *Utopolwa FC* kwenye mchezo mmoja miongoni mwa timu zinazocheza Ligi Kuu.

Mheshimiwa Spika, nilidhani mambo ya msingi ya kuishukuru Serikali na kumpungeza Mheshimiwa Rais pamoja na Bunge lako Tukufu ni kutambua uongozi Imara ulioonyeshwa katika kuendeleza michezo namna ambavyo tumefanikiwa Timu ya Taifa kushiriki mashindano ya *AFCON*, pia tunavyokwendaa vizuri kwenye maandalizi ya Kombe la Dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nilidhani kwamba Simba *Sport Club* timu maarufu kabisa katika ukanda huu siyo kwa Tanzania tu, ilistahili kutambuliwa katika chagizo lake namna ambavyo inaibeba Tanzania. Hii ni timu kubwa inayoongoza katika kuchangia wachezaji kwenye timu ya Taifa, timu ya Simba *Sport Club* ndiyo inayoongoza kutoa wachezaji wengi sana kwenye Timu ya Taifa. Tulidhani kwamba wanaozungumza kwa nyakati zozote zile kuhusu maendeleo ya michezo Tanzania na hasa soka, huwezi kusahau mchango wa Timu ya Taifa, Timu ya Simba ambayo inachangia wachezaji wengi katika timu ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, uongozi pia katika vilabu hivi vyatya michezo ni jambo la msingi sana kutambua.

Pale *Simba Sports Club* kuna uongozi uliosimama imara, ndiyo maana huwezi kusikia mgogoro. Ndiyo maana timu nyingi sasa zinaiga kufuata mfumo ambao unaendeshwa na timu ya *Simba Sports Club* kulifikisha soka letu Tanzania katika anga za Kimataifa. Katika hayo, wapo watu wanazaliwa kwa ajili ya kuendeleza michezo katika kila nchi na wapo watu wahamasishaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa Mheshimiwa Rais, Tanzania tunajivunia kuwa na mtu anayeitwa Haji Sande Manara, amesimama kidete kushirikiana na Watanzania wenzake akitetea na kusogeza mbele kabisa hamasa kwa Watanzania na ndiyo maana leo tumeona hamasa ya soka Tanzania imeimarika sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja, nawatakia kila la kheri wenzangu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngeleja. Nakupongeza sana kwa mchango wako mzuri, *very exemplary* na hasa ulipomalizia kwenye michezo na Bunge hili linaingia katika *record* kwamba ndiyo Bunge ambalo liliweza kupeleka Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 70 kwenda nje ya nchi Cairo Misri ili kuweza kui-support na kuishangilia Timu ya Taifa. Hakika Bunge la Kumi na Moja limefanya mambo mengi ambayo hayajawahi kufanyika huko nyuma, baadhi ya watu hawaelewi tu. (*Kicheko/Makofii*)

Nilishamtaja Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na atafuatiwa na Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. SHAMSI V. NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu nitazungumzia nafasi ya uongozi katika maendeleo ya Taifa. Nitatumia muda mwingi sana kutoa nasaha hasa kwa Waheshimiwa Wabunge vijana na kwa sababu hii itakuwa ndiyo hotuba yangu ya mwisho katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Rais wa Marekani, John F. Kennedy aliwahi kusema; "*Tunafanya mambo siyo*

*kwasababu ni rahisi lakini tunafanya mambo kwasababu ni magumu”*

Mheshimiwa Spika, moja katika sifa kuu na ya msingi ya kiongozi ni utuhubutu wa kufanya maamuzi magumu. Kwa hili tunasmhukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na kiongozi mwenye karama na kaliba hiyo ya uongozi. Tumeona hapa hivi karibuni namna Rais wetu na kwa namna tofauti na tilivyozoea alivyoshughulikia tatizo la *corona*. Dunia nzima imekuwa ikizungumzia juu ya haja ya kuwafungia wananchi wao ndani ili kudhibiti maambukizi ya virusi vyta *corona* lakini Rais wetu alikuja na njia tofauti; na kwa bahati mbaya sana wengi walimkejeli lakini mwisho naona wanaungana naye na hapa inanikumbusha maneno ya watu wenye hekima wanaposema; ‘*unapokuwa na kiongozi sahihi kwa wakati sahihi akafanya mambo sahihi bila shaka Taifa lilitapiga hatua*’ na hilli tunalliona kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa uongozi kwa maendeleo ya Taifa, sisi kama Taifa kwa maoni yangu hatujawekeza kiasi cha kutosha katika kuwatengeneza viongozi, hasa vijana. Siku zilizopita tulifanya makosa kidogo, tuliteleza. Tulikuwa na Taasisi ya Manedeleo ya Uongozi (*IDM-Mzumbe*) iliyofanya kazi kubwa katika kuandaa vijana wenye mwazo ya kimapinduzi akiwemo marehemu Mzee wetu, Edward Moringe Sokoine.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuhi wa basi tunaona dhahiri kwamba katika siku hizi za karibuni tunaanza kupoteza kizazi hicho chenye fikra huru na mawazo ya kimapunduzi. Unaposikiliza mijadala ya Bunge hapa unaiona hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi napata wasiwasi juu ya hatima ya uongozi na muskabali wa taifa letu baada ya Dkt. Pombe Magufuli kumaliza muda wake; na nadhani huu siyo wasiwasi wangu pake yangu, Watanzania wengi wamekuwa akijiuliza jambo hili na unaposikiliza mijadala ya Bunge unalionia hilo waziwazi hasa Wabunge vijana.

Mheshimiwa Spika, Mbunge anaanza kuchangia kuanzia mwanzo mpaka mwisho analaumu tu, hatoi sera mbadala na wala hatoi ufumbuzi wa matatizo. Na tambua kwamba taifa letu Tanzania lina mazuri yake, lina mabaya yake, lakini sisi kama viongozi wa Kitaifa hatuwezi kuwa msitari wa mbele kueleza hadharani matatizo ya Mama yetu Tanzania. Wenzetu walioendelea hawafanyi hivyo. Tujifunze kutoka Taifa la Marekani; Wamarekani wale wana matatizo mengi sana unapokwenda katika nchi yao lakini wanapokuwa nje ya taifa leo wanajenga taswira kana kwamba Marekani ni pepo ya Dunia; na hili halitokei tu kwa bahati mbaya. Viongozi wa kitaifa wana nafasi kubwa sana katika kutoa mwelekei na taswira ya kuwalea watu wao na hasa vijana.

Mheshimiwa Spika, Wanasaikolojia wanasema '*maneno huumba*'. Ukiwa kama mzazi kila ukiamka unasema mtoto huyu hasikii, hana maendeleo, hatafanikiwa. Kinachotokea katika akili na kinachojengwa na wazazi ndicho hicho hicho kitakachotokea baadaye. Na taifa ni hivyo hivyo viongozi wake kila wakiamka wanasema Tanzania haina jema, Tanzania inafanya mambo ya hovyo mwisho wake itakuwa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, narudia nasema, Tanzania kama taifa ina mema yake. Inawezekana ina mabaya yake lakini viongozi hawawi msitari wa mbele katika kueleza hasa hadharani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema sisi kama Wabunge na hasa Wabunge vijana inawezekana tunayaona mengi. Tunayo haki ya kukosoa. Napendekeza tukosoe pale panapostahiki, tupongeze pale panapostahiki, lakini tukosoe kwa hesima.

Mheshimiwa Spika, na mwisho nasaha zangu; tupendane kwa tunayokubaliana na tustahamiliane kwa yale tusiyokubaliana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha hakika wewe ni mmoja wa *Statesmen* humu ndani, tunakuombea kwa kila lillilo jema.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Amina, Amina, Amina.

**SPIKA:** Nilikutaja Mheshimiwa Kangi Lugola utafuatiwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa namna ambavyo umeleta heshima ya Bunge hili machoni mwa Watanzania. Hakika wewe ni Jembe.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri Mpango, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea bajeti ya kiwango na ya kizalendo; na ndiyo maana miradi mingi ya kimkakati itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Majaliwa kwa namna ambavyo ameweza kuhakikisha shughuli za Serikali katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinakwenda vizuri na katika mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa niaba ya wananchi wa Mwibara wote kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa mambo makubwa ambayo ametutendea Wana Mwibara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Magufuli alitupa barabara ya lami tumbakiza kilometra saba, nani kama Magufuli? Mheshimiwa Magufuli alitupatia kivuko (*panton*) kinachohudumia Wana Mwibara na ng'ambo ya Musoma Vijijiini, nani kama Magufuli? Mheshimiwa Magufuli ametupa vituo vitatu vya afya; Kasahunga, Nansimo pamoja Kisorya na Nasuguti, nani kama Magufuli? Mheshimiwa Magufuli ametupa miradi mikubwa ya maji Kata ya Iramba, Bulamba, Kibara, Kalukekere na Magunga, nani kama Magufuli?

Mheshimiwa Mafuguli mpaka sasa tunamalizia kujenga *high school* mbili ya Bulamba pamoja na Nansimo, nani kama Magufuli? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie muda wangu kwa kuwakumbusha Watanzania na kuwaleleza Watanzania na wapinzani waweze kumjua vizuri Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Magufuli ni Lulu ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli amejenga heshima ya Taifa hili na ndiyo maana Taifa hili liko kwenye kilele cha juu cha kutenda haki machoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niiliwahi kusema kwamba Mheshimiwa Magufuli watu wa aina hii hawaziliwi kila wakati na niiliwahi kusema watu wa alia hili huwezi kuwapata kila mahali; na ndiyo sababu watu ambao unaweza kuwapata kila mahali ni walevi kama wakina Mheshimiwa Mbewe ambao unaweza kuwakuta kwenye *Grocery*, unaweza kuwakuta Chako ni Chako...

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** ... lakini Mtu kama Magufuli huwezi kumkuta kila mahali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli ninamfananisha na Mwenge wa uhuru...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kangi naona Mheshimiwa Esther Bulaya amesimama.

## TAARIFA

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, tunaheshimu mawazo ya kila mmoja, lakini *trend* ya mjadala unavyoendelea na kutoa lugha za kuudhi dhidi ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani hili halivumiliki. Ningeomba kititakao kimuelekeze Mheshimiwa Kangi na Wabunge

wengine; unaweza ukawachamba sana wapinzani lakini *personal attack* si lugha za Kibunge.

Mheshimiwa...

**SPIKA:** Nakuhsukuru sana, ahsante sana leo muda wetu ni mdogo sana ndiyo maana unaona niko *strict* kidogo na nina orodha kubwa sana...

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba Kiti chako kielekeze...

**SPIKA:** Nakushukuru, mimi ninachokiangalia zaidi hapa ni kama mtu amesema uongo, ndilo la muhimu. Kwa hiyo kama mtu akisema ukweli basi ukweli unabaki kuwa ukweli. Mheshimiwa Kangi nafikiri hiyo ni taarifa yako zaidi. (*Kicheko*)

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Habari ya mjini sasa hivi ni kwamba Mbewe alilewa akavunjika mguu, ndiyo habari ya mjini.

Mheshimiwa Spika, namfananisha Mheshimiwa Magufuli na Mwenye wa Uhuru. Mwenge wa Uhuru wakati unawashwa tulisema sisi tunakata kuwasha Mwenge na kuweka juu Mlima Kilimanjaro umulike nje ya mipaka yetu, utele tumaini mahali ambapo hakuna matumaini, utele faraja mahali ambapo kuna huzuni na utele upendo mahali ambapo kuna chuki, na vilevile uweze kuleta heshima mahali ambapo kuna dhara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanini nimesema Mheshimiwa Magufuli ni Mwenge wa Uhuru? Tangu Mheshimiwa Magufuli alipoanza kabisa kujenga heshima katika utumishi leo tumeshuhudia dharau iliyokuwa kwa baadhi ya watumishi kutotenda haki na kuwashudumia Watanzania leo kuna heshima ya hali ya juu katika utumishi. huo ndiyo Mwenge wa Uhuru unamulika. Mheshimiwa Magufuli alivyoanza kuwabana Mabeberu na waliokuwa wanaiba rasilimali za nchi hii leo tumeshuhudua amejenga heshima na hivyo

amekuwa mlinzi wa rasilimali za Watanzania. Mheshimiwa Magufuli ni Mwenge wa Uhuru.

Mheshimiwa Spika, leo tumeshuhudia mahali ambapo kulikuwa hakuna upendo; Mheshimiwa Magufuli amekuwa akiyaita makundi mbalimbali ikulu wakiwemo Maaskofu, Masheikh, Wachungaji, wafanyabiashara pamoja na watu wa kawaida, akihubiri upendi pamoja na haki katika Taifa hili. Mheshimiwa Magufuli ni Mwenge wa Uhuru. Mheshimiwa Magufuli ni Mtu mwenye huruma na ndiyo maana ninamfananisha kama Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliye hai

Mheshimiwa Spika, na ukosoma Luka 18 wakati ule Yesu alipokuwa anatembea alipokaribia Yeriko alimkuta kipofu mmoja anaitwa Batoromeo Thimao akamfuata akamwambia unataka nifanye nini juu yako? Akasema nataka kuona. Yesu akamwambia kuanzia sasa ka imani yako unaona na ndiyo sababu Mheshimiwa Magufuli kila ziara anazozifanya katika nchi hii amekuwa kama yesu Kristo, Watanzania wanamlilia, Watanzania wanamfuata kwa shida mbalimbali na ndiyo maana nazitatu papo kwa papo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magufuli ninamshukuru sana aliponiteua kuwa Waziri kwenye Baraza lake; na ndiyo maana aliponitengua Uwaziri Mheshimiwa Rais nilisema maneno haya kwamba; *Mheshimiwa Magufuli ulinipa heshima, ultoa Uwaziri kwangu na leo Mheshimiwa Magufuli umetwa Uwaziri ulio wako, jina la Magufuli libarikiwe*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Watanzania, tunapokuwa na Rais wa namna hii hatuhitaji tena kuingia kwenye mjadala wala michakato ya kutafuta Rais mwingine kwasababu huyu Rais wa Watanzania tayari amekwishapatikana na ndiyo maana Dkt. Bashiru na Polepole wamezunguka Nchi nzima wana-set mitambo ya Chama Cha Mapinduzi kilichobaki ni kufiyatua ili wapinzani wajue kwamba wembe ni ule ule uliowanyoa kipindi kilichopita utaendelea kuwanyoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka Bunge hili liwaambie Watanzania kwamba katika kipindi cha miaka mitano ambacho tumekuwa na Rais, Dkt. John Pombe Magufuli tumekuwa na Bunge ambalo limetuelekeza katika kuhakikisha kwamba tunapitisha bajeti za kuwatendea haki Watanzania. Ndiyo maana kuna mikakati mikubwa ambayo tumeiweka na kupitisha fedha kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, leo tunakwenda kupata umeme wa *Stiegler's gauge, megawatts 2115*. Leo tunakwenda kuwa na reli ya kisasa, leo ndege zinahudumia na kupandisha kiwango cha watalii katika Nchi hii, nani kama Magufuli Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Spika, mimi wapinzani nawashangaa sana. Hivi kweli katika mazingira haya ya sasa ambayo kila mahali linapotajwa jina la Magufuli, linapotajwa jina la CCM Watanzania wote wanassema kwamba pale Kalvari yote yamekwisha, hatuhitaji tena uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mimi nawashauri wapinzani; kwa kuwa kila wakati katika nia njema na katika kutenda haki hatuhitaji malumbano katika taifa hili, hatuhitaji kugawanyika katika taifa hili. Twende tuhakikishe kwamba Rais tuliyempata kwa sasa kipenzi cha Watanzania tunakwenda kuwatendea haki Watanzania katika mazingira ya kuhakikisha kwamba Watanzania hatugawanyiki katika uchaguzi unaokuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja asilimia 100.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa James Mbatia ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwanza nilipongezi Bunge lako Tukufu ambalo lilipitisha Azimio la kukupongeza.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, anafanyakazi nzuri sana. Barabara za lami zimejengwa, huduma za maji, hospitali zimejengwa, vituo vyatya afya vimejengwa.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la barabara. Katika Mkoa wa Dodoma takriban Wilaya zote zinapitiwa na barabara za lami isopokuwa Wilaya ya Mpwapwa tu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika bajeti ya Mwaka 2019/2020 Bunge lilipitisha bajeti hapa; na bahati nzuri Wilaya ya Mpwapwa barabara ya kutoka Kongwa mpaka kwenda Mpwapwa ilitengewa fedha kwa ajili ujenzi. Hata hivyo, jambo la kushangaza ni kwamba mpaka sasa sioni dalili kama barabara ile inajengwa. Kwahiyao naomba Waziri wa Ujenzi atoe maelezo ni kwanini ile barabara haijaanza kujengwa, naomba atoe maelezo. Na ninashukuru kwa Mwaka huu wametenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakinia la pili ni kuhusu usambazaji wa umeme. Nimshukuru sana Waziri wa Nishati, kwa kweli katika Wilaya ya Mpwapwa takriban vijiji vingi vimepata huduma ya umeme isipokuwa bado vichache sana. Kwahiyao naomba sana katika vile ambavyo vimebaki vipate huduma ya umeme. Kwa mfano; Mkanana, Ngalamilo, Kibodiani pamoja na hiyo Kazania na Kigegeya ambayo sasa hivi mafundi wako kwenye site.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kuhusu huduma ya maji, naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji anipe maelezo kwa nini ule mradi wa maji wa mima wameu-*damp* tu hauna mwenyewe hakuna sioni dalili yetote. Kisima kimejengwa

hakuna *pump*, hakuna mapomba na Mima, Mheshimiwa Spika wewe unapafahamu sana ulisoma pale darasa la kwanza mpaka la tatu kwa hiyo, pale Mima sasa hivi kuna ongezeko kubwa la idadi ya watu naomba Waziri wa maji uhakikishe *pump* inapelekwa na mambomba na mradi ule unakamika haraka sana. Pamoja na miradi ya maji ya lhoma, Ndumila na Mzase.

Mheshimiwa Spika, la tatu nataka ninzungumzie kuhusu mwenendo wa bei, namuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, msikilize sana Waziri wa biashara, Serikali ni kweli haifanyi biashara na Serikali ilivunja tume ya bei. Lakini naomba Serikali iangalie sana suala la upatikanaji wa bei ya sukari, jana nimesoma gazeti jana wanasesma Serikali imesema kuna sukari ya kutosha katika nchi ya hii, sasa kama kuna sukari ya kutosha katika nchi hii kwanini bei imepanda mpaka 3600 mpaka kuna maeneo mengine mpaka shilingi 4,000. Kwa hiyo, Serikali itowe maelezo na itowe maelezo kuhusu utendaji wa viwanda vyta sukari katika nchi hii kwanini kuna uhaba mkumbwa wa sukari.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo jingine nimalizie, Mkoa wa Dodoma tunalima sana ufuta, lakini sasa hivi tatizo la ufuta Wilaya ya Mpwapwa inalima sana ufuta wamekatazwa ufuta uzitoke nje ya wilaya ya Mpwapwa na hivi karibuni wakulima wangu wanaoleta ufuta Dodoma wamekamatwa kwamba ufuta lazima uwekwe ghala la Gulwe, sasa ghala la gulwe kweli wanaweza kuweka kwenye ghala la Gulwe lakini hakuna mnunuzi nani atanunua na Serikali iwatafutie wanunuzi wakanunue huo ufuta.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Seneta.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, Ahsante naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa mniwie radhi wanaofuata wote twende kwenye dakika tano kwa sababu orodha ni ndefu kweli kweli ili *at least* kila mmoja apate angalau kufikisha ujumbe *straight* mtaona tumejaribu kutumia saa

moja sasa muda unaobaki twende kidogo jielekeze moja kwa moja ili ujumbe wako uweze kufika. Tunaanza na Mheshimiwa Ally Saleh, alafu Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante ndiyo nimekuwa mhanga wa mwanzo wa dakika tano. Ahsante sana nitazungumza mambo mawili matatu la kwanza nilichanganyikiwa juzi ama nifurahi ama ninyongeke tulipoambiwa tunasamehewa deni la *IMF*, kama mwananchi ningepaswa kufurahi lakini kama mwananchi niliona nimenyongonyea kwa sababu naamini nchi yangu ni tajiri ina uchumi mzuri inawezo wa kutosha kwa nini tusamehewe madeni. Lazima kuna tatizo ama kwenye mipango yetu dira, kwenye vipaumbele vyetu, kwenye *manage* uchumi au pia bajeti ya *deviations* ambazo nydingi zimekuwa zikitokezea.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo si uzuri kama nchi tuseme tunafurahi kusamehewa madeni kwasababu dawa ya deni ni kulipa, na sisi kama hatukujipanga vizuri ina maana kwamba hatufanyi vizuri katika nchi ndiyo maana tunategemewa kusamehewa kila baada ya kipindi.

Mheshimiwa Spika, Iakini la pili nataka kusema kwamba tunatatizo kubwa katika namna ambavyo tumetekeleza bajeti yetu hasa mpango wa maendeleo kwa muda wa miaka mitano iliyopita...

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Endelea sijui uko wapi ah! kwa Mheshimiwa Laigwanan!

## TAARIFA

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, naomba ni m-referkwenye msemo wa kingereza unaosema, *they is nobody too rich to received either their anybody too poor to give* kwa hiyo, kwa tafsiri isiyo rasmi hata tajiri kama amekopwa kwa mtu akirudishwa anahaki ya kupokea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Salleh!

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa hiyo kwasababu ina maana kwamba wewe kama umekwenda kukopa ulikuwa ujitätayarische kulipa dawa ya deni ni kulipa. Fadhila maana yake ukikopa ukirudishiwa utumwa wa kuendelea kukopa upo pale pale na kesho utakopa tena na baadaye utaenda kulia usamehewe.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala ya kwamba tumeshindwa katika maeneo mengi...

**MHE. ALLY KEISSY:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa zimekuwa nyingi mwacheni tu aendelee sasa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, kwa mfano tumeshindwa katika eneo la kupunguza vizazi na vifo kwa wajawazito, tumeshuka kiasi ambacho hatukuweza kufanikiwa lakini pia tumeshindwa kwenye suala la kusema tunaongeza kipato cha mtanzania tumeweka lengo kubwa la dola la 1,500 lakini tumeshindwa kulifikia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeshindwa katika maeneo mengine mbalimbali katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa hivyo mpango wa maendeleo ya miaka mitano ambao tunaumalizia hivi sasa, unamalizika mwakani umefanikiwa kwa kiasi fulani. Pia kuna maeneo mengi ambayo tungepaswa kama nchi kuwa tumepiga hatua lakini tumeshindwa na ni kwasababu hakukuwa na utekelezaji mzuri hakukuwa na mpango mzuri hakukuwa na *location* nzuri ya kifedha kuweza kuyakamilisha mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, na jambo jingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusiana na habari ya Zanzibar tulizungumza katika Bunge hili kwamba mambo mawili tungeyafanya kazi, la kwanza ni *double VAT* kwamba kunatozwa *VAT* mara mbili mtu anatoa Zanzibar kisha anakwenda kutoa Dar es Salaam ili limeshindwa kufanikiwa

mpaka hivi leo kwa hivyo tunasema kwamba hilo kwa Zanzibar linatalulalia mpaka hivi leo mzanzibari analipa kodi ya VATmara mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni suala la kumalizana deni la *TANESCO* la shirika la umeme la Zanzibar, kuna utata *ZECO*, kuna utata Serikali ya Muungano inasema au *TANESCO* inasema inaidai Zanzibar bilioni 149, Zanzibar inasema ni bilioni 10 hilo limeshindwa kutatuliwa mpaka tunamaliza miaka tano hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, na jambo la mwisho nataka kuzungumzia limezungumzwa sana hapa suala la kumsifia Rais wetu kwamba amefanikiwa katika mambo mengi na kwamba anaombewa kura ashinde kwa kishindo. Lakini tunasahau kwamba katika miaka mitano hii pamoja na sifa zote alizopewa Rais Dkt. Magufuli, lakini Rais Dkt. Magufuli hakuruhusu wapinzani kufanya siasa.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** ...kwa hivyo...

*(Hapa kengele illilia kushiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana muda hauko upande wako. Mheshimiwa James Mbatia atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa haraka haraka namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya njema na sote kuwepo hapa ya pili niwashukuru watanzania wote kwa ushirikiano waliotupatia katika kipindi chote cha Bunge na tatu nishukuru wa wananchi wa Jimbo la Vunjo kwa kuniweka hapa na kuwakilisha. Kipekee nishukuru *Vunjo Development Foundation* dhidi ya baba Askofu Dkt. Martin Flatei Shayo kwa kazi kubwa tulioifanya miundombinu elimu afya katika jimbo la Vunjo.

Mheshimiwa Spika, tatu Jimbo la Vunjo lina shule za msingi zaidi ya 144 na za Sekondari 74 mwaka jana tulivyokuwa tunafanya tathimini ya nchi nzima kule Arusha tarehe 13 na 14 Tanzania tuna tatizo la vyoo kwa takribani 60%. Je, bajeti hii na hii ni haki msingi ya kuweza kukuza utu wa binadamu leo hii karne ya 21 tuna tatizo la vyoo takribani 60% matundu ya vyoo. Hata mwaka jana Raís alivyokuwa kule Mwanza wanafunzi Mwanza mjini anasema wako 1,320 wana matundu ya vyoo 132 tu, wakati ni tatizo kubwa na linadumaza utoto wa watoto wetu. (*Makofí*)

Mheshimiwa Spika, upinzani siyo uadui, lakini kwenye bajeti hii na ninasema kwenye *authority* kabisa Waziri alivyowasilisha hoja yake hapa, Rais anasema maendeleo hayana chama lakini kwenye bajeti sisi wote tunalipa kodi lakini bajeti inasema wachaguliwe wale wenye vazi la kijani tu! (*Makofí*)

Mheshimiwa Spika, kwenye katiba tulioapa hapa Bungeni tuliaapa kuilinda na kuiheshimu Katiba ya Jamhuri na Katiba inakataza ubaguzi. Sasa inakuwaje tulipe kodi sote lakini kwenye uchaguzi na Rais anasema atahakikisha inatendeka kwenye uchaguzi na aliniambia hata mimi lakini serikali inaleta bajeti hapa inasema wakuchagua wakijani tu. Maana yake nini yani tunazungumzia umoja wa kitaifa, tunazungumzia Taifa lisifarakane, na wakati huu wa vita vyá kiuchumi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri tunatakiwa tuwe wamoja kama Taifa ili uchumi wetu uweze ukawa endelevu na unaokuza utu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwania njema kabisa suala la *COVID-19*, suala la *virusvyá Corona* ni janga la kidunia na tunakubali kabisa. Mtaalamu wa majanga ninajuwa kupata taarifa sahihi na kushiriki pamoja bila kugawanyika na nikiri hata Mheshimiwa Rais nilimshauri naye alilisema hadharani, kwamba wakati tukiwa kwenye vita vyá aina yoyote inhabidi tuwe ni kitu kimoja, tuwe na sauti moja, tushirikiane pamoja, Tanzania kwanza vyama baadaye, hivi vyama tunapitia tu katika kuhakikisha Tanzania inakuwa sehemu salama na nzuri zaidi pa kuishi.

Mheshimiwa Spika, sasa bajeti hii inaonekana kupeleka tunasahau jukumu la kwanza la kuipenda Taifa la Tanzania tunaenda kwenye misingi tu ya vyama vyaya siasa vyama vinapita tu lakini je, Taifa la Tanzania tunafanyaje tunajua Corona ipo na tupo kwenye vita, Corona ipo na inayoleta athari zaidi ni hofu, lakini kama Taifa tukijitahidi kutokuwa na hofu, tukijitahidi kutoa taarifa zilizosahihi zitasahidia katika kukuza uchumi wetu na uweze kuwa endelevu kwa maslahi ya wote.

Mheshimiwa Spika, watanzania inabidi tuwe na mifumo ya kodi ambayo inatabirika, mifumo ya kodi yenye ufanisi, mifumo ya kodi inayoaminika, hata ukiangalia kwenye bajeti hii na ukiingia sekta ya utalii ambapo 25% ya mapato yote ya Taifa yanatokana na sekta ya utalii fedha za kigeni, 25% ya fedha zote za kigeni zinatokana na utalii, tumeathirika sana kwenye sekta hii ukienda kwenye *hotel/zimefungwa* za kitalii, ukienda hali ya ajira ambazo zinatokana zaidi milioni moja kutokana kuajiriwa kwenye sekta ya utalii wapo vijiweni hali siyo nzuri sasa na dunia tukubali kwamba dunia hajjaweza kupata majawabu sahihi namna ya kupambana na Corona ikiwepo hata Marekani yenye na nchi nydingine zote.

Mheshimiwa Spika, sasa inabidi tutulize fikra zetu waingereza wanasema au John Galan alitufundisha kwamba *you fight while you talk and you talk while you fight*, sasa tuunganike pamoja kuwa na fikra ambazo ni endelevu tuwe pro-active tuisubiri kuwa reactive na hii inatuleta pamoja hii ni vita ni yetu sote. Sasa tukiri kwamba tatizo lipo na kwa kuwa tatizo lipo basi tuwe wamoja. Badala ya kufarakana, badala ya kuingiza *cheap politics* katika masuala ambayo ni muhimu kwenye maslahi endelevu ya Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye kodi naomba tujenge mifumo ya *TRA* ambayo ni endelevu. Mifumo ya *TRA* yenye kutoa haki, Taasisi ambazo ni imara na kwa kuwa tumetekeleza lengo la 16 la malengo endelevu ya dunia. Tukiri hali ya tabia ya nchi, miundombinu ya Taifa letu ipo kwenye hoi bin taaban ambayo imeleta athari kubwa katika nchi, na hiyo inaathiri pia uchumi wa Taifa la Tanzania sasa namna

gani tunawekeza kwenye miundombinu hii tukiwa wamoja na kwa kuwa Rais anasema na naamini hivyo maendeleo hayana chama ambayo yanatakiwa yahudumie watu wote bila ubaguzi wa aina yoyote.

Kwa kuwa sheria inaruhusu sote tuwepo ndani ya Bunge hili, sote tunaruhusiwa kuwa Watanzania basi tuhakikishe tunatelekeza yote haya kwa lengo moja kwenye wimbo wetu wa Taifa kulinda hekima, umoja na amani ili tukiingia kwenye uchaguzi, uchaguzi ni tukio tu uchaguzi ukipita Tanzania bado inaendelea kuwepo kwa hivyo tuwe wanasema *great minds discuss issue but ordinary minds discuss event but simple minds discuss ideas. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru sana Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Joseph Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Rombo walio ndani ya Wilaya na walio nje. Pamoja na Viongozi wa Dini na Wadau wengine, Viongozi wa Serikali, Madiwani na Viongozi wote walio Rombo kwa kuniwaita na kuniwezesha kufanya kazi yangu kwa kipindi chote ambacho nilipata ridhaa kama Mbunge wa Jimbo la Rombo. Tumeshirikiana vyema katika mambo mbalimbali wananchi walishiriki katika miradi ya shule, shule za sekondari, shule za msingi walishiriki katika ukarabati wa Zanahati na Vituo vya Afya, ujenzi wa Vituo vya Polisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vilevile naishukuru Serikali. Serikali imetusaidia katika miradi kadhaa ya maendeleo ninakumbuka ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo inajengwa sasa hivi, Hospitali ambayo ilikuwa inasubiriwa muda mrefusana na wananchi. Vituo vya Afya kadhaa, ujenzi

wa visima vya maji na mradi mikubwa ya maji inayoendelea sasa hivi, mradi wa Tarakea na mradi wa kule Lekchala n.k.

Mheshimiwa Spika, nimesema hayo machache kwasababu ya kuonesha ulimwengu na hasa wale wanaosema kuwa sisi wapinzani tukichaguliwa maendeleo hayaletwi kwenye Majimbo yetu. Kwamba Serikali hii imehudumia karibu majimbo yote na hii inathibitisha kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli anaishi kauli yake kuwa maendeleo hayana chama na kwa hili nampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa asilimia kubwa, bajeti hii fedha nyingi zimekwenda kwenye miradi mikubwa ya maendeleo kama *SGR* na *Stigler's Gorge*. Uzoefu wangu hapa Bungeni unaonesha kuwa nchi yetu imekuwa na matatizo makubwa sana kwenye miundombinu ya barabara na reli. Ni kweli kuwa baada ya Serikali hii ya Awamu ya Tano kukamilisha viporo vingi vya miradi kama miradi ya mwendokasi, *flyovers*, barabara kadhaa kama hii ya Dodoma kwenda mpaka Moshi, mradi wa *SGR* utakuwa suluhisho kubwa kwenye tatizo hili. Utapunguza ajali barabarani, ubebaji wa ng'ombe, mbao, *cement*, binadamu, makaa ya mawe n.k.

Mheshimiwa Spika, na kwa kutumia usafiri wa barabara. Muda wa kukaa barabarani utapungua, biashara za mazao zitapata ufanisi na wanyonge ndio watanufaika sana. Ajira zitaongezeka na vilevile mapato ya halmashauri pamoja na mapato ya Serikali Kuu yataongezeka. Wigo wa Kodi utaongezeka na kwa hiyo, huduma za Wananchi zitakuwa zimeboreka.

Mheshimiwa Spika, katika hili siwezi kumpa sifuri Mheshimiwa Dkt. Mpango, nitamuachia PHD yake na kumuombea Mwenyezi Mungu aweze kurudi hapa ilia je amalizie miradi hii aliyoianzisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kubwa katika nchi yetu ni umeme. Lakini sote ni mashahidi Wabunge karibu wote

miradi ya REA imekwenda kwenye Majimbo yetu. Na pale Jimboni kwangu ni vijiji vichache sana vimebaki sasa hivi kunaendelea na miradi ya *desintification* kwa hiyo, mradi kama wa *Stigler's Gorge* ingawaje wengine hawaungi mkono. Naunga mkono na ombi langu tu ni kuhakikisha kwamba mradi huu umetekeliza kwa ufanisi tuweze kupata huo umeme kwasababu umeme ukipatikana ni wazi uwekezaji utakuwa mkubwa na uwekezaji ukiwa mkubwa ni kwamba ajira zitaongezeka mauzo ya nchi nje yataongezeka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali itapata pia uwezo wa kuwahudumia wananchi wake. Katika bajeti nimesikia zimetengwa fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara ambazo zimeharibiwa na mvua nyngi zilizonyesha katika msimu huu. Naiomba sana Serikali hata katika Jimbo langu kule Rombo barabara nyngi sana zimevunjika naomba sana Serikali isiache kutoa hizi pesa izitoe kwa wakati ili ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba, dakika moja Mheshimiwa. Mwisho niseme tu kwamba upinzani sio uadui na sio dhambi kupongeza jambo zuri ambalo limefanyika. Tujenge tabia ya kufanya kazi kwa kuangalia nchi badala ya kuijangalia sisi wenyewe. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Roman Selasini. Mheshimiwa Naghenjwa Mwenyekiti *PAC* atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel. Halafu Mheshimiwa Salma Kikwete atafuatia.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa vile ni dakika tano, najua utanipa dakika mbili zaidi kuzungumzia jinsi wewe mwenyewe ulivyotusa idia kwenye Kamati yetu ya *PAC* kwa wale Maafisa Masuuli amba walitaka waepuke kikombe chetu cha kuja mbele yetu na uliwakatalia wakawea kuja kwenye Kamati zetu, kwa hiyo nakushukuru kwa hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, nawashukuru Sekretarieti yetu Erick Maseke na Magova kwa jinsi ambavyo waliisaidia sana Kamati yetu kufanya tulyofanya. Kwa vile ni mara ya mwisho kwa mimi kusimama katika Bunge lako hili, niombe kwa heshima na taadhima nisingependa kwamba Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani ambaye hayuko hapa Mheshimiwa Freeman Mbewe asemwe vibaya wakati hayuko hapa. Kwanza nimpe pole kwa yote yaliyomfika na tujue wote hapa hata mbele ya Mungu kila mtu ana udhaifu wake yakianikwa hapa kwa kweli hakuna atakayepona. Kwa hiyo tukumbuke hayo maana hata Mheshimiwa mwisho aliongea kumwita mlevi ajue kwamba hata siye tungesimama kusema yake kwa kweli tungekuwa tumemvua nguo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwashukuru wapigakura wangu wote wa Same Mashariki na niwaeleze kwamba ile barabara ambayo ilikuwa ni mwiba ya kutoka Same Kisiwani mpaka Mkomazi, Rais alinipigia simu wakati tukiongea mambo ya PAC na akaniuliza ile barabara ambayo ilikuwa ahadi yake ilishatengenezwa nikamwambia bado, akatoa maagizo na akasema niandike barua kwenda kwa Waziri wa Ujenzi nakala nimpelekee na nikafanya hivyo na ninayo hapa barua iliyopokelewa lkulu kwake. Kwa hiyo najua kwamba barabara hii kwa vile imeshatengewa bilioni tano itaanza kutengenezwa na ameahidi kwamba itatengenezwa yote mpaka iishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie Madiwani wetu; Madiwani wetu wengi wametoka wakiwa hawajalipwa mafao yao, kama Wilaya ya Same Madiwani wote miezi mitatu hawajalipwa posho zao hawajalipwa kiinua mgongo chao. Kwa vile Waziri Mkuu yuko hapa, tunaomba aseme kwamba hawa watu ambao wametumikia nchi hii na naamini ni sehemu nyingi katika nchi nzima Madiwani hawajalipwa, watalipwa lini haki zao, maana hata siye Wabunge hatutafurahi tuondoke kama hatujalipwa haki zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nipende pia kuongelea kuhusu Wizara ya Kilimo, wengi wameongelea na jinsi ambavyo

imepewa hela kidogo, lakini nieleze pesa nyangi zinapotea kwa hizi bodi ambazo zimeundwa na Serikali. Bodi hizi zimekuwa zote isipokuwa ile inayohusika na mazao ya jumla zimekuwa zikifanya hasara kubwa. Sasa kama zimefanya hasara kubwa kwa nini hizi Bodi nyangi za Chai, Pamba, Kahawa na Korosho kwa nini tuwe na mtitiri wa bodi ambazo hazifanyi kazi kwa faida. Ina maana hawa ni viwavi, wanakula hela nyangi ya wakulima na wana faida.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie mashirika yetu yote ya umma ambayo yanafanya vibaya sana, yanapata hasara, yanatumia pesa za wananchi. Angalia benki zetu, benki zimekuwa zikifanya vibaya sana. *TIB*, benki hii imekuwa ikifanya vibaya sana inapata hasara imeshindwa hata kukusanya madeni kwa maana kwamba imetoe fedha kwa watu ambao wanaonea aibu kuwadai kulipa pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa benki kama hizi nasikia tetesi kwamba zinataka ziunganishwe na Benki ya Posta. Ikumbukwe kwamba Benki ya Posta ilikuwa inakufa, ndio inafufuka sasa hasa hapo ilishaongezewa mzigo wa *Twiga Bank*, imeshaongezewa tatizo la kupelekewa Benki ya Wanawake ambayo ilikuwa haifanyi kazi na hata hivyo ikairudisha nyuma kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa hizi benki zinazofanya vibaya iweje uzichukue ukaunganishe na benki ambayo ndio inafufuka. Hii ni sawa na kuwa na mgonjwa hospitali yuko *ICU* halafu unachua mgonjwa mwenye nafuu unawalaza pamoja ukitegemea yule wa *ICU* apone. Kwa kweli mimi nasema hakika Serikali itakuwa haitendi mema. Naomba sana hizi bodi zote zivunjwe...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naghenjwa.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makof)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ruth Mollel halafu Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja hii. Kwanza nimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii na pia kwa Bunge langu la mwisho ningependa kushukuru chama changu, ningependa kushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama changu kwa kunipa nafasi ya kulitumikia Bunge hili pia ningependa kumpa pole sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu ambaye anaumwa yuko Aga Khan.

Mheshimiwa Spika, tukiwekea video hapa ya kila mtu na maisha yake hapa Bungeni, nafikiri wengi wetu tutaingia chini ya viti. Kwa hiyo, naona kwamba kuwa *personal* sana kwenye masuala hayo si jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza na nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Mpango na nimeona ameorodhesha mafanikio...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel kuna taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza sisi hapa Wabunge wote asilimia 99 tuna maisha kama binadamu wengine, asilimia moja tu ndio Ubunge tulionao na tuna maisha kama binadamu wengine. Tatizo lilioko watu kuchanganya mambo yao ya mtaani kutafuta *political sympathy*, hicho kitu ndio hatukitaki. Mwenyekiti amefanya mambo yake ya hovyo anataka kudanganya umma kuwa masuala ya siasa ndio yamepelekea kupatwa na ule mkasa. Tukubaliane yeye alilewa na mkitaka ushahidi muulizeni Joyce Mukya ndio alikuwa naye. Kwa hiyo jambo hili liszungumziwe ninyi ndio mnaosababisha tuzungumze hilo jambo asante sana.

**SPIKA:** Yaani anachosema, Mheshimiwa Msigwa taarifa yake ndio imeleta vurugu yote hii, kwamba mtu alikuwa na mambo yake mengine Msigwa analeta mambo mengine, kusema sijui kavamiwa na watu gani, sasa pale ndio unaleta shida, lakini ukisema nilikuwa nimepiga masanga nikananii mguu, nani atakusonga, kwa sababu kunywa pombe ni kitu cha kawaida, tatizo *mix up* ya *information* lazima tuwe *consistent*, hatutapata matatizo haya. (*Makofii*)

Endelea Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, naomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Mpango na ameainisha mafanikio mengi sana ambayo yamepatikana katika awamu hii au katika mwaka huu na kuwa eneo la utawala bora na mambo ya kuzuia rushwa ameainisha mafanikio. Katika kutoa taarifa huu watu waliosababisha haya mafanikio ni watumishi wa umma na watumishi wa umma hawajatajwa kabisa katika hii ripoti, ni kwa jinsi gani watumishi wa umma katika awamu hii ya miaka mitano wameweza kufaidika, hakuna mahali popote palipozungumziwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba hawakuzungumziwa kwa sababu watumishi wa umma kwa kweli safari hii wamepata shida, hata zile *increment* zao za mwaka hawakupata, hawakupata nyongeza za mshahara pamoja na kwamba *inflation* iko *one digit*, lakini ukienda sokoni habari ni tofauti utakuta nyanya kilo 3,000 ata chelewa 3,000 kwa maisha ni magumu sana kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba wengi katika Bunge hili wenye kura nyingi wameshindwa kabisa kuwatetea watumishi hawa kusudi waweze kuongezewa mishahara, kwa hiyo wametoka kappa kabisa mwaka huu. Vilevile katika kutajwa kwao wametajwa hela wanazodai kwa mfano watumishi wanadai bilioni 1.3, halifu wanadai madai ya

kimshahara bilioni 114 mpaka leo, ni kwa nini kusiwekwe mfumo ambao utadhibiti madai haya. Kuna TEHAMA kwa nini tusitumie TEHAMA kuhakikisha kwamba masuala ya madai hayajitokezi tena ili kupunguza adha ya kukaa na kuhakiki na kunyima watumishi madai yao.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuonyesha sera za bajeti kwa sasa hivi ameainisha mambo mengi ambayo atayafanya ambayo ni mazuri, watumishi wamepunguziwa *pay as you earn*, lakini katika wasilisho lake hakuna mahali popote ameonyesha kama angalau kwa bajeti hii 2020/2021, watumishi wa umma watakuwa hata na nyongeza ya mshahara, watenge pesa kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Najua kuna miradi ya vielelezo, lakini bado Serikali inaweza ikatenga pesa kwa ajili ya watumishi pamoja na hiyo miradi, sio lazima hiyo miradi iishe mwaka huu au mwaka kesho, *it can be done a long term* ikatengwa pesa kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, zamani sisi watumishi tuliofanya kazi Serikalini, ulikuwa unahemeahemea kwenye visafari kwa sababu mshahara hautoshi, siku hizi hamna safari, hamna chochote, watumishi wana shida kubwa, lakini naona Bunge lako Tukufu hatujawatendea kazi watumishi hawa. Kwa kweli naondoka katika Bunge hili kwa masikitiko makubwa sana...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa pokea Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Dkt. Mary.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimtaarifu mzungumzaji anayeongea dada yangu Ruth Mollel kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga vizuri na inathamini sana watumishi wa umma. Nikitoa takwimu chache tu kwa ufupi ni kwamba katika kipindi cha miaka mitano Serikali ya Awamu ya Tano imeshaajiri watumishi zaidi ya 74,000,

wakiwemo na Madaktari 1,000 na Walimu kwa kipindi cha miaka minne zaidi ya 6,300. Pia kila mwaka wa fedha tumekuwa tukitoa ajira na kwa upande wa *arrears* zaidi ya bilioni 130 za watumishi walio makazini zimelipwa hadi Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, vilevile *increment* huwa zinalipwa kila mwaka na tokea mwaka 2017 baada ya lile zoezi la uhakiki lakini hata wale *masters holders* sasa hivi wanakuwa *considered* katika kulipwa hizo *increments*. Suala la malipo ya pensheni hii inashughulikiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote watumishi wa umma wote *apart from* ile mishahara wanayopewa, lakini tumetoa *policy* kwamba kwa waajiri wote waweze kutoa *incentive policy* juu ya watumishi hawa sio tu mishahara, ni kwa mfano, vitu kama nauli za likizo na kuna vitu kama fedha ya kujikimu. Pamoja na hayo madaraja yanapoongezeka moja kwa moja *automatically* hata mishahara inaongezwa...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, zaidi ya watumishi 290 wameongezewa madaraja. Nilikuwa nataka nimjibu Mheshimiwa Ruth Mollel

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ruth Mollel umetoka siku nyingi Serikalini alikuwa anakukumbusha tu. Endelea na mchango wako

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Katibu Mkuu Mstaafu na maneno yote hayo anayonieleza sijui nini, sijui nini *the truth of the matter* hawajawaongeza watumishi mishahara. Kama ni hizo *arrears* ni haki yao hawajawalipa; kwa hiyo mishahara haujaongezwa *annual increment* nina ndugu anafanya kazi hawajawapa

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa iko wapi? Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba ni vizuri Dkt. Mpango atumie siku ya kesho ya Jumapili kwenda kutubu Kanisani kwa sababu Serikali ni kweli kabisa haijaongeza mishahara kwa watumishi wa umma na sasa hii ni bajeti ya mwisho ya Serikali ya Awamu ya Tano.

**SPIKA:** Mbona huna unachokiongea Mheshimiwa Haonga zaidi ya kuleta fujo. Mheshimiwa anakuvuruga tu huyu bwana, maana yake haongei unachokiongea wewe.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa yake kwa mikono miwili (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Jamii, hii Mifuko ya Jamii ndio pensheni za watumishi, Serikali inadaiwa bilioni 171.9. Athari zake ni nini; athari zake ni kwamba wale wanaostaafu sasa hivi wanakaa miezi sita hawajalipwa ile *gratuity (lump sum)* yao kwa sababu Serikali inadaiwa. Ni kwa nini Serikali hailipi haya madeni kusudi watumishi wanaostaafu sasa waweze kupata *lump sum* zao na kuifanyia kazi kablal hawajachukuliwa hapa duniani...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, hiyo si sawasawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Ruth Mollel, hayo anayoyasema si sahihi kwamba Serikali hailipi. Kwa mfano, Mfuko wa PSSSF, wanachama wake asilimia kubwa ni watumishi wa umma ambao ni Walimu, asilimia 50.8 ya

watumishi wa umma ni Walimu *automatically* hao pia ni wanachama wengi kwenye Mfuko wa PSSSF.

Mheshimiwa Spika, tulipounganisha Mifuko hii mwaka 2018 tulikuwa na madai, kwa mfano kwenye kundi hilo kubwa la Walimu ambao walikuwa ni Walimu 17,660 waliokuwa wanadai fedha kwenye Serikali jumla ya fedha za Kitanzania triliioni 1.4. Mpaka sasa mwezi huu wa Juni tumekwishakulipa triliioni 1.2 na tumebakiba na bilioni 215.6. Kwa hiyo sio kwamba Serikali hailipu, tumekwishalipa na baada ya kulipa hizo maagizo ya Serikali ni mpaka mwezi wa nane bilioni 215.6 zitakuwa nazo zimekwishalipwa. Kwa hiyo siyo sahihi kwamba hatujalipa hizo fedha.

**SPIKA:** Ilikuwa ni taarifa kwako japo muda umeisha kwa dakika moja tu nakupa ili upokee taarifa.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, *issue* hapa ni kwamba sasa hivi watumishi ambao wanastaafu hawapati *immediately* ile *lump sum* yao. Wale waliostaafu zamani wanaendelea, mimi naendelea kupata pensheni yangu, namshukuru Mungu, wale wanaostaafu sasa hivi hawapati ile *lump sum*, kwa nini inachelewa na mifumo ipo ya kufuatilia mtu anapotaka kustaafu, hiyo ndio *issue* kubwa iliyopo hapo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Mboni Mhita na Mheshimiwa James Millya.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja katika Wizara ya Fedha na Mipango kutoka kwa Dkt. Philip Mpango inayohusu mapendekezo ya Serikali na mapato kwa kipindi cha mwaka 2020/2021. Kwanza kabisa naomba nipeleke shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu ambaye amenipa kibali cha kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kuchangia hoja, leo tarehe 13 Juni, 2020 kama ambavyo alinipa kibali tarehe 4 Aprili, 2017 mara tu nilipoapishwa na wewe Mheshimiwa Spika kwa uteuzi wa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwake kwa nafasi zile kumi ambazo mionganoni mwao mimi alinipa nafasi hiyo. Namshukuru sana na hii historia ambayo ameiweka kwangu kwa kweli itakuwa ni historia endelevu kwa kizazi hiki na kizazi kijacho, kwa sababu nilikuwa mke wa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, nashukuru kwa heshima hii kubwa ambayo amenipatia. Pia nikushukuru wewe binafsi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya pamoja na wasaidizi wako kuliongoza hili Bunge kwa umahiri mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pongezi nydingi zimwendee Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ndani ya Bunge letu na nje ya Bunge. Kwa kweli Mheshimiwa anastahili tuzo, Wanaruangwa nawaomba wakupe tuzo na sio tuzo nydingine bali ni tuzo ya ushindi mkubwa wa kishindo pale tutakapoelekea kwenye uchaguzi hongera sana.

Mhesimiwa Spika, sambamba na hilo nipeleke hongera zangu nydingi kwa mama Samia Suluhu Hassan. Sasa nimalizie kwa baba yetu, baba lao Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli amefanya kazi kubwa, nydingi na nzito na zinazoonekana katika Taifa letu hili la Tanzania. Kwa kweli Dkt. John Pombe Magufuli ameitekeleza kwa vizuri na weledi mkubwa llani ya chama chetu Chama cha Mapinduzi. Hongera sana kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango. Mheshimiwa Dkt. Mpango umefanya kazi kubwa na nzuri. Umewasilisha vyema hotuba yako. Hotuba hii ni hotuba ya Watanzania kutokana na mambo mengi yaliyofanyika katika kipindi cha miaka mitano; 2015 – 2020. Unastahili pongezi za dhati.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba niende kwenye eneo la afya, ukurasa wa 18 aya ya 26. Afya ni haki ya kila mtu, afya ni haki ya kila Mtanzania. Afya ndiyo

inayojenga uimara wa mwanadamu kuweza kufanya kazi yake kwa umahiri na kwa weledi mkubwa. Kwa kweli mmeefanya kazi nzuri katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, tukianzia tu, Zahanati 1,118 zimepatikana, Vituo vya Afya 417, Hospitali za Halmashauri 71, Hospitali za Rufaa kumi, sambamba na Hospitali za Kanda tatu na kazi nzuri zimeonekana. Ushauri wangu tu kwa Serikali, ushauri wangu kwako Mheshimiwa Dkt. Mpango ni kuhakikisha kwamba yale maboma ambayo yamebakia ni kuendelea kuyamalizia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maboma hayo, tumejenga maeneo mengi mazuri kwenye hospitali zetu nchi nzima. Ushauri wangu mwingine ambao unakuja kwako ni kuwapeleka wataalam hawa kwenye eneo la elimu. Elimu imepata mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye elimu, kama nilivyosema, afya ni haki ya msingi, ninachokuomba, kwenye elimu vilevile wekezeni kwenye eneo la watoto wenyе mahitaji maalum, nao wana mahitaji yao ya msingi, hasa wale...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, umalizie.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nitaandika kwa maandishi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Umenikumbusha, ningewashauri Waheshimiwa Wabunge mliong wengi mwandike kwa maandishi michango yenu kwa sababu kwa kweli leo kila mtu anataka kuzungumza. Kwa hiyo, nina orodha hapa ni ndefu kuliko maelezo.

Mheshimiwa Mboni Mhita, Mheshimiwa James Millya halafu atafuata Kamishna Mheshimiwa Turky.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Naomba nitumie fursa hii kwanza kumshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na wewe Mheshimiwa Spika, kwa uongozi ambao ni wa mfano. Nina hakika sisi vijana tunaendelea kujifunza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepata mafanikio makubwa sana ambayo ni dhahiri kwamba inabidi tuendelee kujivunia. Ukiangalia kwenye Sekta ya Uchumi, ukiangalia miundombinu, ukiangalia huduma ya jamii, yako mengi ya kuendelea kujivunia. Siyo kwa bahati nasibu bali kwa jithada kubwa ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya tano ambayo imeendelea kutekelezwa katika kipindi hiki cha Serikali ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli na tumeendelea kushuhudia kuwa ni bajeti yenye tija. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, hasa kwa uongozi wake katika kipindi ambacho dunia nzima ilikuwa kwenye taharuki ya mlipuko wa janga hili la *Corona*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amedhihirisha siyo kwa Tanzania tu, bali kwa Afrika na dunia nzima kwa ujumla kwamba yeze ni Rais wa mfano kwa maamuzi yake ya kutoifunga nchi na kuhakikisha kwamba nchi haiingii kwenye *total lockdown*, hakika ameokoa uchumi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuifunga nchi na kufanya nchi iwe kwenye *total lockdown* kungeweza kuathiri shughuli za uzalishaji kwa asilimia kubwa sana. Kama tunavyozungumzia kwamba Tanzania ni nchi ya viwanda leo hii, zile ajira zaidi ya 400,000 ambazo ni mpya kwenye Sekta ya Viwanda, wale wote wangezikosa na ni dhahiri kwamba uchumi ungeweza kuathiriwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Jarida la *The African Report* limemtaja Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kuwa ni mionganoni mwa viongozi bora *top ten* katika viongozi 50 ambao wamewafanyia *research*. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yupo kwenye namba tisa ya viongozi 50 wa Bara la Afrika ambao wamefanyiwa *research* kwa viongozi ambao wameleta mabadiliko chanya kwa Bara la Afrika na dunia nzima kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, dunia imemtambua Mheshimiwa Rais, Afrika imetambua uwezo wake, sisi wanachama wa Chama cha Mapinduzi tunamtambua Mwenyekiti wetu uwezo wake. Wenzetu wa upande wa pili wanapata kigugumizi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo hii wakati wa janga la *Corona* nchi nyingi ziliweweseka, viongozi wengi walishukta na kushindwa kufanya maamuzi sahihi na kuingia kwenye janga kubwa la kuchukua mikopo yenyenye riba kubwa na *destabilize* uchumi wao. Leo hii msimamo wa Mheshimiwa Rais ambao alisema badala ya Mataifa makubwa kujaribu kutumia janga lile kujinufaisha kwa kurubuni nchi ambazo zina uchumi wa kuendelea kukua na kutuletea mikopo yenyenye riba kubwa, basi watupunguzie au tupate ahueni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, halafu unakutana na Mbunge wa Upinzani anayejitambua, anasema kwamba inakuaje Tanzania tunasamehewa? Anashindwa kujua na anashindwa kuelewa kwamba vigezo vyahuyu kusamehewa mikopo ni pamoja na ukuaji mzuri wa kiuchumi na utumiaji mzuri wa fedha ambazo zimetolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mashirika yale yanatoa *loans* na *grants*. Yana uwezo wa kubadilisha *loan* ikawa *grant* muda wowote, kwamba tulitoa fedha hizi kama mkopo, lakini kutokana na...

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Ally Saleh.

## TAARIFA

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mbunge anayezungumza kwamba hoja yangu haikuwa kwamba, sijui kama nchi inaweza kukopa kitu gani? Hoja yangu ni kwamba umefikaje mpaka kwamba deni hujalipa unategemea uje ulipwe; ni utumwa ambao ni endelevu. Ndivyo nilivyosema.

**SPIKA:** Taarifa yako Mheshimiwa Mboni Mhita.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa kwa sababu inaonekana hana hoja. Alitaka kutumia dakika zangu na hawesi kunitoa kwenye reli nikiwa katika mmomonyoko wa kuendelea kupongeza jitihada na kazi za Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende sasa kwenye *performance* ya bajeti, ni jinsi gani ambavyo bajeti ya nchi imeteklezwa. Kwa makadirio ya mwaka wa fedha 2019/2020 yalikuwa shilingi trillioni 33....

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mboni, muda tayari hauko upande wako.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika mbili.

**SPIKA:** Dakika moja.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, kwa dakika moja naomba nitume fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Handeni Vijijini kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao. Natumia fursa hii pia kuwaambia kwamba panapo uhai na majaliwa natia timu katika uchaguzi huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakupongeza sana kwa uongozi wako uliotukuka. Sisi vijana tunaendelea kujifunza kwako. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mboni Mhita, nakushukuru sana. Mheshimiwa James Millya atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale kwa upande wa *CUF*.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kabisa, kwa bajeti nzuri, tunakwenda kuhitimisha miaka mitano ya Ubunge wetu, nasi watu wa Simanjiro tutawakumbuka wewe na Mheshimiwa Rais kwa ujenzi wa ukuta wa kipekee nchini mwetu, ukuta wa Mererani.

Mheshimiwa Spika, miaka mitano iliyopita Mererani pale, yale madini ya *Tanzanite* tulikuwa tunakusanya shilingi milioni 64 peke yake kwa mwaka. Mpaka bajeti hili inapoenda kwisha tunapokea takribani shilingi bilioni mbili kwa ajili ya *Tanzanite*. Haya ni mafanikio makubwa yaliyofanywa kuitia Kamati yako Kuu uliyoienda ya kuchunguza biashara ya madini ya *Tanzanite*. Nasi watu wa Simanjiro tunawashukuru ninyi; wewe pamoja na Mheshimiwa Rais kwa sababu haya ni mapinduzi kwenye madini pekee yaliyopo duniani ambayo hayako popote ila Simanjiro peke yake. Tunawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna changamoto mbili tatu ambazo tayari nimeziwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu mambo ya kodi yanayolalamikiwa na wachimbaji wadogo wa Mererani na nimeambiwa kwamba wiki ijayo nitapewa nafasi waje wakae na Serikali kwa ajili ya kutatua matatizo machache, lakini mimi kama Mbunge wa Simanjiro niendelee kuishukuru Serikali hii iliyofanya mapinduzi makubwa kwenye madini ya *Tanzanite*, hakika tunaendelea kuweka heshima kwa ajili ya madini yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi Simajiro kwa miaka hii mitano tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais. Tumefanikiwa karibu kilometa 18 za lami kutoka *KIA* mpaka Mererani na juzi wiki iliyopita tunakwenda kujengewa karibu

kilometa tatu mji mdogo wa Orkesumet. Haya ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo, tunajengewa mradi mkubwa wa maji ambapo ingekuwa kama siyo mafuriko, shilingi bilioni 41 kupeleka maji Mji wa Orkesumet na shilingi bilioni tano kupeleka maji Mji mdogo wa Mererani. Hakika Serikali ya CCM inafanya kazi kubwa sana, nami kama Mbunge nawashukuru.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita tumezindua Hospitali ya Wilaya kati ya zile 67 na sisi tumebahatika. Tuna kila sababu ya kuishukuru Serikali hii iliyofanya maajabu ambayo hata sisi Wamasai hatukufikiri kama itapatikana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amepokea nchi ambayo ina amani, ameendeleza amani hiyo mpaka leo. Majeshi yetu yanalinda nchi yetu, amepokea kutoka kwa Mheshimiwa Rais Kikwete. Kuna nchi ambazo kwa miezi mitano tu hazitawaliki, lakini Mheshimiwa Rais amesimamia amani ya nchi hii na sisi ambao ni wazalendo lazima tuiheshimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe Watanzania, miaka michache iliyopita pale Kibiti na Amboni, Tanga palikuwepo na mambo ambayo yalitaka kutokea kama ya *IS/IS*na mambo ya ugaidi. Mheshimiwa Rais kwa Jeshi letu imara la Tanzania wamesimamia vizuri, nchi hii ina amani mimi naishukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sasa wadau wa maendeleo kutoka mataifa yote; Marekani, Uingereza na wengine wote watambue jitihada hizi kubwa zilizofanywa na Serikali ya CCM chini ya kiongozi mahiri, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na watunge mkono kwamba Tanzania inajimudu, imejiweza na inaweza kusimamia mambo yake yenye.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri alinifurahisha kwa jambo moja kubwa sana. Kwenye

ule ukurasa wa 146; pamoa na kwamba ametaja mambo ya afya, mambo ya maji, mambo ya elimu na mafanikio makubwa, vile vile alitaja ille suala la mkuki wa sumu, hakika hili limetufurahisha Wanayanga, kwa kweli Mheshimiwa Waziri nakupongeza kwa sababu mafanikio ni makubwa sana. Nasi wanamichezo tunaipongeza sana Timu yetu ya Yanga, kwamba mkuki wa sumu ulilingia na hakika CCM iendelee kuendeleza michezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Millya, naona muda wako...  
(Makofi/Kicheko)

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri amegusia suala la Sekta Binafsi. Hakika amesema changamoto peke yake inayokuja kwa miaka mingine mitano ijayo asaidie sekta binafsi, hasa mfano nilligusie suala la *insurance*. Unakuta *insurance* lnachukuliwa na *NIC* lakini makampuni binafsi yanayofanya u-broker yote hayapewi biashara.

Mheshimiwa Spika, mfano makampuni madogo madogo ya Watanzania kipindi cha miaka mitano ninaomba Wizara hii iangalie ni namna gani Sekta Binafsi itaangaliwa ili Watanzania wale mabilionea watokee mionganoni mwetu. Tuangalie kampuni za Watanzania, tuziangalie vizuri biashara kwa sababu kwa kufanya hivyo tutawainua Watanzania wengi, tutapata ajira, tutawaajiri watakuwa na nguvu ya kushindana duniani. Tukiminya Sekta Binafsi tutawaumiza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba hili liangaliwe, Sekta Binafsi ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Serikali ipate biashara lakini tusiwasahau wenzetu ili wapate mchango na kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, bajeti hii ni ya mfano, ni ya kipekee, hakika Mkoa wa Manyara, Mikoa wa Arusha tutakuja wote bila Wapinzani. Nina hakika majimbo yote yatashinda CCM.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa James Millya. Mheshimiwa Turky, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya kuweza kuchangia bajeti hii. Nitaanza na hoja ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi hususan wafanyabiashara wa Zanzibar na Bara pia, kuna tatizo kubwa sana la VAT. Tumebadilisha mfumo wa VAT. Mfumo wa VAT sasa hivi ukifanya biashara baina ya Bara na Visiwani kinachotokea ni kwamba wafanyabiashara wanaoagiza mzigo kutoka nje wakaleta Tanzania Bara wanalipa VAT. Sasa unapotoka mfanyabiashara kwenda madukani kununua vitu vile, unaponunua mzigo ule ili kupeleka Zanzibar, kwa hiyo, VAT ile inatakiwa kwa njia yoyote nyingine ibaki huku huku Bara kwa sababu risiti ile ikifika Zanzibar haitambuliwi na badala yake unaambiwa Zanzibar ulipe tena VAT.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika na Zanzibar mtu ye yeyote akinunua mzigo wowote akileta Bara, basi naye hata kama amelipa VAT Zanzibar na Bara anatakiwa alipe tena VAT. Sasa hili kwa kweli ni tatizo ambalo linakera sana katika ukuaji wetu wa biashara. Namwomba sana Waziri wa Fedha aliangalie tatizo hili, ikiwezekana turudi katika mfumo wetu wa zamani au toboreshe njia yoyote ambayo tunaona inafaa.

Mheshimiwa Spika, la pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano, ameendeleza sana viwanda. Katika viwanda ambavyo vinakuja kwa kasi sana ni viwanda vya mifuko mbadala. Kwa muda mfupi sana viwanda hivi vimikuwa vingi sana na vinatosheleza nchi yetu, lakini changamoto ya viwanda hivi ni kwamba uzalishaji wao unapata taabu kutokana na mifuko inayotoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeangalia katika bajeti ya Serikali sikuona namna ya kulinda mifuko hiyo. Wakati fulani Mawaziri wetu wa Mazingira walitoa kauli kwamba pale watahakikisha kwamba mifuko hii ya nje inadhibitiwa na kupandishiwa ushuru ili mifuko ya ndani iten gezwe kwa kiwango ambacho tunakubaliana. Naomba sana Waziri wa Fedha aliangalie hili ili kuweza kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi viwanda vilivyopo nchini vinatosheleza na chenji inabaki kupeleka nchi jirani. Kwa hiyo, naomba sana wakati tunahitimisha tungeweka japo kodi yoyote kuipandishia hii mifuko ambayo inatoa nje.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni kwamba biashara baina ya Bara na Visiwani toka nimeingia Bunge hili ni miaka kumi sasa hivi na ninashukuru sana bajeti hii imewafikiria sana wafanyabiashara na wawekezaji kiujumla lakini kuna eneo moja ambalo imekuwa kama pua ya ng'ombe kutiririka mafua, nalo ni eneo la Begejirumu. Begejirimu pale inabidi lazima patazamwe vizuri sana kwa sababu ni eneo moja ambalo wanapita watalii wanaotembea baina ya nchi mbili hizi na wa nje.

Mheshimiwa Spika, anapokuja mtalii Bara au anapokuja mtalii Zanzibar akinunua kitu chochote, akifika Begejirumu pale kitu kidogo anaambiwa aanze kulipa ushuru anahangaishwa, wakati yule mtu alipoenda kununua dukani hajui mipango iliyokuwa pale kwamba inabidi awe na *custom entry* aoneshe mzigoto uliingia vipi. Yeye kanunua, kalipia.

Kwa hiyo, inatakiwa heshima ile apewe kwamba amenunua Tanzania. Kuna wajanja wafanyabiashara ambao wanavusha mizigo na wale watu wa Begejirumu wanawajua, wawashughulikie. Tunaharibu utalii wetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano hai. Kuna Mbunge mwenzangu amepita pale na *cookeranakuja* nalo Dodoma, kashalitumia, limezuiwa, anaambiwa lilipiwe ushuru. Mpaka akajitambulisha kwamba yeye ni Mbunge anaenda Dodoma

ndiyo kaachiwa. Sasa fikiria hilo ni *cookerla Mbunge ambalo lilihatumika*. Kwa hiyo, naomba sana hili litazamwe kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nampongeza sana Rais wetu kwa kazi kubwa aliyofanya wakati huu wa *Covid* na hasa kwa wafanyabiashara, ametusaidia sana. Kulikuwa na kauli awali ikitisema vyuma vimekaza, kuna mambo haya na yale, lakini sasa hivi Rais huyu Mwenyezi Mungu ambariki, kila akiendelea mbele mambo anayofanya ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo amelifanya kubwa ni kuhakikisha kwamba Tanzania haiingii katika *lockdown* na hili limetusaidia sisi wafanyabiashara kwa kiwango kikubwa sana. Kama ingelikuwa *lockdown* ile tumeingia, naaminini ingekuwa vita kubwa sana baina ya watu wenyenacho na wasiokuwanacho kwa sabbau hali ingekuwa mbaya kuliko hizo nchi ambazo tunaziona. Tumeona *South Africa* mpaka Marekani watu wameingia wamevunja *ma-shopping malls* na kuiba. Fikiria leo Tanzania tungekutana na hali kama ile. Kwa hilo, nampongeza sana, Mwenyezi Mungu ambariki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaona vyombo vyao nje tayari *WHO* na wengine wanassema kwamba hii *Corona* iko hivi na vile...

*(Hapa kengele ililiakuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Turkey.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakupongeza wewe, umechukua muda mwingi sana kutuleta humu ndani, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Serikali yote kwa ujumla, tumefanya kazi, hiki kipindi sasa hivi ndiyo tunamalizia. Tusameheane kwa kila kitu tulichofanyiana, kama kuna mtu tumemkosea au

ametukosea tunasameheana tunakwenda mbele kuhakikisha maisha yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Turky. Nimeshakutaja Mheshimiwa Vedasto Ngombale, utafatiati na Mheshimiwa Balozi Mohamed Adadi Rajabu na Mheshimiwa Vicky Kamata ajiandae.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nikupongeze wewe binafsi kwa kuniamini mimi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Usimamizi wa Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) kwa vipindi viwili mfulilizo. Nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakinlingine ni kwamba, nichukue nafasi pia kupongeza viongozi wa Chama Cha Wananchi (*CUF*) wakiongozwa na Profesa Ibrahim Haruna Lipumba kwa namna ambavyo wamenipa ushirikiano katika kipindi hiki cha miaka mitano. Pia, nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kwa kuniamini kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono pendekezo la kuiongezea pesa *TARURA*, pesa ziwe za kutosha kabisa. Hali ya barabara zetu sio nzuri, pendekezo la Kamati ya Bajeti la kuiongezea pesa *TARURA* nafikiri ni jambo jema. Tuna imani kwamba sasa pesa zile zikienda barabara zitaimarika na maendeleo yatapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie kuhusiana na kumpongeza Mheshimiwa Mpango kwa pendekezo lake la kupunguza tozo kwa leseni za kuuza samaki na mazao ya samaki nje. Ni jambo jema sana, nakupongeza sana Mheshimiwa Mpango, ni jambo jema. Kwa sisi ambao tunatoka maeneo ya pwani jambo hilo lilikuwa linatukera

sana. Sasa nafikiri kwa punguzo hili maana yake wafanyabiashara wamepata sasa fursa ya kusafirisha mazao haya ya bahari kwenda nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la fidia ya gesi. Katika bajeti ya 2019/2020 Wizara ilitenga bajeti ya fidia kwa miradi ya gesi, hasa ule mradi wa kilovoti 400 kutoka Somanga Fungu kuja Kinyerezi, Dar-es-Salaam. Katika hali ya kushangaza mpaka sasa ile fidia haijatoka, ndugu zangu wa pale Somanga Fungu hawalipwa zile pesa.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiri kwamba, fidia hii ingepewa kipaumbele kwasababu asilimia 56 ya umeme tunaotumia unategemea gesi, kwa hiyo watu waliojitoa kwa maeneo yao kwa ajili ya kupisha hii miradi wangepewa kipaumbele. Niombe sana hiyo pesa kama imetengwa mwaka huu walipwe wale wananchi wa Kilwa kwasababu wamekaa kwa miaka zaidi ya mitano hakuna kinachofanyika maeneo yale. Hawawezi kufanya shughuli za kulimwa, hawawezi kufanya chochote; Serikali iliangularie hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini jingine nzungumzie suala la minara ya simu. Kila mwaka Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imekuwa ikitenga ujenzi wa minara ya simu katika vijiji mbalimbali. Sasa kinachotokea ni kwamba, minara inayotengewa kampuni za Vodacom, Airtel, tiGO, Halotel inajengwa, lakini maeneo yanayotengwa kwaajili ya ujenzi wa minara ya *TTCL* utekelezaji huwa haufanyiki. Sasa ninapata shida tatizo liko wapi ilhali *TTCL* ni kampuni ya Serikali? Vijiji vyote viliviyotengewa *TTCL* hakuna utekelezaji wowote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mpango kama kuna shida ya upelekaji pesa huko basi uangalie hii kampuni ya kizalendo ili nayo ipate fedha ianze kufanya kazi ili Watanzania wafaidi matunda ya kuitumikia kampuni yao ya kizalendo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, llingine ambalo ningependa nilzungumzie leo ni suala la athari za corona na matokeo

yake. Kutokana na athari ya corona kuna mambo yalijitokeza; tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa msimamo wake, sasa ameanza kuruhusu baadhi ya mambo kufanyika ikiwepo pamoja na michezo, imeruhusiwa kufanyika. Sasa ningeomba kupata tamko la Serikali kuhusiana na shughuli nydingine za kijamii. Kwa mfano, sisi katika maeneo yetu kuna suala la misiba bado Serikali haijasema chochote, kuna suala la jando, unyago, tuna sherehe, tuna maharusi. Tupate tamko la Serikali, lakini kuna mikutano ya Serikali; tupate tamko la Serikali na utekelezaji wake unakuwaje ili basi wananchi wawe huru kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, lakini jingine mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Usimamizi wa Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*). Kumekuwa na changamoto kidogo kwenye utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani na wajibu wa Serikali za mitaa.

Mheshimiwa Spika, nikuombe, wakati zoezi la mfumo wa stakabadhi ghalani unatekelezwa wajibu wa Serikali za mitaa usinyang'anywe, Serikali za Mitaa zisimamie ukusanyaji; wa usinyang'anywe huu wajibu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** sasa kinachotokea kwamba, huu wajibu umenyang'anywa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu, atafuatiwa na Mheshimiwa Vicky Kamata, halafu Mheshimiwa Anatropia na Mheshimiwa Esther Matiko atafuatia.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia kwenye hoja hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana katika kipindi cha miaka mitano umeweza kuendesha Bunge hili kwa busara kubwa sana, na wananchi wa Muheza wamenituma nikwambie kwamba, watakuandikia barua rasmi ya kukushukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, kazi ambayo Mheshimiwa Rais amefanya katika kipindi cha miaka mitano ni kazi ambayo inatakiwa iheshimiwe sana. Kwasababu kwanza tumeprata maendeleo mengi ambayo hatukutaraja. Wakati natembea ukienda nje ukiangalia vitu ambavyo viko nje, ukiangalia ma-*bullet trains* ambayo yako nje, ukiangalia wenzetu ndege ambazo wanazo, ukiangalia *flyovers* ambazo ziko nje nilikuwa nafikiri ni lini Tanzania tutaweza kuwa na miradi kama hiyo. Sasahivi tumeanza kuwa na *SGR*, tumeanza kuwa na ma-*flyover*. Haya yote ni kwasababu ya Mheshimiwa Rais Magufuli. Kwa kweli kazi ambayo amefanya katika miaka mitano ni kazi ambayo ingeweza kufanyika katika miaka mingi ambayo inakuja. Amekuwa na uamuzi mgumu na kwa kweli, ameweza kututendea haki katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha kwa sababu, ameweza kuleta hela kwa wakati katika miradi mbalimbali. Pamoja na kuwa na miradi mikubwa, lakini miradi mingine ambayo sisi Wabunge tunatakiwa tuishughulikie kwenye majimbo yetu Wizara hii imeweza kuleta fedha kwa wakati na miradi hiyo imeanza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, Muheza wana-Muheza tulikuwa na tatizo kubwa na tuna tatizo kubwa sana la maji; lakini nafurahi kusema kwamba Mradi wa Pongwe ambaao hata Mheshimiwa Waziri Mkuu anaujua, Waziri wa Maji na Naibu wake wameushughulikia sana. Mradi huo sasahivi mafundi wanafanya *testing* na maji mpaka jana yamefika Lusanga, na tumeambiwa kwamba, maji mpaka jioni ya leo yataanza kufika Mjini Muheza. Kwa hiyo ni shukrani kubwa sana. Pia tunategemea mradi mkubwa ambaao unakuja wa wahindi kutoa maji kutoka Mto Pangani ambaao utachukua takriban kata 20 utawenza kupunguza tatizo la maji kwa kiwango kikubwa sana katika Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Spika, isitoshe, hivi ninavyozungumza sasahivi hospitali ya wilaya ambayo tulipewa hela na imeanza kujengwa, hospitali hiyo imeanza kufunguliwa, imefunguliwa Jumatatu na sasahivi inaanza kufanya kazi. Kituo cha Afya cha Mkuzi kinaanza kufanya kazi, tumeanza kujenga vituo vya afya kila tarafa zote nne; Tarafa ya Amani, Tarafa ya Gombwera, Tarafa ya Ngomeni na Tarafa ya Muheza zote ziko kwenye hali ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Barabara ya Amani pia wakandarasi wako kazini, Wachina wameshaanza kazi, barabara ya kilometra 40; na bajeti hii pia imeongeza fedha nyingine kwaajili ya kukamilisha barabara hiyo kukamilika. Sasahivi Muheza wameanza kujenga barabara za lami mjini; kilometra tatu ambazo Rais aliahidi zimeanza kujengwa na tunaanza kuona matunda yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, isitoshe sasahivi Muheza tumeanza kusafirisha viungo. Tumekuwa na kiwanda cha viungo kinapokea iliki, mdalasini, karafuu na pilipili manga. Kiwanda hicho ambacho kiko Lusanga sasahivi kimeanza kusafirisha *containers* kwenda Ulaya; na wameshasafirisha ma-*container* mawili, matatu yameshafika Hispania.

Mheshimiwa Spika, sasa haya yote ni maendeleo ambayo yapo. Tumeanza kujenga *high school* kwenye kila tarafa, tunayo *High School* ya Songa iko pale. Kwa hiyo haya mambo yote haya ni fedha ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais na Waziri wa Fedha. Namuona dada yangu Mheshimiwa Ummy tumepata *ambulance* ambayo imefika na ni mpya na ambayo tunaanza kuishughulikia kuanza kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, isitoshe kuhusiana na viwanda, kiwanda chetu cha chai cha *UTCO* tunategemea nacho kimeshaanza kupata kibali cha kuweza kujenga kiwanda na kuweza kufanya *packaging* na hivyo tutaondokana na urasimu wa kupeleka chai yetu kule Mombasa kwenye mnada. Sasa Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo tunategemea

kwamba wataanza kazi kwa ajili ya kuondoa hayo mambo ya mnadana kama ni mnada uanzishiwe hapahapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana bajeti hii, baada ya kuondoa tozo na ada nyingi takriban 60 imefanya maboresho mengi; kwa hiyo ni mambo ambayo itarahisisha sana. Ni mambo ambayo yamezungumzwa kwenye *blue print* na tunategemea kwamba itarahisisha sana kwenye suala la uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, na la mwisho ni suala la *TANAPA* ambalo uliulizungumzia juzi. Tunategemea watalii watakuja kwa wingi, lakini lile suala la *TRA* kuchukua zile fedha zote, labda suala hili Serikali ingejaribu kuliangalia tena ili basi, inaweza isichukue fedha zote, lakini iweze kuangalia namna gani inaweza kuwaachia *TANAPA* au Ngorongoro na *TAWA* illi waweze kuwahudumia watalii; tutakapochukua zote inaweza kudhoofisha. Inawezekana pakawa kuna uharibifu au fedha ambazo zilikuwa zinatumiwa vibaya pale *TANAPA* au Ngorongoro. Hivyo si busara kuchukua hela zote na kuacha wale watu kwasababu utalii tunautegemea sana kwa Pato la Taifa ambapo wanachangia takriban asilimia 17.5.

Mheshimiwa Spika, pia, tunapongeza mifumo ambayo imeanzishwa, hasa mfumo wa *TANePS*. Ni mfumo wa ununuzi ambao umeanzishwa sasahivi kwenye bajeti hii. Kwenye Kamati tumeujadili sana; ni mfumo ambao utasaidia, utaweka *transparency* kwenye mambo yote ya manunuzi hasa kwa watu wote ambao wata-*bid*, wenye *tenders*. Ni mfumo ambao unatakiwa kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na asante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Balozi kwa mchango wako. Mheshimiwa Vicky Kamata.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, udumu milele na ninawaomba wana Kongwa

wasituangushe maana tunakuhitaji na tunakupenda sana. Na mimi nakuahidi kwa jina la Yesu nitarudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena kwaajili ya kuchangia bajeti hii ya mwaka 2020 ambapo Bunge lako Tukufu litavunjwa baada ya siku mbili na kurudi kwa wananchi kuomba ridhaa yao, kama ikimpendeza Mungu basi tuendelee tena kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kwanza kwa kuunga hoja hii mkono kwa asilimia 100 bajeti hii ambayo kwa kweli, imesheheni neema teletele kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopita ya mwaka 2019 ilijikita zaidi katika kutekeleza, kuimarisha na kujenga miondombinu ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi. Umeme, barabara, maji, *SGR* na mambo engine mengi yaliangaliwa katika bajeti ya mwaka 2019. Bajeti hii ya mwaka 2020 ambayo tunaijadili hivi leo, yenyewe imejielekeza katika kulinda na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana. Inajenga mazingira bora kwa wananchi ili kuwapatia maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imeangalia viwango vya kodi kwa watumishi (*Pay As You Earn*) ili kuleta unafuu kwa watumishi. Hiki ni kitu kikubwa sana na ni cha muhimu. Imeangalia na kurekebisha kodi mbalimbali ili kuwawezesha wafanyabiashara waweze kunufaika na kazi na biashara wanazofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mithali 28:1 inasema; “Waouu hukimbia pasipo kufuatiwa na mtu, bali wenye haki ni majasiri kama simba.”

Mheshimiwa Spika, Rais wetu John Joseph Pombe Magufuli ni jasiri kama simba. Alipanga kuiongoza nchi hii na Mungu akaruhusu kwa kuwa ana makusudi mema na Taifa hili la Tanzania. Alipoingia madarakani Mheshimiwa JPM alitaka kuona analifufua shirika letu la ndege na kulipatia

ndege za kutosha. Alipoingia madarakani aliwahurumia Watanzania akasema niwapunguzie mzigo wa kutoa elimu bure ili kila mtoto apate elimu. Alipoingia madarakani aliamua kuanzisha *SGR*, na mambo mengine mengi ambayo siwezi kuyatamka kwa dakika hizi tano isipokuwa nitayaandika kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wengi walidhani kwamba haitawezekana, lakini nia njema ikiwepo, ukiwa na dhamira ya dhati hakuna jambo gumu lisilowezekana. JPM ameyafanya hayo yote na yamefanikiwa kwa sababu ya dhamira yake ya dhati pamoja na jitihada, yote haya yamewezekana, na hilo ni fundisho kwetu wote kwamba tuamini hakuna jambo gumu lisilowezekana kama nia njema ipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema JPM ni Jasiri kama simba hata tuone jinsi ambavyo ametuvusha katika hili janga la corona. Dunia nzima ilikuwa na hofu, vifo kila mahali, huku tukitabiriwa kwamba, tena kwa Afrika Tanzania ikiwemo, maiti za watu zitazagaa kila kona. Wengi mataifa yaliyoendelea yenye pesa, yenye vifaa tiba, yenye kila kitu yaliamua kujifungia ndani, waliona suluhu ni kujifungia ndani na *ku-sanitise*, basi; lakini sisi jasiri wetu huyu kama simba alisema hakuna kujifungia ndani.

Mheshimiwa Spika, sisi tumuombe Mungu, *tu-take precautions* kama kawaida, lakini tufunge siku tatu, tunaamini tukimwomba Mungu, Mungu wa kweli, atatuvusha salama tutapona tuendelee na kazi kama kawaida, lakini huku tukichukua tahadhari. Huyu jasiri kama simba mimi ninasema ni zawadi ambayo tumepewia Watanzania tunatakiwa tuheshimu na tumshukuru Mungu na tumwombee afya njema ili aendelee kutuvusha kama Nabii Musa alivyowavusha wana wa Israel kutoka Utumwani Misri...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, malizia dakika moja.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, nilitamani kuimba kwa sababu, hili ni Bunge langu la mwisho na katika miaka 10 sijawahi. Ninaomba dakika moja niimbe:-

*(Hapa Mhe. Vicky Paschal Kamata aliiimba wimbo uliomsifu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Joseph Magufuli)*

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. Ahsante sana, nawapenda wote. (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Mambo hayo! Ahsante sana Mheshimiwa Vicky Kamata kwa kulichangamsha Bunge hili. Hapa mwishoni hapa mambo mswano sana. Sasa mmecheka sana, nataka mchokozeko sasa, Mheshimiwa Anatropia. Hayupo niendelee? Mheshimiwa Esther Matiko halafu Mheshimiwa Meiseyeki. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; na mimi naomba kuweza kuchangia kwenye hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba Serikali hii iweze kuwalipa wananchi wa Bugosi na Kenyambi fidia ambayo imedumu kwa zaidi ya miaka 20. Nimezungumzia hili nikiwa Viti Maalum, lakini na nikiwa Mbunge. Na mwaka jana Mheshimiwa Anatropia aliposhika shilingi hapa Waziri wa Fedha aliahidi kwamba wanaenda kulipa fidia, mpaka sasahivi hajjalipwa. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi alisema ameshamaliza tatizo lipo Hazina. Tunaomba wananchi hawa waweze kulipwa ile fidia, ili waendelee na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, kingine; juzi niliona Rais anafungua Jengo la Zimamoto, zuri kabisa liliologharimu mabilioni ya hela; lakini tunavyozungumza kuna Wilaya hazina magari ya zimamoto. Kwa mfano Tarime juzi tumepoteza mtu na mke wake ambao ni walimu wa Shule ya Msingi Mapinduzi na Lemagwe kwa ajali ya moto. Moto umetokea, jengo limeteketea mpaka likawa *ashes*, hamna zimamoto. Sasa

tunaomba kabisa; na siku ile nilimuona Rais anatoa na bilioni tano sijui anazielekeza wapi; ningeshauri Kamishna wa Zimamoto aweze kuweka kipaumbele cha kuhakikisha kila wilaya inakuwa na gari la kisasa la kutosha kuweza kuzima moto kwenye majanga yanayotokea, vinginevyo tutaendelea kupoteza Watanzania kwa uzembe kabisa. Tuweke vipaumbele kwa kununua vitendea kazi ili tuweze kuokoa maisha ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kingine wote tunajua kuna adha ya sukari na Mheshimiwa Dkt. Mpango hili tunaomba utufanyie utatuzi kwa hili. Sisi tunaokaa mpakani upande wa Kenya kilo 50 ya sukari inauzwa shilingi 99,000 ambayo kwa wastani ni kama 1,800 lakini tunashindwa kuileta Tanzania kwasababu ukienda leo mpaka wa Sirari kuna mrundikano mkubwa wa malori yanashindwa kuja upande wa pili ambapo ukileta Tanzania sukari ni 1,860. Tanzania sasa hivi sukari ni 3,000 na haipatikani, wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata saruji, kule kwetu tunajengea saruji kutoka Bumbuli ambayo ni bei rahisi 16,000 ikija twiga *cement* ni 20,000 au 21,000 lakini wafanyabiashara wanashindwa kuvusha mizigo ile kuja Tanzania. Tunaomba sana Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango uweze kushughulikia. Hivi sasa ninyi mnaosema Serikali ya wanyonge, wale Watanzania wale waweze kupata zile bidhaa kwa bei ambayo ni *affordable*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kwenye utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, ni dhahiri kabisa kama Taifa Serikali imeshindwa kutekeleza Mpango wa Maendeleo, afadhali hata kwa Awamu ya Nne ilitekelezwa kwa asilimia 50 ule Mpango wa kwanza. Huu mpango wa sasa wa pili umeshindwa kabisa kutekelezeka kwa hata walau asilimia 30 na mifano ipo na ndiyo maana kama Kambi ya Upinzani tumekuwa tukishauri itungwe sheria ya kusimamia hii mipango ili iweze kutekelezeka vinginevyo tutakuwa tunapoteza hela na *resourceskwamba* kuna mipango ambayo haitekelezeki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mfano tu, kwenye Mpango wa Pili uliooelekeza kwamba tutaingia kwenye uchumi wa kati sasa sisi Wabunge ambao tunaenda kuhitimisha hili Bunge tujulize ni kweli tumeingia kwenye uchumi wa kati? Je, ni viashiria gani ambavyo vinatuonesha tumeingia kwenye uchumi wa kati kwasababu ukifanya *assessment* tu ya kawaida utaona sasa kwa sasahivi hata mzunguko wa fedha umekuwa ni wa shida sana kwenye watu wetu. Ajira ni za shida, wafanyabiashara vipato vyao vimeenda chini, wakulima vipato vyao vimeenda chini ya Tanzania zaidi ya asilimia 80, wakulima. Wafanyakazi ndiyo dhohofu kwasababu hamjawaongezea mishahara. Sasa hivyo vipato vyaa katii, mpango wetu tumeutekeleza vipi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye Sekta pia ya Maji na nisikitike pia baba yangu Waziri, unasema bayana kabisa kwamba eti maji tumepata kwa mijini asilimia 84, na kwa vijiji ni asilimia 71. Kwa hili sidhani kama utaliunga mkono maana hata wewe ulilalamika hapo kwa miaka mitano yote hii umepata kakijji sijui kamtaa kamoja. Tarime, nitapata ule mradi walau, mradi wa India lakini ukifanya *assessment* ya leo ambapo ameitoa *as of today* kwa Tarime, eti Tarime tu, Taime Mji tuna maji asilimia 84, ni kitu ambacho hakipo kabisa. Lakini hata kwa vijiji, kwa vijiji ninavyovijua, hakuna vijiji ambavyo vimepata maji kwa asilimia 70. Kwa hiyo, twende kwa uhalisia, tukisema asilimia 70 basi ionekane kweli watu wakitembea Tanzania nzima waweeze kuona asilimia 70. Mkoo wangu ninaotoka wa Mara, vijiji havina maji asilimia 70, miji haina maji asilimia 84.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Unapewa taarifa Mheshimiwa Esther.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana Mheshimiwa Mbunge lakini kikubwa pamoja na mahitaji makubwa sana ya maji lakini Seriakli imekuwa ikifanya jitihada kubwa sana. Mpaka sasa Wizara

yetu tumetekeleza miradi 2,450 kuanzia *WSDP 1*, Rais Dkt. John Pombe Magufuli, ametekeleza miradi 1,423. Lakini katika eneo lake tuna mradi wa Gamasala, tuna *project* ambayo sasa hivi tupo hatua ya kumpata mkandarasi katika eneo la Tarime lakini Mkoa wa Mara tumeshapeleka bilioni 8 zipo katika akaunti na kila halmashauri tumepeleka bilioni 1.3. Serikali ya Awamu hii ya Dkt. John Pombe Magufuli haichagui chama na tunayafanya haya kwa mustakabali wa maendeleo ya Watanzania. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba tu Mawaziri wawe wanasililiza tunavyoshauri, wamepeleka bilioni 10, bilioni 200 bado hujafikia *target* wanayoionesha ya asilimia 70 au asilimia 84, hilo ndilo tatizo! Upeleke trilioni moja lakini bado hujafikia *target* ambayo unalandika hapa kwa uhalisia, ndio hicho tu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Sekta ya Afya, mfano mwingineo, kwenye Sekta ya Afya walisema wangeweza kupunguza vifo vya mama na mtoto na mimi hili naliongea kwa uchungu kabisa kwa sababu mimi nami ni mhanga katika hili na nawakilisha akina mama wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati wanaingia madarakani walisema kulikuwa na vifo 432 kwa vizazi hai 100,000 na jana nimetaa hapa taarifa Mheshimiwa Waziri akanipa. Lakini 2017/2018 kulikuwa na vifo 556 kati ya vizazi hai 100,000. Kwa mujibu wa *National Bureau of Statistics*, lakini ukiendelea mwaka 2017/2018 vifo 524 kati ya vizazi hai 100,000. Mwaka 2018/2019...

**SPIKA:** Ahsante sana...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, dakika moja tu nimalizie hapo. Hili tu, muhimu sana. 2018/2019 vifo 578 kati ya vizazi hai 100,000 ongezeko zaidi. Sasa tunavyoshauri Serikali, wawekeze kuhakikisha kwamba wana-save maisha ya Watanzania. (*Makofii*)

**SPIKA:** Unapewa taarifa Mheshimiwa Esther. Mheshimiwa Waziri tafadhali!

## T A R I F A

### **WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE**

**NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Esther Matiko kwamba takwimu za vifo vya wanawake wajawazito vitokanavyo na uzazi takwimu rasmi ni za 2015/2016 za *National Bureau of Statistics* ambapo wameonesha vifo 554 katika kila vizazi hai 100,000 ambapo ni sawa na wanawake 11,000. Takwimu za mwaka huu za Wizara ya Afya ambazo zitakuwa *published*, vifo ni 3,000 tu! Vifo vya akinamama wajawazito ni 3,000 tu! (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

Mheshimiwa Spika, vifo ni 3,000 na ninyi wenyeWE Wabunge ni mashahidi. Vyumba vya kujifungulia vimejengwa, dawa zinapatikana, huduma za uzazi za dharura zinapatikana. Kwa hiyo, takwimu rasmi sio vifo 11,000 ni vifo 3,000. Tafuteni hoja nyininge. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Gibson Meiseyeki. Muda wako Mheshimiwa Esther umeisha.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Spika, naomba unitunzie muda wangu. Amemaliza dakika yangu moja.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha ambayo ananjaalia mpaka sasa na Baraka tele lakini pia kwa fursa hii tumuombe Mungu awapokee Mbinguni kwake na kuwapa msamaha wa dhambi zao wenzetu wote ambao wametangulia hususan binamu yangu Cuthbert Faustine na rafiki yangu mpendwa Bernard Lowassa. Nawakumbuka kwa fursa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimwashukuru pia Mawaziri wote wa mwanzo, katikati na wa sasa kwa jinsi ambavyo wamenisaidia katika utekelezaji wa majukumu yangu jimboni na zaidi sana naona Waziri Mkuu ametoka. Nilitaka kumshukuru kwa vivuko ambavyo aliviahidi Arumeru. Vingi vimeshatekelezwa na nichukue fursa hii kumkumbusha Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango kwamba kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais Jimboni kwangu hajakaa vizuri, kwa hiyo niombe mwaka huu waikumbuke iweze kutekelezwa kwasababu kwakweli wananchi wamechoka sasa na ahadi nyingi ambazo wanaahidiwa mara kwa mara na Marais na kwamba mpaka sasa hajatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hii ya juzi ya Mheshimiwa Magufuli wanaisubiria kwa hamu vinginevyo Oktoba yetu itakuwa ngumu kidogo kwakweli ni ile lami ya kilometra karibia 20 ambazo aliziahidi allipokuja Arumeru, wananchi wanaitaka sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe pia ukumbuke angalau kupunguza deni letu la halmashauri ya Arusha *DC* ambalo ni 1.9 billion ilikuwa fidia ya ardhi ile tunaihitaji sana kwa ajili ya kukarabati madarasa yetu na changamoto mbalimbali ambazo tunazo jimboni. Kwa hiyo, tunaomba ni muda mrefu sasa toka umetulipa sehemu yake lakini imebaki bilioni 1 na milioni 900 tunaomba uzikumbuke kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu barabara zetu ni mbaya sana na kwa kuwa mlizichukua ninyi kuzitengeneza kwa maana ya Serikali kuu basi tunaomba muisaidie *TARURA* ili itusaidie kuondokana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi zimeharibika kama ulivyosema kwenye hotuba yako, sisi wengine tunakaa kwenye ukanda wa milima, makorongo ni makubwa sana na *TARURA* haina uwezo kwa sasa kwa hiyo tunaomba uipe kipaumbele cha awali kabisa mara tunavyopitisha bajeti yako basi fedha ziende zikatengeneze barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, kuna viporo, Mheshimiwa Kalemani tunakushukuru pia kwa ushirikiano wako kwetu, vijiji vyangu karibia vyote vina umeme lakini kuna maeneo ambayo yalishaainishwa kupeleka umeme, wengine wamepata nguzo zimesimikwa lakini hakuna nyaya. Basi tunaomba kwamba viprovo hivyo mvimalize pia ili wananchi wafurahie zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa mwisho ni suala la *ATCL*, ni mdau wa utalii na mmojawapo ambaao ningependa sana kuona Shirika la Ndege linaimarika Tanzania. Lakini utaratibu unaotumika sidhani kama unakwenda kutusaidia sana. Tunahitaji huduma zaidi ndani ya nchi, Tanzania ikishafika saa mbili usiku, baadhi ya mikoa hakuna usafiri wa anga. Ningeomba kwamba tujikite zaidi kwenye kwenye kuimarisha hivi vindege vidogo vidogo hivi, Bombadier, hizi za watu 20, 25 na 30 ili unapokuwa Bukoba usiku saa mbili au saa tatu uwe na uhakika wa kuweza pia kufika Dar es Salaam. Unapokuwa Mbeya, Kigoma na maeneo mengine watalii wetu tunashindwa kuwasafirisha *within the country*, hawana shida ya kufika hapa pamoja na kwamba gharama ni kubwa sana kwa mashirika ya ndege yanayoleta watalii Tanzania ukitofautisha na uwanja wa nchi za jirani hapa ambazo unaona kwamba watalii wanakwenda kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, *you can imagine* kuna tofauti ya karibia dola 200 kutoka London mpaka Nairobi na kutoka London mpaka Dar es Salaam. Sasa hizo hela ni nyingi sana. Tuangalie kwa namna gani tunaweza kuwarahisishia wapate ule unafuu, kama ni *handling fees* ambazo tunachaji makampuni ya ndege, tuangalie tupunguze ili kuongeza utalii. Mheshimiwa Kigwangalla hatutaweza kuongeza utalii kwa namna hii ambapo kila kitu ni ghali Tanzania. Na sasa hivi ambapo tuna corona tuangalie jinsi ya ku-*harmonize fees*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninyi mmesoma biashara, wanasema unapokuwa hauuzi, unatakiwa upunguze bei ili kuvutia soko. Sasa tumebakni *rates* zile zile kila mahali, kodi zetu zile zile, hakika itatuchukua muda mrefu sana ku-*recover*

kwenye *industry* ya utalii na ni mdau wa utalii kwa miaka mingi, hali sio shwari. Kule tumefunga kila kitu, magari yamepaki, *camps* tumezingunga, hakuna. Vijana wengi na akinamama ambao wanauza bidhaa mbalimbali kwa watalii wanapata shida. Kwa hiyo, katika *initiatives* za awali ni pamoja na ku-*adjust* bei zetu ili ngalau ku-*promote* au kuvutia watalii kuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru...

**SPIKA:** Ahsante sana, malizia.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Spika, shukrani zangu ni kwa miradi ya maji Jimboni kwangu, nikuombe tu Waziri wa Maji pamoja na Mheshimiwa Aweso basi ile miradi ambayo bado haijakamilika tuongeze nguvu ili by October wakati tunakwenda kwenye *judgment* tuwe angalau wananchi wanakunywa kunya maji tunaweza tukapata ahueni sisi wote.

Mheshimiwa Spika, *otherwise*, niseme kwa wale ambao kwa bahati mbaya ama vyovyote watashindwa kurudi hapa Novemba, mnapokuja Arusha tutakuwepo, tutawakaribisha, tunawapenda karibuni sana Arusha baada ya Bunge hili. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa uungwana wako. Mheshimiwa Wilfred Lwakatare atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi nzuri uliyonipa kwanza nikushukuru wewe binafsi natambua nimo ndani ya Bunge kwa uhimili wako nakushukuru sana. Lakini la pili niwashukuru wananchi wangu wa Bukoba, tarehe 5 walinifuta machozi sana, nawashukuru sana kwamba kweli wananipenda, wananiithamini na wameweza kuyatafsiri yale yote yaliyotokea katika mtazamo chanya kwamba kijana wao kwa kweli bado yuko *clean*, yuko vizuri na wanampenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba haya yote yaliyotokea na ninyooshe lugha sawasawa kwasababu watu wengi ambao hasa wanajimbo walifikiri niliondoka kwenye chama changu cha zamani, sikuondoka kwenye chama cha zamani, nilifikuzwa, kwa hiyo, inabidi wafahamu hilo na haya yote yanayotokea ni sawa na kuangusha mbuyu, mbuyu ukiuangusha matokeo yake kama kuna nyumba chini na migomba n.k inakwenda.

Mheshimiwa Spika, nikishukuru Chama Cha *CUF* ambacho kimeonesha dalili ya kunikubali. Walinikaribisha nikawatembelea, yaani nikaonekana kabisa nimerudi nyumbani, *CUF* wamenisaidia kustaafu nikiwa na *number plate*. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii bajeti tunayoizungumzia kwa namna moja ama nyingine inatugusa wananchi wa Kagera, wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini, nayazungumza haya, shemeji yangu Naibu Waziri ananielewa, Mkoa wa Kagera ni mkoa ambao umepambana na mambo mengi makubwa japo watu wakati mwingine wanayatumia kama utani lakini pale palianzia UKIMWI, vita vya Kagera vimepita pale, tetemeko limekumba Mkoa wetu, mafuriko yameukumba Mji wa Bukoba, kwa namna fupi tu ninachowenza kuzungumzia Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wako, Mkoa wa Kagera unahitaji *Martial plan*, unahitaji ukarabati uliojipanga sawasawa kupitia katika bajeti ambayo inapitishwa. Tunashukuru, iko miradi ambayo imo na itatengewa fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini Mkoa wa Kagera naamimi kabisa kabisa katika *vision* aliyonayo Mkuu wa Mkoa, bwana Kaguti pamoja na wasaidizi wake hasa Prof. Kamuzora kwenye mkakati ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu nae alihudhuria pale ambao unaitwa Kagera *Region Investment Guide* ambayo Mheshimiwa Waziri kupitia hapa nitakukabidhi hiki kitabu na hata nitakupa *brochures* zetu.

Mheshimiwa Spika, *vision* ya Mkuu wa Mkoa, wataalam wake na wannachi wa Bukoba tunaamini

ikitekelezwa kwa asilimia japo hata 70 Mkoa wa Kagera utaweza kutoka katika ile hali ambayo huwa tunaambibiwa sisi tumo mionganii mwa mikoa maskini.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera hauna sababu ya kuwa maskini, kama umewahi kwenda nchi ya Switzerland, ndio sawa na Mkoa wa Kagera, ni evergreen, una maji tele, unapakana na nchi nne, kuna nchi mbili ambazo... sasa kama Arusha na Kilimanjaro na Tanga ni kanchi kamoja wanakopakana nako kwanini Kagera ni maskini inapakana na nchi nne au tano? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo umaskini ulioko kule haujawa *addressed* katika hali ambayo inatakiwa na narudia tena, *guidance* hii ambayo imetengenezwa na wataalam naamini inaweza ikaukwamua Mkoa wetu wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumze kitu kimoja, nastaaifu, kama nilivyoeleza ndani ya Bunge hili nakwenda Bukoba, nitakaa Bukoba na Bukoba wameonesha nitakaa nao vizuri tu na kitu ambacho natarajia kufanya kila mwaka nilikuwa naendesha kitu kinaitwa *BUMDEKO* (*Bukoba Municipal Development Conference*) nilikuwa mwezi wa 12 nawakutanisha watu walioko ughaibuni wa Kagera, watu ambaao wako mikoa mbalimbali wanakuja December, kule tunakutana, tunajadili maendeleo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Profesa Tibaijuka, namshukuru Mheshimiwa Rweikiza, namhsukuru Mheshimiwa Mwijage na Wabunge wengine wote wamekuwa wanahudhuria bila kujali itikadi za kivyama. Kwa hiyo, hiki kitu nitakiendeze na kitaendelea kuwepo na watu walioko ughaibuni wamesema watakiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, kwa sababu ya muda jamani dakika tano tano. Atafuatiwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nitaongea mambo machache, La kwanza tokea jana au toka Bunge hili lianze ninasikitika sana ama ninashangazwa sana jinsi Wabunge wa chama tawala mnavyotoka mapovu kueleza namna gani mmetekeleza llani. Kuna msemo wa Kiswahili unasema; Chema chajiuza, kibaya chajitembeza. Hivi ninyi kama ni wema, kama mmeefanya mazuri kama mnavyosema, mnahitaji kutoa mapovu kiwango hicho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaenda kwa *data*, hatuendi kwa porojo, tunajadili mafanikio ama utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano kwa tawimu! Sio kwa ninyi kuwaambia eti kwenye halmashauri yangu nimejenga choo, ama nimejenga zahanati, hapana!

Tulisema jana kama mmesema uchumi umekua kama Mheshimiwa Mpango alivyosema, kama wameshindwa kutimiza *performance* ni zero. Kama wameshindwa kupunguza kiwango cha umaskini, *performance* ni zero... (*Makofi*)

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima kuna taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza kwamba, sisi hatujatokwa na mapovu, mtu anayetokwa mapovu ni yule aliyekunyuwa sumu anataka kufa au yule mtu aliyelewa chakali. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Taarifa yako Mheshimiwa Halima hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, najua walisema Rais Magufuli anawaangalia kwenye TV, kwa hiyo hapa wanampamba ili awafikirie kwenye ufalme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Mpango ndiyo mafanikio ya llani ya CCM, jana tumeorodhesha Wizara nne

muhimu; Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, Wizara ya Viwanda na Biashara, *performance* ya kibajeti inatuonesha kwamba Wizara hizi muhimu zina-*perform* kati ya asilimia 0 na 30 kwenye miradi ya maendeleo. Sasa...

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEN M. BASHE):**  
Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa dada yangu...

**SPIKA:** Kuna taarifa unapewa. Mheshimiwa Naibu Waziri Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**  
Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa dada yangu, nimeisoma hotuba yake ya jana na hasa *component* ya kuhusu kilimo. Kwanza nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba unapotazama Sekta ya Kilimo ni *crosscutting sector*. Sekta ya Kilimo kuna *component* ya nutrition ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya, *is allocated with funds*, kuna *Local Government component* ni *allocation* ya resources. Kwa hiyo, unapotazama Sekta ya Kilimo, unaitazama kwa ujumla wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili; Sekta ya Kilimo ni *one hundred percent private sector* naomba nilitaarifu Bunge lako... (*Makofii*)

**SPIKA:** Na hii *point* naomba uirudie tena, watu wengi hawaelewi hiki kitu. Sekta ya Kilimo ni *private* kwa asilimia kubwa sana.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (NAIBU WAZIRI WA KILIMO):**  
Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ni *one hundred percent private sector*. Jukumu la Serikali ni ku-*invest* kwenye maeneo ambayo *private sector* haiwezi kupeleka fedha. Naomba nilipe takwimu Bunge lako kwamba kati ya mwaka 2015 mpaka 2019 Sekta Binafsi imewekeza trilioni 4.7 katika Sekta ya Kilimo ambayo ni wastani wa trilioni moja kwa kila mwaka. Sekta ya Kilimo *development partners* na hii ni miradi ambayo tunaiita *off budget*, tumewekeza shilingi trilioni 3.8 wastani wa bilioni 800 kila mwaka. Kwa hiyo, ni vizuri tunapojadili Sekta

ya Kilimo tuijadili both from the Government Sector na from the Private Sector kuitazama bajeti yake. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima taarifa kwako hiyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tunatenga bajeti ili Serikali itengeneze mazingira wezeshi ili *Private Sector* iweze kuja kuwekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo...

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Spika, naomba...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Bashe namheshimu; mimi hapa nina taarifa ya ukaguzi maalum uliofanywa na *CAG*; kaguzi saba za kilimo anasema; mpaka mwaka 2018 Serikali ya CCM kuitia Wizara yako ilikuwa haijui mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo. Mnafanya kwa makisio, taarifa ya *CAG* miaka 59 ya Uhuru mnambwelambwela hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anasema hizi bajeti za maendeleo, hizi *project* za umwagiliaji hizi na maendeleo asilimia 90 mnategemea mabeberu, maendeleo, *CAG* nitakupa ripoti. Anasema....

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Msichokoze moto nilikuwa sina hata mpango wa kuyazungumza haya... (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Halima, umechokoza mwenyewe, kwa hiyo pokea taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na mchango wa Mheshimiwa Mbunge nataka kuongezea alipoishia Mheshimiwa Bashe kwamba Sekta ya Kilimo kwamba ni Sekta Binafsi na kuna hela nydingi tunapeleka kama Serikali nje ya bajeti. Nataka nimpe mfano mmoja tu, sasa hivi tunatekeleza mradi wa *TANPACK* zaidi ya dola milioni 35.5, tumeanza tangu mwaka 2018, mradi huu wa miaka mitano na hela zipo tayari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili, tumemaliza juzi tu Dakawa, tumewekeza kwenye mradi ule wa umwagiliaji zaidi ya bilioni 21. Pia kwenye miradi yote ya umwagiliaji *ERPP* tumewekeza zaidi ya dola milioni 16,500,000, zaidi ya bilioni 33. Pia tunajenga vihenge vyahisya maghala kuwezesha Sekta Binafsi kuhifadhi na maghala zaidi ya bilioni 56. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana. Mheshimiwa Halima pokea taarifa hii.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tunajadili bajeti na mipango tuliojiwekea, fedha za bajeti; sasa kama kuna watu wana pesa nje ya bajeti, mnatuambia kumbe kuna pesa zetu mnazipiga ama mnazitumia nje kinyume na utaratibu. Kwa sababu maana ya uwepo wa Bunge ni kuitisha mipango, bajeti na kutekeleza; sasa tunaanza kujua ni kwa namna gani mnafanya matumizi ya fedha kinyume na utaratibu na mnakiri wenyewe. (*Makofii*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Hivi Katibu huu muda wa dakika tano mbona? Taarifa anapokea taarifa, iko wapi taarifa aah, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumpa taarifa Mheshimiwa Halima Mdee kwamba anavyozungumzia bajeti ya maendeleo, kwa mfano kwenye upande wa kujenga uchumi wa viwanda

hatuzungumzii kujenga uchumi wa kisekta. Yaani ukitazama Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ukasema hiyo ndiyo fedha ya kujenga uchumi wa viwanda unakuwa unafikiria *in a narrow way*. Tunajenga uchumi wa kitaifa wa viwanda, kwa hiyo, bajeti yote ya Serikali inaenda kujenga uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, ningependa nimpe taarifa hiyo Mheshimiwa Halima Mdee. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hujaipokea taarifa, napata picha kwa nini Dkt. Ashatu siku moja alisema anataka aje atoe *tuition* ya namna ya kuchambua haya mambo, naona watu wanapata tabu kuchambua mipango, bajeti na uhusiano wake. Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kama mnatuambia haya mambo ni *crosscutting*, nitakupa mfano mmoja, viwanda mmeputa asilimia 20, *crosscutting right?* Kilimo mmeputa asilimia 17, maji mmeputa asilimia 30, *right?* Afya mmeputa... sikiliza kwa sababu fedha ambayo mnasema zinachomekwa huku na huku zina uhusiano, kama wewe hujapata, yule na huyu hamjapata zipo wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naanza kugundua kwa nini kila mmoja akisimama anasema Magufuli uwe Rais wa milele, inawezekana *span of thinking* na hawa jamaa ni ma... (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima muda umeisha. Mheshimiwa Nsanzugwanko. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Halima anapiga chini ya mkanda huyu. Mheshimiwa Nsanzugwanko tafadhalii. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naomba unipe dakika moja usiihesabu kwenye dakika zangu tano niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika utamaduni wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola siku zote wala siyo hapa tu, Wapinzani siku zote hawawezi kuona jema la Serikali iliyopo madarakani; hiyo ndiyo *tradition*, hawana macho ya kuona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa sisi wenye Serikali kwa maana ya chama chetu tunaangalia maendeleo ya nchi hii katika picha pana zaidi, siyo *narrow* kwa sekta moja moja; tunatazama *the bigger picture of the development of the country*, ndiyo msingi siyo kuangalia sekta moja moja mara mbolea, mbegu, hapana tunaangalia picha pana ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sasa nina hakika hiyo dakika moja hutaihesabu, naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii, Mheshimiwa Dkt. Mpango kusema kweli hotuba yake ametoa tarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2015 mpaka 2020, hongera sana. Amefanya uchaguzi mkubwa na Naibu wake na timu yao wamefanya kazi nzuri sana. Nchi inaendelea vizuri, wenye akili tunaona, mabadiliko tunayaona, wala huhitaji darubini kuona maendeleo haya wala huhitaji kusifiwa, sisi wenyewe tunaona maendeleo yetu na nchi hii inabadilika na wala siyo jambo la siri, Mheshimiwa Rais Magufuli amekuwa ni rubani mzuri sana wa maendeleo ya Taifa letu; Mheshimiwa Rais Magufuli hongera kwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa sababu Ilani ni ya CCM, naomba kupitia Wabunge wenzangu wa CCM tukipe hongera chama chetu kwa kzi nzuri ya kusimamia utekelezaji wa Ilani. Sisi wana CCM na Watanzania wengi wenye akili, mafanikio na utekelezaji wa Ilani tumetekeleza kwa asilimia 82.3, hizo ndizo takwimu tulizonazo; kazi ni nzuri, kazi ni kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo, nizungumze mambo mawili tu. La kwanza, Mheshimiwa Waziri Mpango nimefurahishwa sana ukurasa wa 62 wa bajeti yake;

amezungumzia habari ya Sera ya Matumizi ya Fedha za Serikali. Katika maeneo yale, ameainisha kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inakamilika kabla ya miradi mipya kuanza, hiyo kwa msisitizo kabisa Mheshimiwa Waziri hilo akalisimamie vizuri. Kuna maeneo katika nchi yetu anajua *central corridor* miradi imeanza haijakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anajua sisi Kigoma na Katavi bado hatujaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na mpango upo na ni matumaini yetu kupitia bajeti hii pamoja na shida ya *corona* bado miradi yetu hii sasa itakamilika. Naomba ajikite kwenye matumizi ya kibajeti ili mikoa hii miwili nayo ifunguke kama ilivyo mikoa mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kwa wananchi wa Kasulu Mjini ambako mimi ni Mbunge wao. Kwa niaba ya wananchi wote wa Kasulu Mjini, tunasema asante sana kwa CCM na Rais Magufuli tumefanya kazi nzuri na kubwa. Kule wananchi wa Kasulu wana akili, macho na wanaona; Halmashauri yetu ya Kasulu peke yake kwa miaka hii mitano fedha zetu za maendeleo tumepata toka Serikalini zaidi ya shilingi bilioni 19 za maendeleo. Ni kazi kubwa imefanyika na tunashukuru sana, tunashukuru Serikali, Rais Magufuli na CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nипитie kwenye miradi michache ambayo tumeitekeleza kule ili wananchi wa Kasulu na hata wale wanaofikiria eti kuja kugombeagombea kule wajue kwamba kuna kazi kubwa imefanyika. Nianze na Sekta ya Maji, Sekta ya Maji kule Kata ya Ilujuu tumepokea milioni 60, mradi wa maji umekamilika mambo yanaendelea. Huko Kata ya Muhunga tumepokea milioni 800, maji yanatoka na mradi unaendelea; huko Kimobwa awamu ya kwanza na ya pili tumepokea shilingi milioni 600 na kazi inaendelea, Kabanga mradi wa maji unaendelea, Kata ya Malumba... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko hebu nakuongeza dakika moja ile ya mwanzo ili wale wenye nia waweze kusikia vizuri. (*Kicheko*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, kuna watu wanapitapita kule Kasulu baada ya kuona Kasulu imependeza, ina umeme na barabara za lami zinajengwa, sasa wanapitapita. Sasa eti wameipenda Kasulu baada ya kuwa imeanza kupendeza, tunawaambia hiyo biashara hatufanyi. wananchi wa Kasulu kuna kazi tumeanza nazo tunataka tuzikamilishe tukiwa na Rais Magufuli. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nsanzugwanko muda...

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, bado moja, dakika moja...

**SPIKA:** Nakushukuru sana.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Sekta ya Elimu kidogo, dakika moja tu nizungumzie miradi ya elimu. Kule Kasulu kuna miradi mingi ambayo tumepata kwa halmashauri na mingine ni mtambuka, hoja yangu ni hivi miradi hiyo imeletwa na Serikali na siyo familia ya mtu mmoja. Nilitaka hilo nilliweke sawa kwa sababu kuna udanganyifu na uongo mwingi kwamba eti mtu analeta miradi, hao wanaokuja kugombea tunawakaribisha waje... (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko ahsante sana kwa sababu ya muda, nakushukuru sana. (*Kicheko*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, asante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana muda haupo upande wako, ila Mheshimiwa Nsanzugwanko kuna taarifa kutoka kwa Profesa Ndlichako. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Bonaventura Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mama Sitta na Mheshimiwa Silinde ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini huku ukijiandaa kunipa dakika tano nyingine. Napenda kumshukuru sana Mungu kwa namna ya pekee ambavyo anatuwezesha siku zote kufanya kazi yake ambayo wananchi wametupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea mimi nilikuwa naomba tu kama inawezekana Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi wewe pamoja na Waziri Mkuu mpite bila kupingwa kwenye chama chetu kwa sababu mmefanya kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri mambo mawili kwenye kodi; kuna kodi ya mabango kwenye magari ambayo yanatembeza bidhaa. Mabango haya ni kichocheo cha biashara, inapochochewa biashara mauzo yanakua, yanapokua mauzo kodi ya Serikali inakua; hatuna sababu ya kutoza mabango ambayo yanachochea biashara kukua. Hili niishauri Serikali hata kama siyo mwaka huu, ikiwezekana tulete sheria ya kufuta kodi ya mabango kwa sababu ni kichocheo cha biashara, kodi ya Serikali inakua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina ushauri wa kodi ya huduma (*service levy*). *Service levy* ni kodi ambayo inatozwa kutohana na mapato yote bila kuzingatia faida wala hasara. Kodi hii inakwenda kudhoofisha mapato ya *corporate tax* kwa sababu inalipwa kabla ya kutoa gharama. Kwa hiyo kodi hii Waziri wa Fedha aiangalie inakwenda kupunguza mapato ya *corporate tax* kwa mwaka. Ni kodi ambayo kimsingi lazima uangalie mapato na matumizi ndipo uitoze lakini sheria yake haikukaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, nilisimama hapa Jimbo la Magu nikasema kama hamtapelekea maji sitarudi Bungeni; maji Magu sasa ni masaa 24. Akinamama walikuwa wanaamka usiku saa

nane hata akinababa mambo ya ndoa yalikuwa yaimesha, sasa Mheshimiwa Dkt. John Magufuli ameyarudisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ambayo yamefanyika kwa Wilaya yetu ya Magu na kama Jimbo siwezi kuyataja yote kwa sababu wananchi wenyewe ni mashahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kimsingi sijawahi kusikia kiongozi ye yeyote duniani anasema yeye ni sadaka ya wananchi wake, nimemsikia pekee Mheshimiwa Rais akisema yeye ni sadaka ya Watanzania. Natafakari sana kwamba kiongozi anaamua kujitoa sadaka kwa wananchi wake ni kiongozi wa aina yake na hii pekee ndiyo zawadi ambayo Mwenyezi Mungu ametupa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mambo haya ambayo yamefanyika, tunayo kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais mimi nafikiria ni mbegu tofauti, tuna mbegu nyngi duniani na mbegu za binadamu. Hii ya Dkt. John Pombe Magufuli ni mbegu tofauti na mbegu za aina hii duniani zimebaki chache sana, lazima tuilinde na tuitunze kwa sababu haya mambo hayafanyiki kirahisi duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipotuambia Watanzania kwamba tumwabudu Mungu, tumwombe Mungu kwa sababu ya *Corona* na matokeo yake tumeyaona. Mungu hawezi kumdhailisha Mheshimiwa Rais. Sisi sote Watanzania tutatokea kwenye tundu la Mheshimiwa Rais kwa sababu Yesu Kristo alipokuwa anapigwa msalabani alidhihakiwa sana Mungu. Kwa hiyo, Mungu hawezi kurudia kosa hilo. Kwa hiyo, Watanzania kwa sababu tumemtegemea Mungu kupitia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Mungu hawezi kutuacha, *Corona* itaisha.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingi iliyokuwa imeshindikana hapa. Tunapozungumzia reli ya *Standard Gauge* ni miradi iliyokuwa imeshindikana, tunapozungumzia watumishi hewa hilo jambo lilikuwa limeshindikana,

tunapozungumzia *Stiegler's Gorge* ni miradi iliyokuwa imeshindikana, tunapozungumzia Vituo vya Afya kila Kata, miradi hii ilikuwa imeshindikana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ametuonyesha kwamba Tanzania tunaweza. Kwa sababu ametupa uzoefu huo, naamini kwamba Bunge lilajo tunapopitisha bajeti lazima tujikite tuhakikishe kwamba miradi yote ambayo imewekwa imetekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kila jambo lina wakati wake. Jambo hili ni wakati wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURE D. KISWAGA:** Ahsante sana, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante, ubarikiwe sana. Nishakutaja Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, utafuatiwa na Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Bunge letu hili tunapomaliza muda wetu. Pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuendelea kutumikia wananchi wa Urambo kwa kipindi chote tangu mwaka 2015 na wamenipa ushirikiano mkubwa sana wananchi wa Urambo, naomba waendelee kunipa ushirikiano ili tuendeleze maendeleo ambayo tayari yameshapatikana.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jinsi ambavyo imefanya kazi inayoonekana. Unajua kuna vitu vingine kweli tunaweza kuongea humu ndani ya Bunge lakini ukweli bado uko pale pale; Serikali ya Awamu ya Tano imefanyakazi kubwa sana.

Ushahidi mmojawapo, njooni Urambo mwone, kuna mambo mengi ambayo tumeyapata, tunajivunia kwamba tumeendelea na tumesaidiwa sana katika kipindi cha Awamu hii ya Tano ya uongozi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuishukuru Serikali. Nilipoingia Bungeni mwaka 2015 nilisema Urambo ina changamoto nydingi sana; lakini mbili ambazo zilikuwa kubwa ilikuwa ni uhaba wa maji. Naishukuru Serikali, tayari imeshatuingiza katika mpango wa kupata maji kutoka *Lake Victoria* na Mheshimiwa Waziri mhusika amenihakikisha kwamba Urambo ipo, itapata maji kutoka *Lake Victoria*. Nashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ilikuwa ni zao letu la tumbaku. Mkoa wa Tabora Urambo ikiwemo tunategemea sana zao la tumbaku. Naishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali ambayo imechukua, lakini kwa siku ya leo nilitaka nimalizie kuchangia kwa kutoa ushauri wangu wa jinsi gani ambavyo wanawenza kutusaidia sisi wakulima wa tumbaku Urambo tukafaidika na zao hili.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kwanza ni kwamba katika zao lolote lile wanadolima wananchi, kitu kikubwa ni masoko. Tunajua Serikali imetafuta masoko, lakini bado kuna haja ya kuwa na masoko zaidi. Kwa hiyo, nashauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Soko la Misri limepatikana. Naishauri Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Mambo ya Nje washirikiane kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunaingizwa katika soko la Misri kwa sababu wako tayari kuja kununua tumbaku nchini mwetu na Urambo ikiwemo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili, pamoja na kwamba tunategemea masomo kutoka nje, naishukuru Serikali kwamba sasa hivi imewatia moyo wanunuzi wa ndani; makampuni ya ndani. Naishauri Serikali iyasaidie makampuni ya ndani ili yasaidiane na yale yanayotoka nje ili tusikae

asilimia mia tunategemea makampuni ya nje, Serikali isaidie wanunuzi wa ndani yaani makampuni ya ndani iwawezeshe kwa kuwapa mikopo kuitia mabenki na kadhalika waweze nao kununua zao la tumbaku badala ya kusubiri makampuni ya nje tu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa tatu ni kwamba tumeshuhudia katika Awamu hii ya Tano jinsi zao la korosho liliyoshughulikiwa. Kwa hiyo, nami natoa wito kwa Serikali na kuishauri kwamba itumie utaratibu uliofanyika katika zao la korosho kwa kuwa na ushindani wa wazi; wanunuzi washindane, bei halali ipatikane ambayo itainua maisha ya wakulima kama walivyofanya korosho. Naipongeza sana Serikali kwa utaratibu iliyotumia kwa upande wa zao la korosho, nasi kwetu tumbaku ifanyiwe utaratibu huo huo ili wakulima nao wanufaikie na zao lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Serikali kwa kuja na *TARURA*, kwa kweli hata nasi Urambo tumesaidiwa na *TARURA* kupata barabara nzuri, lakini natoa wito kwa Serikali ikubaliane na mapendekezo ya Kamati ya Fedha ambayo ilipendekeza kwamba Serikali itoe shilingi billioni 132 kusaidia *TARURA* irekebishe barabara ambazo zimeharibowi sana na mvua ili wakulima waweze kupeleka mazao yao wanakotaka kwenda kuuza.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe. Kazi hii umeitendea haki, hongera sana. Pia tunasema kwa niaba ya *TWPG*, umefanyakazi kwa karibu sana na Umoja wa Akinamama; Umoja wa Wabunge Wanawake, umeshirikiana nao sana mpaka hapa ambapo tunafikia kesho tunakwenda kuangalia na kuzindua au kuweka jiwe la msingi katika shule yetu ya *Bunge Girls High School* au Shule ya Wasichana ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge; kwanza nawashukuru sana kwa ushirikiano wetu tulivyochangisha fedha kwa pamoja tukacheza. Nitafurahi

sana kama kesho pia tutakwenda kufurahi na kucheza kwa kuona matunda ambayo tuliya fanyia kazi wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wa kiume, mmetuunga mkono sana, tunaomba kesho mkiimba pamoja nasi itapendeza sana. Waheshimiwa Wabunge akinamama, sisi ndio wenyewe tena, tukiungwa mkono itakuwa vizuri sana; twende tukacheze, tukafurahie matunda ya kazi yetu kama *TWPG* amba tulikaa hapa kutetea masuala ya kijinsia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nakuheshimu na ninakushukuru kwa niaba ya *TWPG*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Sitta. Nilishakutaja Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia bajeti ya nchi yetu ya mwaka 2020/2021. Kabla sijaanza kuchangia, nilipokuwa namsikia Waziri Dkt. Mpango akiwasilisha Hotuba yake hapa Bungeni, ilibidi nami niende nikaangalia baadhi ya historia ya nchi ambazo uchumi wake unakua, ni namna gani walifanya kuhakikisha uchumi wao unakwenda ambapo sisi tulikuwa tunafanana nazo miaka ya 1950 na miaka ya 1980.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikaangalia China ya mwaka 1950 uchumi wa China ulikuwa unafanana na Tanzania. Ni kwa nini China ya leo iko tofauti na Tanzania. Nikaangalia Malaysia na Tanzania ambayo miaka ya 1980 uchumi wake ulikuwa sawa sawa na Tanzania. Ni kwa nini leo Malaysia wametuacha kwa mbali? Nikaangalia uchumi wa Singapore, Indonesia pamoja na uchumi wa India ambapo katika miaka ya 1980 zilikuwa sawa sawa na Tanzania. Hizi nchi zinaitwa *Tiger Economy*.

Mheshimiwa Spika, jambo pekee ambalo nililiona pale ni uthubutu wa viongozi wa wakati huo, ndiyo wallobadilisha nchi zao. Kwa hiyo, ukiangalia Malaysia, leo wote tumekwenda kule kujifunza, alikuwa ni Mahatir Mohamed. Kwa nini ni mtu mmoja? Mabadiliko ya kiuchumi yanaanza na mtu mmoja, sisi wengine tunatafsiri maono. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeamua kuyasema haya kwa sababu moja. Ninachokiona, watu wengi wanashindwa kutafsiri maono ya Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli kuhakikisha yanatupeleka mbele, walau na sisi tuweze kuonekana huko mbele kama ambavyo wenzetu Malaysia, Singapore na Indonesia tulikuwa nao sawa kiuchumi. Kwa hiyo, mtu yejote anayeshindwa kujua uthubutu, uamuzi wa kufanya maamuzi sahihi kwa Taifa lake, hawezi kuelewa. Ndiyo maana hapa kuna mjadala ilitokea kwa kifupi hapa, Mheshimiwa Halima Mdee mchangiaji aliyetangulia alikuwa anajaribu kutafsiri takwimu.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tuliosomea haya mambo, kwa wachumi kuna tafsiri mbili tofauti. Kuna *direct interpretation* na *indirect interpretation*. Sasa mtu ambaye hajasomea hayo mambo anakwenda kwenye *direct interpretation* kwa kuangalia takwimu. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, ngoja nieleze. Jambo kama hili la kilimo unaweza ukasema tu kwamba walipeleka fedha kiasi kadhaa asilimia 17, asilimia 18, ndiyo maana kilimo hakijakua. Wakati huo huo unasahau kilimo ndicho kinaongoza kwa *contribution*, mchango wake katika pato la Taifa katika nchi hii. Sasa maana yake ni nini? Yaani huwezi kusema kitu kinapelekewa hela ndogo lakini wakati huo huo matokeo yake ni makubwa. Sasa hapa hii ni elimu ya muda mrefu ya kuzungumzia *multiplier effect* ambayo Mheshimiwa Waziri Bashe alikuwa anajaribu kuieleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliamua niliseme kwa sababu tatizo ambalo lipo, kila mmoja anataka kutafsiri akiamini ni mchumi wakati hii kazi ni ya kwetu sisi wenyewe

ambao tulikaa darasani muda mrefu. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nimelisema hilo kwa sababu nilikuwa najaribu kuyaweka mambo sawa sawa na ndiyo maana unaona kidogo utulivu upo. Sasa... (*Kicheko*)

**SPIKA:** Nikubaliane na wewe tu, kwa kweli kama hujafanya hata *elementary economics* ni taabu kutafsiri haya mambo. Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na utangulizi huo mdogo ambao niliutoa, nimeona ni vizuri sasa niishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa miradi mikubwa ambayo Jimbo la Mombasa tumeipata katika kipindi cha miaka mitano. Tuna mradi wa maji Chitete Serikali ilitupa shilingi milioni 500; tuna mradi wa nyumba 20 za Serikali, shilingi bilioni mbili; tuna mradi wa skimu ya Naming'ong'o ya umwagiliaji, hivyo vyote vimekamilika, shilingibilioni 4.8; tuna mradi wa kiwanda cha chumvi kimekamilika kwa shilingi milioni 535 na pia tuna mradi wa soko la kimkakati la kisasa la mazao, shilingi bilioni nane, Waziri Jafo alikwenda kule juzi na akapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tuna mradi wa maji Ndalambo wa shilingi milioni 324; vilevile tuna mradi wa Kituo cha Afya cha shilingi bilioni 400 Kapele; tuna mradi wa *TASAF* kwa miaka mitano tumepata zaidi ya shilingi bilioni moja Halmashauri ya Mombasa na miradi mingine. *In total* Halmashauri ya Mombasa miradi ya maendeleo peke yake tumepata zaidi shilingi bilioni 30. Kwa hiyo, kwa hili kwa kweli wananchi wa Mombasa wamenituma kuniambia kwamba tunashukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, lakini vile vile wanamshukuru Rais Magufuli kwa kazi kubwa alioifanya na wamemwahidi kwamba Mkoa wa Songwe katika uchaguzi unaokuja tutaongoza kwa kura na tutatoa mfano kwa kazi maalum. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, bado niseme tu kwa kifupi sana hii nchi lazima tukubali matokeo ambayo

yamefanyika. Ili nchi iweze kubadilika lazima pawepo na watu wa kuonyesha maono na maono ni hii miradi mikubwa ambayo imefanyika katika hili Taifa. Kwa hiyo, unapozungumzia mradi wa *SGR*wenye matokeo chanya ya kiuchumi, mradi ule haufaidishi Chato peke yake ama maeneo mengine, mradi ule ni wa Kitaifa. Unapozungumzia ndege ambazo zipo sasa hivi, zaidi ya shilingi triliioni 1.2 zimeshatolewa mpaka sasa, mradi ule ni kwa maslahi ya hili Taifa letu lote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, angalia *Stiegler's Gorge*, zaidi ya shilingi triliioni saba zimewekwa pale. Haya yote ni matokeo ya kutaka kuihamisha Tanzania kutoka uchumi wa chini kwenda uchumi wa kati na baadaye tutakuwa uchumi mkubwa. Niwape moyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndiyo chama changu kipyaa, nikieleze wazi kwamba haya yanayoendelea, unapotaka kubadilika kimaisha utapata upinzani mkubwa, lakini baada ya muda wata-appreciate.

Mheshimiwa Spika, hiki kinachofanyika ni kwa kila mtu, hata sisi tuliokuwa tunasoma darasani, kuna watu tulilingana nao, baadaye wakaona tunawashinda, tunapata *division one* tunakwenda *form six*, tunapata *division one*, tunakwenda, tuna-move; walikuwa wanaskia wivu kwa nini hawa watu wanafanikiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni ku-keep on moving kwa sababu jukumu la kiuchumi halisubiri watu wakusifie. Jukumu la kiuchumi ni kutekeleza. Wajibu huo Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli anauweza, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inauweza, Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu na Mawaziri wengine wote mnauweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe rai kwa wenangu kwamba tu-appreciate kazi kubwa iliyofanyika. Hii miradi iliyofanyika ilipaswa ifanywe kwa miaka 15, lakini miradi hii imefanywa ndani ya miaka mitano, nasi sote ni mashahidi. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Safari hii nitaunga mkono hotuba ya bajeti pamoja na kuipigia kura ya ndio. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde. Nakushukuru sana kwa hotuba yako ya kufunga. Nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Haonga na Mheshimiwa Frank Mwakajoka jinsi wanavyotetemeka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Amina Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi. K wa kuwa dakika ni chache, niende moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, leo ikiwa ni mara yangu ya mwisho kuzungumza katika Bunge lako kwa kuchangia Bajeti ya Serikali, kipekee kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nakushukuru sana wewe kwa kuwa Bunge lako hili la Kumi na Moja limeandika historia, mimi nikiwa kama mwakilishi ambaye ninawakilisha watu wenye ulemavu. Tarehe 18 mwezi wa Sita mwaka 2018 katika Muswada wa *Finance Bill* tulipitisha Sheria ya nne nne mbili. Sheria hiyo ya nne nne mbili kipekee kabisa nakushukuru wewe kwa jinsi ambavyo uliuendesha ule mjadala na hatimaye 2% ikakubalika kwa watu wenye ulemavu. Nawashukuru pia Wabunge wote waliounga mkono jitihada zile. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, 2% kwa watu wenye ulemavu imekuwa na manufaa makubwa sana ambapo hivi sasa maeneo mengi watu wenye ulemavu wanachukua mikopo hiyo na wamejajiri. Kwa mfano mzuri, katika Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya llala, katika mikopo iliyotolewa, watu wenye ulemavu walipata shilingi bilioni tatu. Katika hizo, wengi wamejikita katika biashara za bajaji. Kwa hiyo, kazi kubwa

tulioifanya nami kama mwasisi wa hiyo 2% katika Bunge lako ninaondoka kifua mbele nikfurahia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako mengi yamefanywa katika Bunge hili, lakini kipekee tumpongeze sana Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa na jicho la ziada na kuvunja miiko na mitazamo iliyokuwepo hapo awali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Ikupa.

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa Ikupa, Taarifa.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayeendelea kwamba 2% ilianza mwaka 2016 ambapo liliulizwa swali la msingi na Mheshimiwa Stella Ikupa na hatimaye 2017 Bunge lako la bajeti pia nilichangia na *clip zipo* kwenye mitandao. Kwa hiyo, ye ye siyo mwasisi wa 2%. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina iruke hiyo, endelea na mengine. (*Kicheko*)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, katika Bunge lako kuhusu mjadala ule utakumbuka Mheshimiwa Ikupa aliunga Serikali mkono. Kwa hiyo, bado kwa kweli nitaendelea kukumbuka katika hilo pamoja na jitihada zake nzuri, niiweke wazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika tasnia ya habari, kwa sababu mimi ni mwana taaluma katika tasnia ya habari, katika Bunge hili tumeshuhudia Muswada wa Huduma za

Habari ambao uliletwa mwaka 2016. Muswada huo, ni moja ya mambo ambayo ni muhimu sana ya kuzingatia na yamesaidia sana kukuza weledi katika taaluma hii ya habari. Kufikia mwaka 2021 ninaamini kabisa kwamba wanahabari wengi wenzangu popote pale walipo watalifanya kazi hili na kuweza kunufaika na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ujio wa kidigitali umekuwa na manufaa makubwa sana kwa sababu hivi sasa vijana wengi wameweza kujiajiri na katika kujiajiri huko wameweza kwa kutumia *YouTube channel* ambapo kwa vijana wengi habari sasa zimekuwa ni kiganjani. Kwa hiyo hizi ni jithada nzuri sana ambazo zimefanywa na Bunge lako hili kwa kuweza kupitisha muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pia ndani ya miaka mitano Serikali imewapa rasmi waandishi uhuru wa kukosoa kwa haki na kisheria kwa kuweka kifungu namba 52(2). Hiki ni kifungu cha kihistoria ambapo sasa waandishi wanaweza kukosoa kama haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya watu wamekuwa wakikosoa kifungu hiki. Mimi niseme tu kwamba sheria hizi hazijaanza hapa kwetu na hata Uingereza pia wanazo sheria za makosa ya kimtandao. Na kwa kuwa tuna pia kwenye uchaguzi sheria hii itaweza kuwalinda watu wengi na kuleta manufaa makubwa. Kwa hiyo katika taaluma hii ya tasnia ya habari kwa kweli mimi najivunia sana yale ambayo yameweza kufanyika, hasa katika taaluma nzima ya kidijitali.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Arusha ni mionganini wa mikoa iliyoafidika na maendeleo yaliyofanywa katika mikoa hii mitano chini ya jemedali Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Katika Jimbo la Arumeru Magharibi tarehe 2 Disemba, 2018 Rais alikuja kuzindua mradi wenyewe zaidi ya bilioni 520; hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ya kupata mradi huu mkubwa wa maji mbele ya Rais pia niliweza kumwombwa barabara ambayo leo hii Rais aliridhia na mchanganuo tayari

umeenza na barabara ile inaanza kutengenezwa hivi karibuni. Pia ukienda katika Jimbo la Logido kaka yangu Kiruswa mradi mkubwa wa maji kutoka katika Mlima Kilimanjaro, wa Mto Simba umesaidia kwa kiasi kikubwa sana; vituo vyatya afya pia na mengine mengi. Kwakweli niseme kwamba tunayo kila sababu ya kumpitisha kwa kishindo jemedari huyu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli katika uchaguzi huu wa mwaka 2020 na kipeke kabisa kwako wewe umekuwa mfano...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante naunga hoja mkono na ninawatachia wote kila kheri, ahsante

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hawa Ghasia atafutiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kwa kuweza kuchangia. Nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya Bunge Tukufu na mimi niweze kuchangia. Niwashukuru wananchi wa jimbo la Mtwara Vijiji ambao wamenichangua Mbunge wao kwa vipindi vitatu mfulululizo, na nina imani kutokana na utekelezaji mzuri wa ilani wa Chama cha Mapinduzi ambayo tayari tulishaisoma kwao, na pia utekelezaji ilani ambao unafanywa na Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ushindi kwa Chama cha Mapinduzi katika Mkoa wa Mtwara utakuwa ni wa dhahili,

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa wa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake. Katika Mkoa wetu wa Mtwara tumeweza kupewa bilioni 157 kwa ajili ya upanuzi wa Bandari ya Mtwara ambao utawezesha meli yenye uzito wa tani 15,000 na makontena 4,000 kuweza kutia nanga na

kuweza kuhudumia wananchi kwa urahisi na hivyo zao letu la korosho kuweza kupanda bei. Pia nimshukuru Mheshimiwa Rais, uwanja wetu wa ndege umeweza kupewa bilioni 50.33 kwa ajili ya upanuzi ambapo utaweza kuwa na njia tatu za kurukia na pia tutawekewa taa na hivyo kufanya urahisi wa kuendeleza gesi yetu hasa kule baharini ambako suala la uwanja linahitajika kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais, tumepewa bilioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini. Pia katika halmashari yangu ya Mtwaraji Vijiji tumeweza kujengewa vituo vitatu vya afya viwili vikiwa vipyta kimoja kikiwa kinaboresha.

Mheshimiwa Spika, tumeposta hospitali ya wilaya, na pia vituo vyetu vya afya ambavyo vilikuwa ninafanya kazi kama zahanati sasa hivi vinaweza kufanya upasua jili na hivyo kupunguza vifo vya akina mama. Kwa hiyo, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti nibishane na takwimu na Mheshimiwa Halima Mdee, kwamba vifo 11 kwa mwaka, hizo si taarifa sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, sisi kule wamakonde ikiwa mtu anaimba nyimbo nzuri sana na mwingine akawa haupendi ule wimbo kuna kitu tunaitwa kuyang'anija; yaani anaweza akaenda kama kuvuruga hivi. Kwa hiyo alichokuwa anakifanya Mheshimiwa Halima Mdee ni katika kupunguza katika masikio yetu tusikie mafanikio ya Chama Cha Mapinduzi. Kwa hiyo alikuwa anatoa taarifa za uongo, pamoja na za kilimo na za afya. Unasema tumeandaa *perform* kwenye kilimo ilhali hatuna njaa na tunapeleka chakula nje.

Mheshimiwa Spika, humu ndani wote tumeshiba hatujasikia njaa inazungumzwa popote; sasa *under performance* hiyo inatokana na nini? Lakini ile yote ni kwamba wimbo mzuri wa mafanikio wa chama cha mapinduzi yeye alikuwa hataki kuusikia ndiyo maana akaja na takwimu za uongo ambazo alikuwa anazipeleka kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais, kwa maelekezo yake barabara yetu toka Mtwara kwenda Newala hadi Masasi Kilomita 60 zilizobaki namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba Benki ya Dunia imekubali kugharamia ujenzi na wako katika hatua za mwisho na barabara hiyo itajengwa yote kwa pamoja na itakamika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sina wasiwasi hata kidogo, kuanzia jimbo langu na majimbo mengine yote ya Mkoa wa Mtwara yataenda mikononi mwa Chama Cha Mapinduzi kwasababu ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 90. Hayo mengine ya Mheshimiwa Mdee ni katika tu kufurahisha shughuli ambayo kwa kweli kwa upande wao mambo ni magumu na sijui kama tutakuja kukutana mwezi wa kumi na moja.

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali yangu, katika ile miradi ambayo kwishafanyiwa upembuzi yakinifu, ikiwemo Barabara ya kutoka Mtwara kwenda Msimbati na Kilambo, na upembuzi yakinifu umekamilika, fidia watu wameshaanishwa basi walipwe ile fidia kwasababu pesa ipo *TPDC* na ile barabara ijengwa na ikamilike kwa wakati. Nimshukuru Mheshimiwa Rais na Waziri wa Nishati nimeambiwa kwamba vijiji vyangu vyote 24 vilivyobaki katika jimbo la Mtwara Vijijini wakandarasi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia nakushukuru.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee ulikuwa unaambiwa ukiona inafaa baadaye nikupe dakika tano za kuaga Kawe. Mheshimiwa Emmanuel Papian,

Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae atafauta Mheshimiwa Mchengerwa. (*Kicheko*)

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nitaomba angalau dakika moja niweze kumaliza jambo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliafu Bunge lako Tukufu kwamba yule mfugaji aliyejekwa analia kwenye vyombo vya habari kwa kutaifishiwa mifigo yake jana saa sita mchana tumeshinda kesi katika Mahakama ya Rufaa, anatakiwa kurudishiwa mifugo yake na sasa tunakwenda kushughulikia yule bwana kurudishiwa mifugo yake; na kama haipo Serikali ichukue jukumu la kumnunulia mifugo yake ili aweze kurudi barabarani ilo jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo pili, mimi nilipoteuliwa na Kamati Kuu kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi na hatimaye kushinda nilipewa kazi moja tu. Kwamba, nenda Kiteto ukaongeze wale watu baada ya maafa makubwa na matukio mengi yaliyojitekeza Kiteto iweze kuwa salama. Mimi nimemaliza kazi yangu; Kiteto ni salama, wakulima na wafugaji wanakula, wanakunywa na wanatembea pamoja; ndiyo kazi pekee kubwa niliyopewa kwa ajili ya kuleta amani Kiteto.

Mheshimiwa Spika, kazi nydingi zimefanyika Kiteto, miradi ya maji ipo, umeme upo, afya imefanyaka, vituo vya afya vimejengwa, shule zimejengwa, barabara zimejengwa.

Mheshimiwa Spika, ombi! Nilitaka kuomba juu ya hizi barabara za *TARURA* tunazotengeneza vijijini; kwa nini kusifanyike jambo angalau la kupunguza asilimia hata tano kutoka *TANROAD* ije *TARURA* ili tuweze ku-*overcome* hizi barabara zetu za vijijini ambazo ni kubwa na zinatakiwa kutengenezwa kwa sababu zinaharibiwa na mvua kipindi kirefu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaombi jingine kubwa Serikali tunaomba katika bajeti ijayo na *plan* zilizopo tupate

soko kubwa la mazao ndani ya wilaya yetu, ambalo litasaidia Kiteto Kilindi, Chemba, Kondoa, Simanjiro ili tuweze kuwa na *collective market* ya mazao.

Mheshimiwa Spika, tuombe sasa, baada ya hapo Serikali, kwa sababu ya ahadi ya barabara Kiteto, *NARCO* itujenge lami ili mazao yetu yaweze kutoka kwa urahisi na wakulima wetu wapate faida.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo nimeona kwenye bajeti. Benki ya Kilimo imekaa muda mrefu sana haina bodi. Tunaomba mamlaka zinazoweza kuteua bodi ziteue bodi ili benki iweze kuendelea kufanya kazi, *i-support* wakulima; vingine benki *ime-stack*, haiendelei haifanyi chochote na benki ya *investment* kwa upande wa *agriculture*. leo tunavyozungumza kilimo kinachotakiwa kuchangia kodi na mapato ya taifa halafu hawana bodi wanafanyaje kazi? Tunaomba *instruments* zote zinazowezekana, na sidhani kama Mheshimiwa Waziri anajua jambo hili, sidhani kama Gavana anajua jambo hili, na sidhani kama Mheshimiwa Rais anajua hili jambo. Bodii ndicho chombo pekee kinacho-*allow* benki kuweza kufanya kazi; *otherwise imesisima*, haitoi mikopo na mwisho wa siku benki haitazalisha. Hawa wakulima tunaowapangia kuwatengenezea benki ni ya nini kama haiwezi kufanya kazi?.

Mheshimiwa Spika, naomba mamlaka ianze mara moja itengeneze bodi watu wafanye kazi, kazi iendelee waongezewe mtaji iweze kupeleka mikopo kwa wakulima wetu ambao leo tupo humu tunawatetea.

Mheshimiwa Spika, mwisho! Niliona kwenye kitabu wamepeongeza Benki ya *Exim*; kwamba imefuata zile taratibu za *BOT* katika kufuata zile taratibu baada ya Corana kupunguza riba na *ku-structure* mikopo ya watu.

Mheshimiwa Spika, ningependa mamlaka ipongeze benki zote zilizofanya. Benki ya *CRDB* *ime-of set interest* na kusimamisha *repayment* kwa wazalishaji wa maua na wafanyabiashara wote wa maua nchini *for six month*;

wanastaili pungezi kama wengine hawa. Ningombwa NMB na benki zote zilizopo hapa nchini zipewe pungezi *collectively*; kwasababu tusipofanya hivyo tunaweza tuka-demolaze.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru sana ninajindaa kurudi jimboni ili niweze kurudi humu ndani salama. Nikirudi nitaomba, mimi nawewe, ni tufikirie ni namna gani ya kuondoa sheria ya kutaifisha mifugo inayokuwa kwenye hifadhi. Kutaifisha mifugo si jambo zuri linalotaiwa kusikika. Mheshimiwa Rais ameondoa kwenye maeneo ya kifugaji...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Papian.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Hilo tunakubaliana kabisa kimsingi; yaani hilo tutashughulika nalo Mungu akitujaalia. Hakuna kitu kibaya kama kumtaifishia mtu; malii metoka kwa Babu amehangaika maisha yake yote, baba, sasa wewe mjukuu eti kwa sababu ng'ombe wasiokuwa na akili wame-*cross boarder* basi wataifishwe wote, hii ni sheria ambayo haikubaliki kwa kweli; yaani haina ubinadamu wowote ndani yake. Na sheria hutungwa na sisi na hufutwa na sisi Bunge hili kwa hiyo ni moja ya maeneo ya kuyatazama haya yamebaki kama kiporo wala hilo halina haja ya kubishana huko mbele lipo liko wazi tu. (*Makofi*)

Ila lile neno la kusema benki zote zipongezwe kwa kupunguza riba nakubaliana na wewe lakini ile benki iliyokopesha Waheshimiwa Wabunge ile zile riba mbona hawapunguzi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna Benki moja ilikopesha Wabunge riba za ajabu. Hebu ongea ongea nao tuone nao wema wao wapunguze ile riba. (*Makofi/Kicheko*)

Nafikiri Waheshimiwa mnaafiki! si ndivyo?.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Cosato Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kwa kipekee napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia wananchi wenzangu wa Jimbo la Mafinga Mjini na zaidi Chama cha Mapinduzi ambacho kiliniona kwamba ninafaa kwenda kuwa mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini na wao wakanithibitisha na hapa nipo nafanya kazi na nitaendelea kufanya kazi yao.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii niseme kwa msemo wa kikwetu wa kihehe; *muwewilikoko*; uoga ni adui sana, na hii ilithibitika wakati ule masuala ya Corona yako kwenye *pic* Mheshimiwa Rais alituondolea uoga na kwa kweli kukawa na utulivu. Uoga ni adui mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi muwewilikoko kwa sababu gani, kuna watu wanapita Jimbo la Mafinga Mjini kwa uoga wanasema Chumi hagombei. Napenda kuwaambia wananchi wa Mafinga Mjini Chumi nagombea tena. Yaani kwa uoga, wameshaishiwa mpaka wanasesma Chumi hagombei, sasa huo ni muwewilikoko mimi nitagombea, nipo.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa usikivu wake hasa wakati ule.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chumi kuna mtu anakupa taarifa, nani!

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, Haonga.

## TAARIFA

**SPIKA:** Haya Haonga.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, asiogope watu kupita kwenye Majimbo, ye ye ni nani kwa sababu Jimbo la Mheshimiwa Mwigulu anapita Professa Kitila kila siku na anafanya kazi nzuri kule Jimboni japo atachukua Mheshimiwa Jesca. Jimbo hili la Mheshimiwa Nsanzugwanko anapita Mama Ndlichako pale kila siku na upepo wa Nsanzugwanko kidogo umeyumba. Jimbo la nanii...

**SPIKA:** Hapana kaa chini hizo si taarifa Mheshimiwa Haonga. Mbona hujasema kama Jimbo lako CCM inachukua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Zambi anarudi, Mheshimiwa Chumi endelea.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, mdogo wangu Mheshimiwa Haonga hajanielewa. Nimesema muzewilikoko; yaani kwamba wale wanaopita pita wana uoga to the extent kwamba wanaanza kusema kwamba Chumi hagombei. Yaani wameingiwa na uoga sasa wananiogopa mpaka wanasema sigombei, nadhani umenielewa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa usikivu. Alipopita pale Mafinga kuna masuala tuliomba na yakatekelewa; ikiwa ni pamoja na kuomba kuruhusu mazao ya misitu yasafiri masaa 24, kuomba *transfoma*, lakini pia kuomba majengo yaliyokuwa ya mkandarasi yatumike kama kituo cha afya ambayo sasa tumeshakabidhiwa. Hayo ni kati ya mengi ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya katika Jimbo la Mafinga Mjini; ikiwa ni pamoja na miradi ya maji, Kituo cha Afya cha pale lyongole, pamoja na masuala ya ujenzi wa barabara pamoja na kuwa bado uhitaji ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kumshukuru pia Makamu wa Rais; alipokuja pale lyongole alipoweka Jiwe la Msingi Kituo cha Afya cha lyongole kuna maelekezo aliyatoa na ushirikiano mwangi aliufanya ambapo Halmashauri ya Mji wa Mafinga imeufanya na kutekeleza. Pia Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa Ziara yake; lakini pia kwa kushirikiana na mimi kuhakikisha kwamba sekta ya mazao ya misitu inakuwa na utulivu. Sasa hivi hakuna tena ujanja ujanja wa watu kupata vibali, sekta imetulia vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini shukrani zangu pia kwako Mheshimiwa Spika, Naibu wako, Katibu wa Bunge, Maafisa wako na hata pale Kituo cha Afya kinachoweza kutupa huduma sisi. Kwa kweli watu wanafanya kazi kwa weledi na kwa upendo mkubwa. Hata pale Kantini ni *full* upendo, lakini pia hata Maaskari katika maeneo ambayo tunaingia wanatukagua kwa upendo. Haya ni mambo ambayo yanetuwezesha kufanya kazi vizuri. Kama huwezi kushukuru haya basi wewe unakuwa si mtu muungwana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia sitasahau upendo ndani ya *Bunge Sports Club*, pamoja na mapungufu ya hapa na pale lakini tumeishi kwa upendo. Na ninakupongeza Mheshimiwa Spika, miaka yote umehakikisha kwamba tunashiriki katika michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata wenzangu katika mtaa huu tunauita *maisha plus*, alikuwepo Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Mwenyekiti Dada Lucy; tumeishi kwa upendo na maelekezo na kuniongoza maana mimi ni mara ya kwanza lakini sasa nimeduwa ni mtu ambaye hata naweza kuchangia kwa ufanisi mzuri. Mungu awabariki sana wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nije sasa katika masuala muhimu; kwanza kitaifa. Kuna watu wanajenga picha kama vile Serikali ya Mheshimiwa Magufuli haikubaliki kwa vyombo vya kimataifa na washirika wa maendeleo. Nataka niwathibitishie, kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri washirika wa maendeleo mpaka kufikia

Marchi, 2020 katika kile walicho-*pledge* wametoa kufikia asilimia 93. Hiki kithibitisho kwamba Serikali yetu inakubalika na inaaminika kimataifa na pia kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme kuhusu sekta ya usafirishaji. Nimwombe Mheshimiwa Rais; amekutana na makundi mengi sana hapa nchini; akutane na madereva katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kwa sababu muda wangu kidogo ulitaka kupotea, naomba dakika moja, niseme ninaomba Serikali iruhusu baadhi ya Miji ambayo kiukweli kibiashara ifanye biashara masaa 24, huwezi kuja pale Mafinga saa nne unawaambia watu wafunge biashara, tunataka uchumi usisimke, Polisi kazi yao ni kulinda dola. Sasa hivi ilivyo kwa sababu ya Sheria saa 4 Sheria ndivyo inavyoongoza wanatakiwa wazule biashara. Sasa kuna Miji jinsi ya *nature* yake Miji kama Mikumi, Ruaha Mbuyuni, au hapa Dodoma au Mafinga watu waruhusiwe wafanye bishara masaa 24. (*Makof!*)

Mhesimiwa Spika, naona hili ni jambo ambalo la muhimu litasisimua uchumi, litaongeza mapato kwa mtu mmoja, lakini kwa taifa hii mambo iko dunia kote... (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuunga mkono hoja, lakini hilo litazamwe sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana, nakubaliana na wewe kabisa yaani *actual/litazamwe* kwa nchi nzima, *unless* yale maeneo ambayo yanakila sababu labda yana changamoto za kiusalama na hata kule Kongwa, sasa saa nne watu wanaenda kulala wapi bwana, bado, kuwalaza watu saa nne ina madhara yake. Maana saa nne tu ushalala, watu usingizi hawana, sasa ukishawalaza watu saa nne basi yafuatayo yanafurahisha. Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. (*Makof!*)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, kwa misingi ile ile ya Kibunge...

**SPIKA:** Atafuatiwa na Zainab Katimba.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, na kwa kuzingatia kwamba kumbukumbu za Bunge hili Tukufu zina mudumu karne na karne na zitatumika na vizazi hivi na vizazi vijavyo nikuombe Bunge lako tukufu kwa misingi ya Kanuni ya 64 na Kanuni mbalimbali za Bunge la Kudumu basi kufuta *paragraph* iliyopo katika taarifa ya Mseji wa Kambi Rasmi upande wa pili inayozungumzia kuhusu tukio la Mheshimiwa Mbewe kwamba alitekwa na kuvamiwa, na hii inatokana na taarifa za kishahidi na misingi iliyopo katika Sheria za kijinai. Kwa sababu Jeshi la Polisi limetoa taarifa ya tukio zima lilitotokea wakati Mheshimiwa Mbewe alipopata matatizo hiyo siku ya juzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe utoe ridhia kwamba taarifa ile ya Kambi Rasmi iliyowasilishwa na msemaji iweze kuondoa kipengele kile kwa kuwa Kikanuni jambo hili iwapo lisipoondolewa litadumu vizazi na vizazi na kwa kuwa kilichosemwa ni taarifa ni uwongo basi nikuombe uweze kuridhia kwenye eneo hili, lakini... (*Makof*)

**SPIKA:** Kwa nusu dakika tu Mheshimiwa Halima unatolewa ushauri tufute pale tuondoe, nakupa kanusu dakika kama una sababu vinginevo nyamaza tuendelee, shukrani amekubali tuondoe, endelea Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kutambua pia kwamba...

**SPIKA:** Sekunde tu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, amua unachoona kinafaa kwasababu wewe ndiyo una mamlaka.

**SPIKA:** Ahsante sana ninachoamua kwasababu taarifa ya Polisi tayari imetoka kwamba jambo la kutekwa na nini halipo, wala halikuwepo. Kwa hiyo, tunaiondoa paragraph hiyo kwenye Hansard, endelea Mheshimiwa Mchengerwa.(*Makofi*)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo ya Sheria za Kimataifa tuwaombe ndugu zetu mashirika ya Kimataifa na Balozi mbalimbali hapa nchini, zitambue kwamba Taifa hili ni Taifa huru. Masuala ya ndani ya nchi, ni masuala ya uhuru wa nchi, wakati fulani tumeona baadhi ya Balozi zikitoa taarifa kuhusu tukio hili la kusikitishwa kutekwa kwa Mheshimiwa Mbewe.

Kwa hiyo, tuwaombe wazingatie Sheria za Kimataifa kwamba *Tanzania is Sovereignty State*, hii ni nchi huru hatupaswi kuingiliwa kwenye misingi ile ile ambayo nimeizungumza hapo awali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hotuba iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Mpango hotuba ya Mheshimiwa Dkt, Mpango imejaa uzalendo wa hali ya juu, imejaa ujasiri, matumaini na dira ya Taifa letu, inazungumza tulipotoka, tulipo sasa na kule tutakoelekea. Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango imejikita katika maeneo mengi hususani kwenye eneo la afya, eneo la kilimo, eneo la elimu, maji, nishati na maeneo mengine, sisi jumla wananchi wa Jimbo la Rufiji lazima tuseme kwamba hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango inaonyesha utekelezaji wa ilani kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekamilisha utekelezaji wa ilani kwa zaidi ya asilimia 100, kwa hiyo tunashukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi iliyofanya. Lakini yako mambo mawili ya kuzingatia iwapo tunataka tufanikiwe kama Taifa, iwapo tunataka tuliopeleke Taifa hili katika dunia ya kwanza basi yako mambo mawili lazima tuzingatie, jambo la kwanza ni aina ya utawaka tulionao sasa. Ili tuweze kwenda kwenye dunia ya kwanza basi ni lazima Taifa letu lizingatie kwamba namna ya utawala wa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli tuweze kwenda nao angalau kwa miaka 20 miaka 30,

ninaamini Taifa hili litapiga hatua na litakuwa dunia ya kwanza kabisa, ninasema haya kwasababu ya maamuzi magumu ambayo Rais wetu Dkt. John Joseph Magufuli anayafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nishauri kwenye la upatikanaji wa kodi ambalo Mheshimiwa Dkt. Mpango hajalizungumza vizuri, kwenye taarifa yake ya hotuba. Tunayo madini yanaitwa madini ya magadi yaani *caustic soda*, madini haya yanayopatikana katika mlima wa Oldonyo Olengai, madini haya katika mlima ule yanatiririsha madini haya katika ziwa lile zaidi ya *metric* tani milioni 1,300,000. Lakini kama Taifa letu tutaamua kuyafuna madini haya tunaweza kuvuna kila mwaka tani 360,000.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia kwenye takwimu za soko la dunia madini haya kilo moja yanauzwa dola 165 ina maanisha *cometric* tani 3,60,000 ambayo tukiamua kuyavuna Taifa letu litapata dola bilioni 59, hizi ni fedha nyingi sana tumuombe Waziri wa Fedha na Wizara zote zinazohusika kuangalia uwezekano wa *utilize*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna tutakavyoweza kuendelea kuchelewa wenzetu wa nchi jirani kule Kenya wameanza ku-*utilize* mto Mara maana ya ku-*utilize* mto Mara maana yake ni kwamba maji sasa hayataingia Serengeti, pia tukumbuke kwamba kuna Flamingo wanaozaliwa katika hili, na kwamba Flamingo wote waliopo Afrika wanatoka katika hili hili ambalo ninalizungumzia.

Nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha basi muweze kuona uwezekano wa kufanya ku-*utilize* madini haya ili Taifa letu liweze kupiga hatua na baada ya miaka 20 taifa hili litaweweza kutoa msahada katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mchengerwa, mimi kama mhifadhi nikuambie usiwe na wasiwasi na Flamingo, wote wa Afrika Mashariki ni watanzania, ila huwa wakisha zaliwa Tanzania basi wanakwenda Kenya, Lake Bariko, Lake Nakuru nakadhalika, lakini wakishakuwa na kufika mahali pa kupata kutaka kutaga mayai lazima warudi Tanzania, Lake Natron, Lake Manyara, Lake Eyasi nakadhalika, wakishazaliwa vifaranga wakikua kidogo wakishakuwa watanzania ndiyo wanakwenda nchi jirani. Kwa hiyo, kuna maajabu mengine ambayo watanzania tumependelewa sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Zainab Katimba, halafu atafuatiwa Mheshimiwa Kamishna Mary Chatanda, na Prof. Jumanne ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Awali ya yote nipende kwanza kupongeza kazi kubwa sana ambayo imefanya na Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Magufuli katika Awamu hii ya Tano amefanya kazi kubwa sana na niwapongeze wasaidizi wake wote kwa kumsaidia kazi na kuweza kutekeleza ilani kwa kiwango kikubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mbunge na ni kijana kuna kitu kikubwa sana pamoja na mambo mengine ya uchapakazi pamoja na mambo mengine mengi ambayo naweza kujifunza kutoka kwa Mheshimiwa Rais, lakini nimejifunza kitu kikubwa ambacho ninaweza nikasema kwamba kuna neno wanasema kuna *phrase inasema if you don't stand for something you will follow for everything*, yaani kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba usipokuwa na malengo, mipango, vipaumbele, na kuvisimamia utashia kupapasapasa kila mahali na kukosa cha kushika au kwa lugha jingine unaweza ukasema usipokuwa na msimamo utayumba, au usipoweza kusimamia unachokiamini hautofanikiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hiyo imekuwa ni dhahiri kutoka kwa Mheshimiwa Rais ambaye ameonyesha ujasiri mkubwa sana, msimamo mkubwa sana na kutokuyumba katika janga

la *corona*, katika nchi hii ambayo dunia nzima imeonekana ikitetereka, lakini sisi kama watanzania kwa uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais ameweza kudhihirisha kwamba ukiwa unakiamini kitu, ukiwa umefanya maamuzi yako uyasimamie usiyumbe mpaka mwisho na usipoweza kusimamia maamuzi yako mpaka mwisho utapapasa na hautofanikiwa. Kwa hiyo, kama jina nimejifunza *if I don't stand for something I will follow for everything*, kwa hiyo, kitu cha muhimu katika maisha na vijana wenzangu wajifunze ni kwamba lazima tuwe tuna mipango, tuwe tuna malengo, tuwe tuna vipaumbele tuvisimamie na mwisho wa siku tutafanukiwa kama tunavyoona Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli anafanikiwa katika utekelezaji wa llani ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Viongozi wengine kwa mfano Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye na yeye amekuwa ni kielelezo kikubwa sana cha Uongozi Imara wa mwanamke na sisi vijana na hasa sasa vijana wa kike tunaendelea kujifunza vikubwa sana kutoka kwake. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye yeye ameonyesha busara ameonyesha unyenyekevu lakini uchapakazi. Lakini pia nipongeze viongozi wengine wote lakini Chama Cha Mapinduzi kwa utekelezaji kwa utekelezaji wa llani kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nipongeze pia Mheshimiwa Waziri Mpango pamoa na timu yake kwa kazi kubwa wanayofanya hakika Waziri huyu ni mchapakazi na hilo halina ubishi. Serikali ya Awamu ya Tano imeweza kuwasaidia sana vijana imeweza kuwagusa sana vijana, kwanza imetoa fursa nyingi za vijana kushika nafsi mbalimbali za uongozi tena uongozi nyeti ndio maana tunaona kwanza kuna nafasi ambazo zipo kwa ajili ya vijana kuingia ndani ya Bunge lakini kuna nafasi nyingi za uteuzi kwa ajili ya ambao vijana wengine wameteuliwa kuna Wakuu wa Mikoa, kuna Ma-DC, kuna RAS, kuna Wakurugenzi nafasi mbalimbali mpaka katika ngazi za chini tunaona vijana tumeaminiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwaomba vijana wenzangu wote tuweze kufanya kazi kwa

weledi uaminifu, umahiri ili tusimuangushe Mheshimiwa Rais wetu ambaye ameonyesha kutumini sana sisi vijana . lakini kuna masuala... (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamishina Mary Chatanda atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib halafu Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti ya 2020/2021. Naanza kuunga mkono hoja nampongeza Mheshimiwa Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli lakini nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu wa Wizara na watumishi wote wa Serikali kwa namna ambavyo wamewezesha nchi hii kupata maendeleo kuitia bajeti mbalimbali ambazo tumekuwa tukizipitisha ndani ya Bunge hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawiwa kusema kwamba Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ni dume la mbegu tena mbegu bora ni ukweli usiopingika amekuwa ameisaidia nchi hii kusema ukweli kuweka mipango mizuri ya Serikali kupatikana fedha ili ziweze kufanya shughuli za maendeleo hakuna anayebisha katika hili na ndio maana kila anayesimama hapa anamsifu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kulisimamia hili na ndio maana tumepata maendeleo.

Kule kwangu Korogwe nimepata barabara za lami katika ule Mji wa Korogwe na barabara zinaendelea mpaka sasa kujengwa za lami. Pale kwangu Korogwe nimepata fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba nya maadarasa pamoja na mabweni kwa ajili ya shule za sekondari na shule za msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kule kwangu Korogwe nimepata miradi ya maji ikiwemo mradi mkubwa ambao ni wa India ambao tume katika ile Miji 28 fedha ikishakuwa imetoka tayari tutakuwa na maji ya kumwaga katika Mji wa Korogwe. Kwa nini tusimsifu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika hili! Namshangaa aliyesema hapa kwamba madeni mnajisifu suala la kusamehewa madeni hakuna ambaye hajakopa hata yeye mwenyewe amekopa alipoingia ndani ya Bunge amekopa, hivi akiambiwa yeye anasamehewa deni leo ataacha kufurahi? Kwa hiyo, suala la kukopa ni suala la kawaida huko Marekani kwenyewe wanakopa, huko Uingereza wanakopa sio ajabu kwa Tanzania sisi tumeonyesha nidhamu ndio maana wamesema wanatusamehe. Kwa nini tusifurahie kusamehewa mkopo! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe tu yule ndugu yangu naona ulimi wake uliteleza basi ajue kwamba Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni mwaminifu ndio maana wamekubali kutufutia hiyo mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe kaka yangu nakuhakikishia narudi ndani ya Bunge hili. Dada yako nitasimama tena kuhesabia kura zako unarudi kuwa Spika wa Bunge hili umefanya mambo makubwa kabisa ya kuliendesha Bunge hili *ki-standard* umerekebisha watu waliokuwa wanayumbayumba huku mara hivi vurugu ndogondogo unawaambia *stop!* Nakuhakikishia unarudi kule kwenye Jimbo lako hata yule aliyekuwa anakuchezea ukamuonyesha kidogo yule nadhani safari hii hawezи kuchukua, kwa hiyo, wewe sasa ukisharudi hapa dada yako nakuhesabia tena kura na Mheshimiwa Naibu Spika namuombea anaenda kupita kule Mbeye na anarudi kuwa Naibu Spika hapa. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamishana ile bakora bado ipo. (Makofi/Kicheko)

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii sasa kushukuru kwenye taarifa aliyoisoma

Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameonyesha kwamba zimetengwa fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ambayo imeharibiwa na mvua nyingi ambazo zimekuwa zikiendelea katika nchi hii. Kwa hiyo, niombe sana hata kule kwangu Korogwe barabara nyingi zimeharibiwa fedha hizi zikishapatikana basi tunajua kwamba zitarejesha miundombinu ile yote ambayo imeharibika katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda tu angalau niweze kusema haya machache kuishukuru sana Serikali kwa waliyotutendea lakini niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini kwa kuniwezesha kunipa nafasi ya kuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini mwanamke na nimefanya mambo makubwa kwa kushirikiana na Serikali yangu. Kwa hiyo, nina matumaini makubwa kwamba nitarudi ndani ya Bunge hill bila wasilwasi nitaungana na Waheshimiwa Wabunge wengine wenzangu wote ambao tutaweza kurudi ndani ya Bunge hill na wewe tutakuwa na wewe kama Spika wetu. Mwenyezi Mungu akubariki ambariki Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na watendaji na viongozi wote ambao wanafanya kazi katika Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khatib atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. KHATIB SAID. HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nichukue fursa hii muhimu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kusimama hapa na kuongea leo na nadhani ndio itakuwa mara ya mwisho kuongea katika Bunge hill na kipekee nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru watu wa Konde walioniamini kwa vipindi viwili mfululizo kuwawakilisha katika Bunge hill la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania niwaambie watu wa Konde ahsante sana nimekuja nimewawakilisha inavyotakiwa na nitarudi Konde naomba wanipokee na maamuzi yatakayofuata tutayafanya tukiwa huko.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nikushukuru wewe binafsi kwa jinsi ulivyotusimamia katika kipindi chote cha Bunge hili Mwenyezi Mungu akujali salama ukijaliwa kurudi kheri ukijaliwa hukurudi pia ushukuru.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nitumie fursa hii kumshukuru Kiongozi ambaye hapo mwanzo tulikuwa naye katika chama hichi alikuwa Katibu Mkuu wa Chama chetu cha Wananchi CUF lakini kwa bahati mbaya akatuacha mimi naendelea kusema ni Kiongozi ambaye tumekuwa muda wote tukitumia falsafa zake na siasa zake kwa kuamini kwamba ni kiongozi bora na ataendelea kubaki kuwa Kiongozi bora katika Taifa hili, huyu ni maalimu Seif Sharif Hamad nasikitika leo bado niko CUF na yeye amekwenda Chama kingine lakini bado mema alioyakitendea chama hiki yataendelea kubaki historia na milele na milele. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nataka niseme hivi, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ametenda aliyoweza kutenda katika utawala wake. Yapo mengi mazuri na hapa mbele yangu ninae Makamu Mwenyekiti Naibu Katibu Mkuu wa Chama. Nimejaribu kumuuliza hivi hapa hivi kuna dhambi kwani kusifu mazuri yanayofanya na Serikali, akaniambia hakuna dhambi, hakuna dhambi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hili nataka nimsifu Mheshimiwa Rais katika maeneo mawili kidhati kabisa. Nataka nimsifu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia anachokiamini na kipekee nataka nimsifu pale juzi alipokuwa Mtumba akaeleza wazi kwamba ataheshimu Katiba kwa kukaa katika kipindi chake cha utawala cha miaka kumi tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nataka nimsifu kwa sababu anajua umuhimu wa kulinda na kuisimamia Katiba kwa mujibu wa kiapo alichokula. Ni vyema tukajua sote tumeapa kuiti Katiba, mazuri anayoyafanya Mheshimiwa Rais wetu yatabaki kukumbukwa na warithi wake watatoka either CCM au pengine popote, lakini bado si *certificate* ya

kumfanya ye ye afikirie tutamgeuza akawa ye ye tuone hatatokea mwingine zaidi yake. Tungeyafikiria hayo kwamba Mheshimiwa Kikwete ndio mwisho wa kufikiri leo tusingempata Mheshimiwa Magufuli, naomba muelewe hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kadri ambavyo tunaona Mheshimiwa Rais Magufuli anafanya mema mengi na kusifiwa, nina hakika ndani ya CCM atapata warithi wazuri sana na mkikosa huko Wapinzani wapo wazuri sana wata-take over.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa hivyo turidhike na Katiba inavyosema na napenda nikwambie....

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib pokea taarifa tafadhali.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nampa taarifa mzungumzaji. Professa Lipumba sijui ana miaka mingapi kuwa Mwenyekiti wa Chama chao. Hiyo Katiba kweli anaizingatia, alikimbia kwenda Burundi akarudi hata Maalim Seif, Katibu wake miaka mingapi? Hiyo Katiba wanazingatia? Ukienda CHADEMA Katiba wanazingatia? Mheshimiwa Mbowe ana miaka mingapi kwenye Kiti? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Pokea taarifa Khatibu, pokea taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Keissy, Katiba za Vyama si Katiba ya Nchi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Katiba ya nchi ni kitu mbali na Katiba ya Vyama ni vitu mbali. Ninachotaka kukwambia na tena especially nataka nimwambie Mheshimiwa Keissy *this is United Republic of Tanzania Democratic Country, this is not Sultanate of Tanzania*. Kama umezoea Oman kwenye Usultani, Usultani hautakuja Tanzania. Rais atakaa kwa mujibu wa Katiba nchi hii haitawaliwi kisultani na kule Zanzibar

aliondolewa Sultani kwa sababu tupate nchi za kidemokrasia. Kama una ndogo ya Usultani rudi kwenu Yemeni ukatoe pendekazo hilo. (Makof)

**SPIKA:** Aaaaah, sasa Mheshimiwa Khatibu hapo umeharibu. Unajua cha kufanya.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi, nafuta hilo neno.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy amefuta hayo maneno, ni maneno ya kibaguzi, ni maneno yasiyofaa. Amefuta hayo maneo basi tuendelee.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, afute hayo maneno mara moja. Kwanza hata ye ye mwenyewe ukimchunguza ni Mkongomani huyo, Waarabu walimtoa wakamleta huku. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Sasa mtaniweka mahali pagumu sasa. Sasa ngoja ninyi watani wa jadi, naomba iishie hapo hiyo.

**MHE. KHATIB SAIDI HAJI:** Mheshimiwa Spika, ngoma droo.

**SPIKA:** Eee, ngoma droo basi iishie hapo eee. (*Kicheko*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo ninachomalizia kwa kusema pamoja na mazuri...

**SPIKA:** Waheshimiwa, Waarabu wa Pemba hawa wanajuana kwa vilemba.

**MHE. KHATIB SAIDI HAJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri yote niwakumbushe CCM tunarudi kwenye uchaguzi. Mheshimiwa Rais ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya nchi hii. Mheshimiwa Rais amefanya kazi na kazi yake ndio inayokwenda kumpeleka kuomba kura. Wapo Wabunge humu wanadhani watabebwa kwa sababu wao

wako kwenye Chama Tawala, muondoe hilo na kwamba Rais angejua ana Jeshi atalitegemea katika uchaguzi asingefanya kazi anayoifanya ili Watanzania wamwamini na wampe tena kura.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo niwaambie wale Wakurugenzi wa Halmashauri waliojitega kufanya waliyoyafanya Serikali za Mitaa watanzania wapo macho na hatutokubali uhuni ule urudiwe katika Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Professa Jumanne Maghembe atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi najua nafasi ni kidogo lakini umenikubalia kunipa nafasi hii. Kwanza ningependa nimpongeze sana Waziri Dkt. Mpango kwa hotuba nzuri sana. Kwa kweli hotuba hii ni kama *icing* ya ile miaka mitano ambayo tumekuwa hapa katika Bunge letu hili la Kumi na Moja, pongezi sana na nawapongeza na wasaidizi wake kule Wizara ya Fedha kwa sababu ya muda sitawataja majina yenu.

Mheshimiwa Spika, kwa pamoja ukiangalia bajeti hii ya mwaka huu, bajeti ya mwaka jana utaona kwamba tunavyokwenda na hii miradi ya kimkakati tunayoenda nayo, inatufundisha kitu kikubwa sana. Kwamba tukienda kwa nguvu hizi kwa miaka mitano hii inayokuja, tutaingia kwenye Taifa la uchumi wa kati. Kulikuwa na wakati tunakuwa na hofu hofu kidogo kwamba labda hatutafika huko, lakini sasa nina uhakika kabisa kwamba tutaingia uchumi wa kati katika Taifa letu tutakapofika mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kama katika kipindi hiki tutachagua miradi mingine ya mkakati tutakuwa na msingi mzuri wa uchumi ambao unawahusisha watu wote basi ukichanganya kilimo tulichonacho, ukichanganya na madini

na mambo mengine ambayo tunayo utaona kwamba katika kipindi kifupi tunaweza kuwa nchi iliyoendelea.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nitoe mfano mdogo sana, sasa hivi hata bila kuongeza juhudzi katika kilimo tuna maeneo karibu hekta 500 ambazo tayari ni za umwagiliaji, ziko chini ya umwagiliaji ukizichukua hizo hizo hekta karibu 500 na ukawafundisha wakulima namna ya kuzitumia kulima mpunga peke yake, unaweza kuzalisha kwenye kila hekta tani 16 za mpunga kwa maana kuzalisha mara mbili kwa mwaka na kuzalisha tani nane kila kipindi.

Mheshimiwa Spika, utaona kabisa kwamba kwa uzalishaji huo tunaweza kupata kama tunaweza kuuza kwa dola 600 peke yake tunaweza kuwalisha watu wote hapa Afrika Mashariki na Afrika ya Kati mpunga kutoka kwetu. Tukiweka nguvu katika masoko mengine, tukiongeza nguvu katika utafiti wa kilimo, tunaweza kuwabadilisha wakulima wetu kutoka wakulima hao wanaoitwa wakulima wadogo wakawa wakulima wa kibiashara. Hivyo hivyo tukashika kwa mfano alioutoa hapa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, madini yale ya *soda ash* tunaweza kuwa wazalishaji wa pili duniani kwa kuzalisha *soda ash*. Na *soda ash* ile inaweza kutuzalishia *sustainably* au kwa uendelevu kwa zaidi ya miaka 1,000 na utaona kwamba kutohana na mambo haya na nafasi zingine ambazo tunazo za gesi, za madini mengine, tuko vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mambo haya mwanzoni tulikuwa tunayaongea kinadharia kwamba tuna madini, tuna hiki, tuna kile, lakini bado ni masikini, lakini kwa jinsi ambavyo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imechacharika na kutengeneza miundombinu kwa miaka mitano tukafika hapa tulipofika, naamini kabisa kwamba kwa nguvu hizi hizi za Rais tulienaye tunaweza kuwa nchi ambayo ina uchumi wa kati tena kwa katikati kabisa na tukaenda kwa raha zetu. Kwa hivi twendeni kwenye uchaguzi na nataka kuwaambia wale wanaovaa nguo za kijani msiogope maana yake tutashinda kwa kishindo na wale wanaogopa

ogopa basi wametuaga, lakini sisi ambao tumo tutashinda kwa kishindo kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe na mimi tumeingia hapa mwaka 2000 tusiondoke kabla ya mwaka 2025 na ukija hapa kwa kazi ambayo umeifanya kubwa namna hii, zamanii nilikuwa nashika *note book*, lakini sasa umeona nilichoshika, tunakuuhakikishia kwamba tutakurudisha hapo kwenye kitu maana unaweza kutuletea maendeleo makubwa zaidi ya yale ambayo tumeshayapata hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa wale tutakaorudi turudi na azma moja, watoto wetu tuwasomeshe vizuri na wale wanaokwenda Chuo Kikuu wote tuwape mkopo...

## TAARIFA

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa Eng. Stella

### **NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesikiliza toka mwanzo wa hotuba hii michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge wenye busara na hekima zao juu ya sifa nyingi wanazompa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, nikafikiri kwamba kwa sababu yeye kwanza ni mwanasayansi lakini pia ni mpenda Kiswahili na sasa hivi anayechangia ni Professa nikasema sasa kwa nini sasa Bunge lisiweze pia wakati wa kumaliza hoja yake au kuhitimisha, kutoa maelekezo kwa Vyuo vyetu kutengeneza timu itakayoweza kuangalia kwa mapana hii falsafa ya huyu Dkt. John Pombe Magufuli. Pia hata ile Baraza letu la Kiswahili kuja na neno au neno la Kiswahili linalomtafakari Dkt. John Pombe Magufuli kama ilivyozoleka kuna watu wanaitwa Vigunge, lakini pia tunafahamu kuna maneno kama *Borris Law*, *kuna Newton's Law* kutoekana na mambo ambayo waliyokuwa wameyafanya. Kwa hiyo naona niliweke hilo ili tuweze kuona namna bora ya kumuenzi kiongozi wetu huyu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana *Engineer Stella Manyanya*, anamuunga mkono Profesa P. L. Lumumba aliyesema *Magufulication of Africa*.

Malizia Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana sana kwa kunipa nafasi na naipokea kwa mikono yote miwili taarifa aliyonipa dada yangu Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Professa. Mheshimiwa Deo Sanga, halafu atakuja Mheshimiwa Suzanne Kiwanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa bajeti nzuri na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na TRA kwa kufanya kazi nzuri ya bajeti hii yenye muonekano mzuri wa maendeleo katika mwaka 2020/2021. Mheshimiwa Mpango abarikiwe sana kwa bajeti hii ambayo ameileta Bungeni hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Naibu Waziri wa Jimbo la Kondoa kwa kazi kubwa anayowafanya Watanzania hii ambayo tunaendelea kujadili hapa, tunamwombea kule Kondoa, ameacha shughuli nyingi za wananchi wake wa Kondoa anawafanya Watanzania amba ni pamoja na Kondoa. Kondoa wampitishe bila kupingwa na Mungu atawabariki sana wananchi wa Kondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nimempa pongezi Mheshimiwa Mpango na Watendaji wake. Mheshimiwa Mpango, Mungu najua aliyeyleta kutuhudumia sisi ambaye ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hatuna namna ya kusema ila tunamwombea aje tena Bungeni hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii nichukue kipengele kimoja tu. Yale ambayo tulikuwa tunalia kwa muda mrefu

tukizungumzia maboma ambayo wananchi kule wamefanya kazi za maendeleo za kujenga maboma mbalimbali wakishirikiana na Madiwani na sisi Wabunge. Leo bajeti hii inajibu kwenda kumaliza maboma tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niende sasa kwenye Jimbo langu, Jimbo Ia Wananchi wa Makambako ambao nawapenda sana na wao wananipenda sana. Tumefanyiwa mambo mengi ambayo na Wabunge wenzangu hapa wamesema. Ukienda kwenye maji nimesema hata kipindi kilichopita, sasa hivi Wakandarasi wapo *site* wanaendelea kufanya kazi. Ombi langu ile miradi ya Miji 26 ambayo na Makambako ipo na Wanging'ombe ipo na Njombe Mjini ipo na mahali pengine na pengine. Tunaomba fedha zile sasa miradi hii ianze wananchi wa Makambako tumewaambia mwezi wa Julai au Agosti, Mheshimiwa Profesa Mbarawa yupo hapa. Tunaomba miradi hii ianze ili iweze kuwasaidia wananchi wetu katika miji hii ukiwemo Mji wa Makambako. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia nitoe neno la shukrani. Tulikuwa na fidia pale Idofi kwa ajili ya kujenga *One Stop Centre*. Nilipokutana na Waziri mwenye dhamana na Katibu Mkuu akaniambia mwishoni mwa mwezi huu wa Juni au mwanzoni mwa mwezi Julai watakwenda kulipa fidia. Kwa hiyo wananchi wangu wa Makambako mkae mkaow wa kupokea fedha ambazo Serikali italipa.

Mheshimiwa Spika, jitihada zilizofanywa na Mheshimiwa Rais wetu, kubwa kwa nchi nzima na pamoja na mimi Makambako na mimi Makambako baada ya jitihada hizi za miaka mitano na mimi nimeunga mkono kujenga madarasa, kufanya shughuli za maendeleo zaidi ya shilingi milioni mia saba na ushee. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru na wadau walioitunga mkono, nawashukuru pia na Waheshimiwa Madiwani, namshukuru na Mwenyekiti wangu wa Halmashauri na Mkurugenzi kwa kazi nzuri waliyosimamia juu

ya maendeleo ya Halmashauri yetu ya Mji wa Makambako. Juzi tu tumeppata fedha za kumalizia jengo la halmashauri zaidi ya milioni 900, Mheshimiwa Mpango ubarikiwe sana, tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho sio kwa umuhimu, hili linakuhusu wewe Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika una vijana hapa wameomba wameeleza, nilikuwa nawasilikiliza kwa makini. Kijana Mheshimiwa Silinde, Kijana Mheshimiwa Lijualikali na wewe mwenzetu ndio unaingia Vikao vya Juu vya Chama cha Mapinduzi. Tunaomba mimi kama Mwenyekiti Mstaafu wa CCM, vijana hawa wapokelewe. Huyu Mheshimiwa Silinde na huyu Mheshimiwa Lijualikali, wapokelewe. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, la mwisho, tulishasema kurudia sio vibaya. Tunaendelea kukuombea kule Kongwa, wananchi wa Kongwa wakurudishe, upite bila kupingwa kwa sababu umefanya kazi kubwa ya nchi na ya Bunge hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, vile vile na wewe Mheshimiwa Tulia, kule Mbeya upite bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Maneno ya Mzee mzima hayo, hayaanguki chini hovyo hovyo. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami pia nichangie. Nashukuru nimeishi Bungeni kwa kipindi cha pilli sasa nikiwa Mbunge wa Viti Maalum. Nimefanya kazi yangu na wananchi wakaniona nikaenda kugombea na nikashinda Jimbo na nina imani kubwa kwamba wananchi bado wananihitaji, lakini hata wakinihitaji bila kwa kudra za Mwenyezi Mungu maana hapa

tunasema utafikiri kama vile tuna simu ya Mwenyezi Mungu kwamba kesho tutaaamka.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema na hapa nilipofika, yaani leo yangu ni leo, siyo kesho. Kesho namwachia Mungu. Watu wanajimwambafai utafikiri wao wana simu ya Mwenyezi Mungu, wamempigia simu, wanaona baadaye watakuwa bado wako hai. Mimi huko simo na Mungu anajua. Nasali kila siku, namwomba Mungu maisha marefu, afya njema, aniondolee kifo cha ghafla na niwaongoze wananchi kwa moyo mkuu kwa vile waliniamini, nami namwomba Mungu. Ahsante sana Yesu kwa neema zako ulizonjali na nimefikia hapa nilipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuko hapa kwa ajili ya uwezo wa Mungu na siyo kitu kingine. Pili, naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzania Bungeni iliyosomwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Halima Mdee ame-*crass quote* utafikiri ye ye ni Mchumi, Mwanasheria, CAG na kadhalika. Kwa kweli hongera sana Mheshimiwa Halima. Kwenye mitandao huko tunajua watu wanavyokusifu, kazania huko huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kwamba hapa tulipo tuliona ile barua, Mabaraza ya Madiwani yanavunjwa mwisho tarehe 10, lakini niseme tu kwamba hususan kwa Mkoa wa Morogoro, Mabaraza yako kwenye kizungumkuti. Mpaka leo Madiwani hawajui kinachoendelea. Wananiuliza, hivi Mabaraza yamevunjwa au hayajavunjwa? Nikawaambia si barua ilisema mpaka mwisho wa Bunge? Wengine hawajaitwa, hawajui kama Mabaraza yamevunjwa, hata stahili zao hawajui itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, sasa hiyo siyo vizuri ndugu zangu. Tumwogope Mungu ninyi TAMISEMI. Hebu fuatilieni, kwa mfano Mkoa wa Morogoro Mabaraza yote yamevunjwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Unapunguza dakika zangu tu.

**SPIKA:** Ndiyo taarifa.

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wa Mheshimiwa Mbunge ambao unaendelea, ni vizuri kwa ajili ya Watanzania wote wakajua, kwanza suala la kuvunja mabaraza lipo kwa mujibu wa sharia. Ni siku saba kabla ya kuvunja Bunge. Taarifa hizi zimepelekwa.

Mheshimiwa Spika, tuliwataka Waheshimiwa Madiwani kuhakikisha kwamba ikifika tarehe 10 mwezi wa Sita iwe ndiyo mwisho wa vikao vyote vya kisheria. Kwa hiyo, taarifa zimefika. Barua ya kuvunja nayo tayari ilishatumwa na *copy* ninayo, kama wanataka naweza nika-share. *GN* ilishatoka tayari.

**SPIKA:** Ndiyo, zimetumwa. Halmashauri zote wametumiwa hiyo. Mheshimiwa Suzan endelea.

**MHE. SUSAN L KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimeleta haya malalamiko hapa, ninamaanisha. Barua zimefika kwa Wakurugenzi lakini Madiwani kama Madiwani hawaelewi chochote, utekelezaji kule hamna na wala hawajui stahili zao wanapataje? Mpaka leo hawajapewa chochote, hawajui chochote, yaani wapo wapo tu. Kwa hiyo, hali ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie huko chini, hali siyo nzuri. Kwa hiyo, naomba tunapokaa hapa tuone kwamba kuna wenzetu wamewatumikia wananchi lakini wako kwenye kizungumkuti. Mmeandika barua lakini utekelezaji kule haupo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu bure, naomba tu mnaposema uchumi umekua, mimi sio mchumi, lakini umekua

kwa nani? Kwa Mtanzania huyu mmoja mmoja au kwenye mambo ya miradi mikubwa? Je, tunapokuwa kama viongozi wa wananchi, tunaposema uchumi umekua je, umekua kwa kununua ndege? Umekua kwa kujenga reli? Umekuwa kwa kufanyaje? Mbona hali ya wananchi kule chini meng'e meng'e, ndembe ndembe! Mbona kule wanafunzi; wazazi bado wanaajiri walimu?

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suzan pokea taarifa. Uko wapi? Aah, Mheshimiwa Laigwana.

## T A A R I F A

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba tu kunukuu kwa ajili ya ndugu yangu Mheshimiwa mzungumzaji kwamba katika ukuaji wa uchumi; uchumi wetu ambao sasa tunafungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu, kuna shilingi trilioni 1.03 iliyotengwa kwa ajili ya elimu bure na kama ushahidi kwamba ni ukuaji wa uchumi, shilingi bilioni 18.7 ya hiso fedha zimeingia Longido na zikabadilisha maisha ya watoto 18,000 waliokuwa wanaenda shule sasa wamefika 30,000.

Mheshimiwa Spika, huo ni mfano tu nimemtolea.  
*(Makofii)*

**SPIKA:** Taarifa hiyo, Mheshimiwa Suzan.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ninajadili hapa kama kKiongozi wa watu kule chini. Ninachosema ni kwa niaba ya wananchi. Jimbo la Mlimba Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero mpaka leo wazazi wanachangishana kwa ajili ya kuajiri elimu.

*Acha ubabaishaji wewe!* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Kama Jimboni kwako walimu wamejaa, ni wewe, kwangu mimi hamna walimu, hawatoshi. Wazazi wanalamika wanachangishana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan yafute maneno hayo, tafadhalii.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nafuta, lakini walimu bado wanaajiriwa, tena walimu wa mtaani ambao hawajapata ajira, wazazi wanachangishana mpaka leo kuajiri elimu. Kwa hiyo, mnaposema uchumi umekua, umekua kwa nani? Mbona wananchi bado wanateseka?

**SPIKA:** Kwamba walimu ni wachache au kuna *gap* ya walimu, hilo Serikali imekiri mara nydingi na imeeleza. Serikali peke yake siyo ya kulaumiwa, si tunafyatua sisi hawa watoto jamani! Hatupumzikil! Tunaambiwa taratibu, taratibu hatusikil! Hasa kule Mlimba, watoto wengiiii! (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa iko wapi? Aah, Mheshimiwa Naibu Waziri.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba katika Bunge lako Tukufu tulipitisha sheria ambayo inataka kuwatambua walimu wenye *profession* na ni *profession* ambayo ni sawa na *professions* nydingine.

Kwa hiyo, kama kinachoendelea Mlimba kwamba wanaokota watu mtaani na kuwaajiri kama walimu, wanakwenda kinyume na sheria. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Malizia Mheshimiwa Suzan, naona dakika zimeenda. Ni dakika tano tu kama wengine, sasa hivi imebakia moja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mungu wangu! Haya bwana, ndiyo mnachotaka.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia wastaafu wa TAZARA. Waziri anajua wamechakata. Kuna wastaafu 1,172 walistaafishwa kww lazima miaka 55 wakati sheria ilishatoka ni miaka 60. Mpaka leo wako mtaani wanadai haki zao lakini chochote kinachoendelea. Hawa wastaafu wanastahili haki zao. Naomba walipwe. Serikali imekaa kimya, kwenye bajeti ni kimya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mengi ambayo yanatatiza nchi hii. Mnposema uchumi umekua wakati wananchi wako na maisha duni, naomba uchumi ukue katika mambo ya miradi mikubwa, lakini wananchi mizunguko ya pesa iwepo kule chini ili wapate maendeleo yao na wao, kwa sababu wanasomesha, wanatakiwa wakate Bila za Afya na mambo chungu nzima. Uchumi umekua kwa nani? Labda kwa kikundi kidogo, siyo kwa Watanzania milioni 55.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Suzan Kiwanga. Kwa taarifa yako inakuja bunduki moja kutoka hapa Dodoma Mjini, sijui kama utaiweza Mheshimiwa Suzan. Jiandae huko, maana naona kitimtim chake ni kikubwa. (*Kicheko*)

Yeye ananielewa nasema nini. Ahsante sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Peter Serukamba uwe mchangiaji wetu wa mwisho. Waheshimiwa mko wengi, nimejitahidi lakini wapi. Kwa upande wa Wabunge Mheshimiwa Peter Serukamba, halafu itafuata zamu ya Mawaziri sasa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa leo, kwa kweli ni kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa waliyoifanya kwenye Jimbo letu la Kigoma Kaskazini. Kigoma Kaskazini leo kila Kata ukienda kuna miradi inaendelea. Kubwa zaidi ambalo ni kubwa sana, sasa tunatekeleza mradi wa Soko la Kimataifa la Kagunga, tumejenga Vituo vya Afya, vile vile kwa jambo kubwa la kihistoria tumeanza kujenga Hospitali ya Wilaya ya Kigoma Kaskazini. Tumejenga shule lakini pia tumepeleka maji Zashe, Kalinzi, Mkungwe, mradi wa Kidawe unaendelea, Matendo tunaendelea, Mkongolo II inaendelea, Kaseke, Kimbwela, tunapeleka maji Mwandiga; yote haya yamefanyika katika kipindi cha miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeanza na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ya kuleta mageuzi kwenye zao la michikichi. Tumeanzisha kituo pale Kihinga, sasa hivi tunabadilisha michikichi yetu. Kwa namna yoyote ile, ni kazi imefanyika kwa miaka hii mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali na kwa kweli baada ya kufanya yote haya, sisi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango tutamjibu Mheshimiwa Magufuli tarehe 25 mwezi wa 10. Majibu atayaona kwa watu wa Kigoma Kaskazini, tutasema Ndiyo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia wakati wa uchaguzi huu nataka nikuhakikishie kama alivyosema Mheshimiwa Mary, nitakuomba tutakaporudi hapa unichague nihesabu kura zako za Uspika kwa sababu mimi nitakuwa Mbunge. Kwa hiyo, kwa vyovypote vile kama wanavyosema wengine, kwa kweli hakuna harusi ambayo haina wasindikizaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, harusi yetu tutaitimiza mwezi wa Saba. Tutaanza *send off* mwezi wa Saba, wako watu watakuja kwenye *send offile* lakini pia tarehe 25 ndiyo siku

tutatimiza harusi yetu. Uwe na hakika watu wa Kigoma Kaskazini watasema baada ya yote haya tulioafanya kwa namna yoyote ile uwe na hakika tutakuja hapa na nasema hili nikiwa najiamini kwa sababu nawajua watu wa Kigoma Kaskazini wanataka nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sikutaka kusema kuhusu kazi alizofanya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli. Kazi alizofanya Mheshimiwa Rais huitaji tochi kuzitafuta. Kazi zake zinaonekana, zinajisemea zenyewe. Kwa miaka mitano hii ya Mheshimiwa Rais Magufuli, kwa kweli amefanya kazi kubwa, amefanya kazi tofauti na tulivyozoea na ndiyo maana tunaona mafanikio makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, alilisema Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango kule mwisho kabisa. Katika mambo makubwa mawili Mheshimiwa Dkt. Mpango alisema; moja, ni suala la *science and technology*.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali, huko tunakoenda mbele, lazima tuwekeze vya kutosha kwenye sayansi na teknolojia. Dunia yetu ya leo ni *science and technology*. tukiwekeza kwenye sayansi kilimo kitaboreka, mazingira yataboreka, elimu itaboreka, afya itaboreka na tutatoa ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hakuna namna yoyote, tunaweza; nami nataka nikuombe, najua siyo sahihi, lakini nikuombe, tuiombe Serikali itakayokuja ambayo itakuwa ni ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ikiwezekana tuunde Wizara ya *science and technology* ili tuwe na Waziri akiamka, akilala anawaza *science and technology*, huko ndiko ambako watu wote wameenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo kuna *drowns*, kwa siku moja unaweza ukapanda miti milioni tatu, kwa sababu unatumia *drowns*. Leo ukitumia *drowns* unaweza ukapeleka mbolea kwenye mazao yako *with the precision* kwamba hapa nataka kiasi hiki, inapeleka hicho hicho; ni kwa sababu ya *science and technology*.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, basi samahani. Naunga mkono hoja, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Sasa tunaanza na upande wa Serikali, ni uchangiaji pia. Tuanze na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo dakika tano tano.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Karagwe kwa kuniamini na kwa ushirikiano ambao wamenipa kwa kipindi cha miaka mitano. Tumeshirikiana kufanya mambo mengi na ninaamini Oktoba, 25 watafanya maamuzi ya kunirudisha hapa ili tuendelee kuchapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Mheshiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika majukumu aliyonipa. Pia nakushukuru na kukupongeza wewe kwa namna ulivyotuongoza kwa kipindi cha miaka mitano. Bunge hili umeliongoza kwa weledi na viwango vikubwa, tunakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, Naibu Waziri na timu ya Wizara nzima Wizara ya Fedha na Mpango kwa bajeti nzuri sana. Kama Waziri wa Viwanda na Biashara pongezi nydingi kutoka kwa *Private Organization; Tanzania Private Sector Foundation, Confederation of Trade Industry, Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, TCCIA*. Mheshimiwa Dkt. Mpango wa niaba ya Serikali, pokea pongezi hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara na wenye viwanda nchini wamepongeza bajeti hii kwa mambo mengi, lakini naomba nitaje mambo matatu. Kwanza, maboresho

makubwa ya mfumo wa kodi, ada na tozo kwa ajili ya kukuza sekta binafsi hapa nchini, lakini pia utekelezaji wa *blue print*, kwa kiasi kikubwa sana Serikali tunaendelea kuzidi kutekeleza ile *Business Action Plan*. Mpaka hivi sasa ukiangalia *fiscal year* ya mwaka 2018/2019, 2019/2020 tayari tozo 114 zimeshaondolewa. Hata ukiangalia Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvu siyo chini ya kodi, tozo 124 zimeshaondolewa. Kwa hiyo, wafanyabiashara na wenye viwanda nchini wanaipongeza na kuishukuru sana Serikali kwa jitihada na *speed* kubwa ya kutekeleza *blue print*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nielekee kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge katika michango yao wamegusia Wizara ya Viwanda na Biashara. Ni kutoa *clarification* tu; nianze na suala la sukari. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania mnaelewa, Serikali ilifanya jitihada ya kuleta *gap sugar* ili kuondoa upungufu wa sukari nchini lakini tunashukuru hivi sasa viwanda vya sukari vimeshaanza uzalishaji. Kwa hiyo, hamna haja ya kuwa na wasiwasi, *gap sugar* bado inaendelea kuingia nchini lakini viwanda vimeanza kuzalisha. Sasa hivi viwili kwa pamoja sukari inayooingizwa nchini pamoja na uzalishaji ulioanza, hamna haja ya kuwa na wasiwasi juu ya upatikanaji wa sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, pia zao la Tumbaku namshukuru sana Mheshimiwa Rais Msukumo aliotupa, tulishirikiana na Waheshimiwa Mawaziri na hivi sasa zile tozo ambazo zilikuwa kero kwa viwanda vya Tumbaku tumeshaziondoa na kulikuwa na tozo za *FCC* tumeziondoa zote, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tabora na maeneo mengi yanayolima Tumbaku pamoja na wakulima wa Tumbaku, Serikali imewasiliza na tutakuwa na misimu mizuri ya zao la Tumbaku kwa misimu inayokuja kwa hizi jitihada ambazo zimefanywa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna kiwanda cha vifaa tiba cha Simiyu, Mheshimiwa Ndaki ameongea kwa machungu, lakini nimhakikishie Serikali katika hili tuko katika jitihada ya haraka sana kuhakikisha kiwanda hiki kinaanza. Natambua *MSD* hata jana walikuwa na kikao kuhusu hiki kiwanda cha kutengeneza

vifaa tiba kule Simiyu. Kwa kutambua umuhimu wa kufungamanisha kilimo na viwanda hasa mazao ya wakulima ambayo pia yanaingiza fedha za kigeni ziklwemo zao la Pamba, basi nikmhakikishie Mhshimiwa Ndaki, Serikali tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kiwanda hiki kinafanya kazi haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kutoka kwa Mheshimiwa Turky kuhusu *import* ya mifuko mbadala. Tumesikiliza hoja yako na Serikali tutafanya *study* kwanza kujiridhisha kwamba viwanda vinavyozalisha nchini vinaweza kuzalisha mifuko ya kutosha mbadala ili tusiweke zuio bila kufanya *study* kuweza kuleta adha ya upungufu ya upatikanaji wa mifuko mbadala; lakini tumekusikia tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna mchango kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Kafumu kuhusu Ngaka.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge Serikali tumejiridhisha kwamba mradi wa *TANCO* hauna manufaa kwa nchi, *partnership* kati ya *NDC* pamoja na *inter energy*, mkataba ule ulikuwa hauna maslahi kwa Taifa. Kwa sababu ya jithada nzuri ya Serikali iliyoifanya ya kuwa na sheria za kulinda rasilimali, tayari tumeshaunda *Government Negotiation Team* kwa ajili ya kupitia upya mkataba wa *TANCO* kwa malengo ya kuhakikisha nchi inanufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile viwanda vya saruji vinahitaji sana makaa ya mawe, baada ya kuwa na mkataba mzuri ambao umezingatia maslahi ya Taifa, *TANCO* itaendelea kusaidia viwanda vya ndani ili viweze kuzalisha kwa ajili ya mahitaji ya ndani na kwa ajili ya soko kubwa kwa nchi zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka sana; kwa bajeti nzuri ambayo Mheshimiwa Mpango ameiletla hapa Bunegni, sisi Wizara ya Viwanda na Biashara tutajikita kwenye kuhamisha uendelezaji...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** ...na matumizi ya bidhaa za ndani, kuimarisha *SIDO* ili iweze kuwasaidia wafanya biashara nchini, kujenga kongani za kujenga viwanda vikubwa kwa ajili yaku-export pamoja na mambo mengine mengi sana.

Mheshimiwa Spika, kwahiyio, naungana na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania waliopongeza kwa kishindo kikubwa sana juu ya bajeti hii ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Mapango. Tunakupongeza sana, hongera sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Watanzania tutakaporudi kwenye uchaguzi kura zote zitakwenda kwa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tafadhali, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mpango pamoja na timu yake nzima ambayo imekuja na bajeti ya kishindo ya namna yake ya mwaka. Hii ndiyo bajeti ya kwenda nayo kwenye uchaguzi; kwa kweli ni bajeti nzuri sana. Mimi nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa kiwango kikubwa sana; lakini wapo waliosema kwamba mpango huu hautekelezeki na mambo mengi hayajatekelezwa. Nataka niseme kitu kimoja; yapo maeneo ya kipaumbele ambayo

tulikubaliana kwamba haya tutayasimamia na tutayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza la kipaumbele ilikuwa ni ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda. Hili halina mjadala, mambo na mafanikio makubwa yaliyofanyika kwenye upande wa viwanda hili hatuwezi hata kulijadili. Eneo la pili, ilikuwa ni kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, hili nitalifafanua. Eneo la tatu ilikuwa ni ujenzi wa mazingira wezeshi wa biashara na uwekezaji.

Haya maeneo makubwa matatu ndiyo msingi wa mkubwa wa utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Tano na haya yote tumeyafanya kwa ukamilifu na yameleta matumaini makubwa na maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie hili la pili, hili ambalo tunasema kufungamnisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, na nataka nijikite hapo. Tunaposema kufungamanisha maendeleo ya ukuaji wa uchumi, tunaposema ukuaji wa uchumi tunazungumzia kwanza sekta za uzalishaji zinazochangia kwenye uchumi ikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi, madini na sekta zingine; hizo ni za uzalishaji; halafu unaziunganisha na Maji, Afya, Elimu. Uwekezaji uliofanyika katika hayo maeneo unaposema kwa kweli hatufanikiwa utakuwa kweli nafikiri umelala. Mambo makubwa yallyofanyika kwenye hili eneo yamechangia sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa kilimo watu wanasema uwekezaji haukuwa wa kutosha. Kama uwekezaji haukuwa wa kutosha kwenye kilimo tusingekuwa tumejitosheleza kwa chakula kwa kipindi cha miaka mitano. Utoshelevu wa chakula umekuwa ni zaidi ya asilimia 120; hiyo ni ishara kwamba tumeweza kufanya vizuri sana; na hili ni la muhimu sana kwa Waheshimiwa wote kulielewa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili; wengine wanaangalia uwekezaji wa ujenzi wa miundombinu. Kwa mfano sasa hivi tuangalie miradi ya kimkakati ambayo imetekelozwa, nitasema michache.

Mradi wa Ujenzi wa Umeme, Bwawa la Nyerere, ule utawasaidia. Umeme unakwenda Vijiji utawasaidia kuchakata mazao, utawasaidia kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya mazoa yao, ni sehemu ya uzalishaji, ni sehemu ya kilimo. Miradi ya SGR; tunajenga reli, hii reli itakwenda kuwasaidia wakulima kusafirisha mizigo na wao wenyewe kuasafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, tunajenga viwanja vya ndege; sasa hivi tunahangaika na mazao mbalimbali kuyapeleka nchi za nje, maana yake hivi viwanja vitasaidia katika kuweza kuongeza thamani ya mazoa na kusafirisha mazao yetu. Pia tunanunua meli na kila namna.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo utakuta kwamba sekta zote hizi, uwekezaji wa miradi yote hili kwa kiwango kikubwa utasaidia kuendeleza kilimo cha Tanzania. Kwahiyo huo ni uwekezaji ambao ni mkubwa. Ajira nyingi zimeongezeka tulishasema kwenye bajeti, tuliweka takwimu, viwanda vingi tumevoweza lakini yote hayo ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, najua Waheshimiwa Wabunge wamzeungumzia changamoto ya masoko, na mimi nimekubaliana kabisa. Tumejipanga katika hili, na tumeshasema tumeunda kitengo cha masoko, tunashirikiana na viwanda na biashara kuhakikisha masoko ya mazoa ya wakulima; mazao ya biashara, chakula, mboga mboga, maua pamoja na mazao ya matunda nayapatikana; na hili litawezekana kwa kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeongeza uwezo wa kuhifadhi. Unaweza ukazalisha, usipokuwa na uwezo wa kuhifadhi utapata changamoto. Tumeongeza uwezo wa kuhifadhi. Sasa hivi chini ya Serikali hi ya Awamu ya Tano uwezo wa kuhifadhi katika Wakala wa Taifa wa *NFRA* na Bodi ya Mazao tumefikia sasa uwezo wa kuhifadhi tani 651,000, kwa hizo taasisi tu. Ukichukua kwa pamoja ni zaidi ya tani 3,700,000 zinaweza zikahifadhiwa kwenye maghala mbalimbali yaliyoko kwenye halmashauri na yaliyoko huko

katika maeneo mbalimbali. Nadhani Serikali hii imefanya mambo makubwa sana ambayo tumewezesha.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amesema kwa kweli hatujui takwimu za pembejeo. Mimi nafikiri hili suala atakuwa analiota, hajasoma Bajeti ya kilimo. Tumeweka takwimu zote za miaka minne yapi yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, labda nimwambie tu kwa mfano; mwaka huu peke yake; Mheshimiwa Spika labda kwasababu ya muda nipe tu dakika moja; kwa mwaka huu peke yake tumesema kwenye upande wa mbolea tulikuwa tunahitaji tani 586,000 lakini hadi mwisho wa mwaka tumeefikia mbolea tani 675,000. Ukituambia hatujui takwimu tunakushangaa. Tumeweka takwimu za mbegu, tumeweka takwimu za madawa yanyohitajika kwahiyo kila kitu kipo...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa

**WAZIRI WA KILIMO:** ...akisoma atapata takwimu zote zinaeleweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa.

**SPIKA:** Dah, muda wangu mdogo Halima. Ndiyo nusu

## **TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, sisi Kambi ya Upinzani tulikuwa tunatumia nyaraka za Serikali yenyewe kwenye hoja yetu kuhusiana na pembejeo na jinsi ambavuo

Wizara haifanyi utafiti, inaotea. Si maneno yangu mimi, ni maneno ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye amezungumza baada ya kufanya kaguzi maalum saba kuhusiana na kilimo. Sasa kama Mheshimiwa Waziri ana tatizo asiwe na tatizo na sisi, muwe na tatizo kati yenu wenyewe na mifumo yenu ya kazi ambayo CAG amekagua na kugundua hivyo. Kwahiylo kwa maelezo ya CAG ni kwamba, hata hicho anachokizungumza sasa ni kwamba umeotea, kwasababu mlisema hamna fedha ndiyo maana mnafanya makadirio, hamna fedha za utafiti. Kwahiylo usininyooshee kidole. Wakati unaninyooshea mimi vine vinakurudia, tatizo ni ninyi siyo sisi.

**SPIKA:** Lakini Mheshimiwa Halima katika Sayansi *ku-estimate* vitu nayo ni methodology ambayo inakubalika. Kuotea Kiswahili kingine, inakubalika kabisa lakini ilimradi estimation yako iwe na *basis* ambazo ni *correct* lakini tumekuelewa kama ni maneno ya CAG. Mheshimiwa Waziri wa Nishati ajiandae Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Mpango wa Serikali ambao umesheheni mafanikio makubwa sana wka kweli kwa miaka hii mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwakilisha mpango huu mzuri ambao unatekelezeka karibu kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia mambo machache ambayo ni muhimu sana kwenye kukua kwa sekta zote za kiuchumi duniani na hata hapa kwetu katika kutekeleza uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, yako mambo manne ambayo ningependa niyatolee ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni upatikanaji wa nishati ya uhakika na inayotabirika. Sote ni mashahidi, kabla ya miaka mitano iliyopita usingeweza kukaa katika Bunge Lako Tukufu kwa mfululizo kwa vipindi vyote vya Bunge bila

umeme kukatika. Hii ni ishara kubwa hakuna dalili. Nikisema kitendawili ni tarehe ngapi umeme ulikatika Bungeni siwezi nikapata jibu leo. Nategemea makofi ya Waheshimiwa Wabunge kwasababu ni mafanikio makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niendelee kusema kuhusu uzalishaji wa umeme. Mwaka 2015 tulikuwa na upungufu wa umeme wa *megawatts* 170 hadi *megawatts* 270 upungufu, na ndiyo maana kulikua na mgao wa umeme. Hata hivyo Serikali hii imechukua hatua madhubuti za kuhakikisha umeme unapatikana wa kutosha na unatabirika na hatua kubwa ambazo zilichukuliwa ni mbili tu. Jambo la kwanza ni kuondokana na mitambo ya kukodi iliyogharimu pesa nyingi za Serikali; na kukarabati mitambo muhimu ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, tunapoongea hapa Mtera iliyokua inazalisha *magawatts* 80 kwa wakati ule ilirudi chini na kuanza kuzalisha *megawatts* 20 tu, Kidatu inayozalisha *megawatts* 204 ilibaki kuzalisha *magawatts* 40; na mingine na mingine. Lakini Serikali imechukua hatua kubwa ya kukarabati mitambo yote hii leo hii inazalisha umeme kwa kiwango chake cha juu cha asilimia 100. Kwahiylo ni jambo la kuipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sana kwa mwaka huu tuna bahati. Ningependa nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, kwamba Bwawa letu la Mtera leo limefika kiwango chake cha juu; na tuna bahati nzuri sana kwasababu maji ni ya kutosha, ya mita za ujazo 698.74 ambacho ni cha juu kabisa. Kwahiylo, tuna uhakika wa kupatikana kwa maji ya kutosha na kuzalisha umeme wa uhakika kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo mfululizo. Ningependa kuwapa taarifa hiyo Waheshimiwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Mbunge wkamba tumezalisha umeme kidogo kwa miaka mitano iliyopita; naomba niweke sahihisho kidogo. Tumezalisha zaidi ya *megawatts* 398.8 kwa miaka minne hii iliyopita, na huu ni umeme mwingi sana unaweza ukatumika

kwa nchi za jirani za Rwanda na Burundi. Wenzetu Burundi wa *megawatts* 45 tu na Rwanda wana *megawatts* 180 lakini sisi tumeweza kuzalisha *megawatts* 398.94 kwa miaka minne iliyopita; kwahiyo jamani kwanini msipige makofi kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa jambo hili kubwa liliofanyika? Na hiyo ni sawa na asilimia 33.45 ya umeme uliokuwepo hapo nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatekeleza miradi mikubwa ukiwemo wa Julius Nyerere wa *megawatts* 2115. Tukiongeza na tulizonazo, tukaongeza na *Kinyerezi extension* inayokuja ndani ya miezi minne ijayo pamoja na wa Rusumo *megawatts* 27 ndani ya miezi sita ijayo na miradi ya jadidifu *megawatts* 950ndani ya miezi saba ijayo tutakuwa na zaidi ya *megawatts* 4,828 na wakati huo mahitaji yetu ya umeme yatakuwa ni *megawatts* 2,778. Tutakuwa na umeme wakutosha kufanya shughuli zetu na kuwauzia majirani zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii Zambia wana-*shortage* ya umeme *megawatts* 151. Tuna mahusiano mazuri, tunahitaji tuwauzie, tuongeze mapato na kujiiamarisha kiuchumi. Nimeona nitoe taarifa hii kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi ili waweze kulijua.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kukatika kwa Umeme. Ni kweli zipo changamoto ndogo ndogo, lakini kukatika kwa umeme kunakofanyika kwa sasa hivi au kunakotokea hakuchangiwi na kutokuwepo kwa umeme wa kutosha bali kunachangiwa na matengenezo yanayoendelea takriban nchi nzima ambako ni lazima tufanye matengenezo. Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi kama nyumba yako inakata umeme mara nane, mara tisa inawezekana aliyefanya *wiring* ultumia kishoka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba tunafanya matengenezo mara zote, na tunapofanya matengenezo ni lazima tukate umeme, lakini tunatoa taarifa. Katika hili nitoe wito kwa mameneja na wakandarasi wote, wanapokata umeme kufanya matengenezo watoe taarifa, lakini lengo letu ni kuboresha.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili tuliyoichukua ili kuondoakana na kukatika kwa umeme kunakokatwa na wataalam wetu ni kujenga miundombinu kwa *ku-replace* nguzo za miti na nguzo za zege tunazoanza kuzitekeleza kuzitumia kuanzia tarehe 01Julai, 2020. Kwahiylo ni matumaini yetu maeneo ambayo yamekaliwa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie

**SPIKA:** Ndiyo, ndiyo malizia.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na atamalizia Mheshimiwa Waziri wa Uwezeshaji

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie. Kwanza naunga mkono hoja iliyoko mezani. Mimi pia niseme machache kwenye baadhi ya hoja zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunachangia Bajeti ya Serikali nianze kama mtaalam wa sekta ya uchumi. Niliwasikia ndugu zangu hapa wakiongelea mambo ambayo wameyapotosha kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, moja, walikuwa anaongelea takwimu za kupungua kwa umasikini, niliwasikia pale, wakijaribu kuhoji uhalisia wake; lakini la pili waliongelea kuhusu utekelezwaji wa mpango na wakaubatiza jina kwamba ni zero.

Mheshimiwa Spika, tunapojadili masuala ya kiuchumi kwa wale wasio wachumi ni vyema sana wakaomba *guidance*, wakapewa usaidizi ili wachangie vizuri yale mambo wanayotaka kuyachangia.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hilo tu kwasababu hapa ni Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri sana ukikosa *guidance* za kutafsiri takwimu ni vizuri pia ukaenda kutafsiri vile vinavyofanyika katika eneo lako la kazi.

Mheshimiwa Spika, hebu angalia ndani ya miaka mitano, ametoka kusema Waziri wa Nishati, vimeongezeka vijiji vilivyopata umeme kutoka 2,000 mpaka 9,000 kati ya vijiji 12,000 na zaidi vilivyoko kwenye nchi. Je, hiyo ni zero kwenye utekelezaji?

Mheshimiwa Spika, ndani ya kipindi hicho hicho, taasisi ambazo zimepokea umeme; yaani taasisi za elimu, afya na sehemu nyingine ambazo zinahuduma kwa jamii kama visima vya maji, 11,000 na sehamu. Yaani hapo ndipo wanaposoma watoto wetu, wanapotibiwa zetu, watoto wetu lakini pia na jamii nzima wanapokwenda hospitalini ambao walikuwa wakitibiwa kwa kuwashaa tochi; 11,000 zimeunganishwa kwa umeme. Hiyo ni zero kwa mtazamo wao?

Mheshimiwa Spika, barabara za vijijini hata tunalofanya ziara zaidi ya kilometra 74,000 ndani ya miaka mitano zimetengenezwa kwa kiwango ambacho kinapitika. Kwa *assessment* yao hiyo ni zero kwenye utekelezaji wa Mpango?

Mheshimiwa Spika, lakini si hiyo tu, achilia sekta nyingine na miradi mikubwa ile; pamoja na ndege ambazo hazijanunuliwa kwa kiwango hicho tangu uhuru. *SGRambayo* tulikuwa tunasoma kwenye maswali ya kuchagua kwamba ilijengwa na Wareno, wajerumani na wengine wote watakaowataja leo zimejengwa na Rais Magufuli, mtoto wa Kitanzania wa wazazi masikini; hiyo ni zero kwa mtazamo wao?

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu, kila kitongiji kimeguswa kwenye elimu bure. Pesa zile zinakwenda; ukitajiwa iddai ya fedha zile ukizimwaga hapa kama ni mpya utasikia harufu ya dawa tu, kama ni kuukuu utasikia harufu ya Tumbaku; zinamwagawa kusaidia watoto wa shule, hiyo ni zero?

Mheshimiwa Spika, lakini pia waangalie basi hata hao watu wanaosema zero, ukisema zero kwenye mpango kama *program* au zero kwenye mpango kwa jina la Dkt. Mpango? Huwa tukienda kwenye *panel* za kiuchumi kabla hujaijadili hoja unatakiwa upate *CV* ya *presenter*. Waulize sasa wale wanaojadili; nilimuona Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Esther na Mheshimiwa Jesca. Labda muwe mna-*publish* vizuri na *CV* za Waheshimiwa Wabunge ili tuone anayemjadili mwenzake ana *CV* gani. Hawa waliokuwa wanajadili Dkt. Mpango leo hii Dkt. Mpango akiamua kurudi kufundisha Chuo Kikuu na wao wakaamua kurudi kwenda kujifunza uchumi inawahitaji miaka kadhaa kuwa tu na sifa ya kuwa mwanafunzi wa Dkt. Mpango. Dkt. Mpango licha ya kuwa Mhadhiri lakini ndiye gwiji wa kuandaa mipango, amefanyakazi Tume ya Mpango, tuna-*doubt* nini kuhusu mpango ilhali mambo tunayaona *site*.

Mheshimiwa Spika, vituo vya afya zaidi ya 478 ndani ya miaka mitano kwa wastani wa kituo cha afya kila tarafa ya nchi hii chenye hadhi ya hopsitali ya Wilaya unasema zero?

Mheshimiwa Spika, lakini siyo tu, hospitali za ngazi ya wilaya 71 nusu ya karibu wilaya zote ndani ya miaka mitano, unasema zero?

Mheshimiwa Spika, nenda kwenye bajeti yenye ya vifaatiba, dawa, bilioni 270. Hizi ni sekta chache tu ninazozitaja, unasema zero? Zero kwao inamaanisha nini? Kwahiylo niliona hili na lenyewe nilisemee kwasababu kwa kweli kazi imefanyika kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini hata ukienda kwenye utaratibu wa utoaji wa haki, zaidi ya mahakama 960 sasa

hivi ziko kwenye hatua ya mwanzo, maana yake ni nini, maana yake ni kwamba haki imesogezwa kwenye huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, na la mwisho dakika moja tu; Mheshimiwa Khatibu alikuwa anaongelea suala la Katiba kuvunjwa. Nchi yetu kwa mujibu wa Ibara ya nane, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na wananchi ndio msingi wa mamlaka yote. Sasa kama tunafuata misingi ya kidemokrasia na haki mnataka tuanze kukamata kila mtu anayeongea jambo? Hatutafanya hivyo kwasababu Watanzania nchi ni yao, Katiba ni yao na Rais ni wao, wana haki ya kusema kila kitu wanachoona kinafanywa vizuri. Hata tunavyosifia kazi hizi, ukiona mwenye nguvu sana amebeba mzigo usidhanie ule mzigo ni mwelesi. Rais wetu kafanya mambo makubwa mno na hayatafutika; ni vyema tukampa hata haki ya kupongeza tu kila anachofanya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja na kwakweli namtakia afya njema Rais wetu na Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi kubwa aliyofanya pamoja na mtani wangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu kwa kazi aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Ashatu hata wakitaka tuwaongeze nyama ya punda tutapeleka tu kwasababu hiyo tumeona kazi kubwa wanayoifanya. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, umeongea vizuri pia tuwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba Bunge hili katika vikao vyake katika mikutano yake minne kwa mwaka mkutano huo unajadili habari ya mipango ya nchi kila mwaka na kwa hiyo kabla ya bajeti tunajadili na kutoa mapendekezo kuhusu mipango yote mikubwa ya Serikali na baada ya mjandala ule wa Bunge hili ndiyo Mheshimiwa Dkt. Mpango anaenda kutengeneza mpango sasa ambao unafuatana na Bajeti. Kwa hiyo, kinachokuwa *presented* hapa ni chetu hakiwi cha Mheshimiwa Dkt. Mpango peke yake, kwasababu na sisi tumehusika katika mchakato mzima kwa hiyo, na sisi ni

sehemu ya kilichopo. Mheshimiwa Waziri wa uwekezaji Mheshimiwa Kairuki. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na uongozi mzima wa Wizara ya Fedha kwa kuja na bajeti ambayo imejikita katika kukuza uchumi, kuja na bajeti ambayo imejikita katika kukuza uwekezaji nchini, lakini vile vile kuweza kulinda wazalishaji na wawekezaji wa ndani. Lakini zaidi kuhakikisha kwamba bidhaa zetu tunazozalisha nchini zinaweza kushindana dhidi ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kiasi kikubwa wameweza kuzingatia maoni na mapendeleko yaliyotolewa na ofisi yetu wizara ya viwanda na biashara lakini vilevile, sekta binafsi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza *blueprint*, lakini vile vile ni kuona kwa namna gani tunaiwezesha nchi yetu iendelee kujitegemea kiuchumi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa namna ambavyo ametambua mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa pato la Taifa lakini vilevile, katika kuona ni kwa namna gani sekta binafsi inashiriki na kuchangia katika ukuwaji wa uchumi wetu vilevile.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa kuwa na bajeti hii kwasababu ni bajeti ambayo inaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ni bajeti ambayo imejikita katika kuoanisha na kupunguza viwango nya kodi, ada na tozo mbalimbali, lakini ni bajeti ambayo imejikita katika kuongeza wigo wa walipa kodi na kuweka mazingira rafiki kwa walipa kodi. Lakini vilevile kuendelea kuimarisha haswa baraza letu au bodi yetu ya rufani ya kodi katika kuharakisha mashauri mbalimbali na mapingamizi ya kodi kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tunashukuru sana sana kwa namna ambavyo kuitia bajeti mbalimbali

tumeona mchango mkubwa katika ukiangalia mchango wa reli katika *SGR*, ukiangalia katika ununuzi wa ndege mpya ambaao umefanyika kwa kiasi kikubwa yote haya na nishati na maji yana mchango mkubwa ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwa na mazingira bora ya uwekezaji kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nishukuru sana kwa upande wa ardhi katika mpango wa kupima kila kipande cha ardhi itatuwakikishia na sisi kwa upande wa uratibu wa uwekezaji kuhakikisha kwamba wawekezaji wanapokuja basi wanakuwa na uhakika wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Lakini bajeti hii imejibu malalamiko ya madai ya wazabuni wetu na wakandarasi tunashukuru zaidi ya bilioni 476 zimeweza kulipwa kwa wazabuni na wakandarasi na tunaamini wengi zaidi wataweza kuendelea kulipwa tunashukuru kwa namna ambavyo kodi au riba mbalimbali katika *bank* zetu imeendelea kupungua tukiamini kwamba wawekezaji wataweza kupata mitaji kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tunashukuru kwamba kuititia bwawa letu la Nyerere *Hydro*, inajibu changamoto wa upatikanaji wa nishati kuititia *megawatt* zile 2,115. Lakini tunashukuru namna ambavyo *TRA* pamoja na taasisi za Serikali ambazo zimeendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielotroniki tutaendelea kuhakikisha kwamba tunakuwa na huduma zaidi za uwekezaji na biashara kutumia mifumo hii ya elekroniki ili kuweza kuwapa nafuu wawekezaji wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ni shukuru katika marekebisho yaliyofanyika ya kodi katika zaidi maeneo kumi na sita ikiwemo ushuru wa forodha, msamaha wa *VAT* hususani katika bima ile ya Kilimo ya Mazao ilikuwa ni changamoto kubwa kwa sasa wakulima wetu wataweza kunufaika na haswa wawekezaji wetu wakubwa na wakati kujikinga dhidi ya mahafa, mafuriko ukame lakini na matukio na majanga mengine yejote ambayo yanakuwa hayajapangwa.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa punguzo la *SDL* kwa niaba ya waajiri na wawekezaji ambao ni wadau wetu wakubwa tunaamini fedha hizi punguzo hili itassaidia kuongeza mtaji katika uwekezaji katika shughuli zao. Lakini vilevile tunashukuru katika masuala mbalimbali katika mapunguzo ya vifungashio katika ushuru wa forodha, katika vifungashio katika korosho pamba ulinzi wa magunia ya mkonge tunaamini yote haya yataweza kusaidia kuchochea uwekezaji wa ndani lakini zaidi kulinda viwanda vyetu nya ndani.

Mheshimiwa Spika, lakini sita sahau punguzo au wa ushuru wa forodha katika vifunko katika chupa za mvinyo lakini tunaamini miaka ijayo basi waweze kuangalia pia *label* chupa pamoja na vitu vingine kwa sababu bado ni bidhaa ambazo ni muhimu katika ushindani katika bidhaa zetu za mvinyo. Lakini nashukuru katika ulinzi kwa viwanda nya marumaru lakini vile vle katika viwanda vyetu nya kahawa katika vifungashio, katika nepi zile za *baby diapers* kwa kweli nipende kushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mpango katika vikao vile vilikuwa ni vizito na nya moto lakini nashukuru kwamba mengi ambayo tumeyaleta kama ofisi ya Waziri Mkuu na uwekezaji na Viwanda na Biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini wizara za sekta kilimo mifugo na uvuvi kwakweli mmetutendea haki ni imani yetu bajeti ijayo sasa basi mtawezza kuwa shirikishi na kuweza kuzingatia masuala mengi zaidi ili zaidi kuhakikisha kwamba wawekezaji wetu hasa wazawa na wenyewe pia wanachangia katika uchumi wa Taifa lao tunashukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mkiangalia muda wetu mnikubalie kwamba kwa leo tuishie hapa. Niwaombe radhi sana wale ambao hamkupata nafasi mko wengi sana maana yake majina yanazidi kuja. Nafikiri ambao hawajapata nafasi ni zaidi ya hata waliokuwa wameorodhesha asubuhi. *Almost* zaidi ya 50 hivi hawakupata nafasi.

Jumatatu bado kuna wenzetu wachache watapata nafasi ya kuweza kuchangia kidogo katika baadhi ya mambo kwa zile hoja zitakazokuwepo siku ya Jumatatu kama ambavyo nimekwishakueleza kabla. Siku ya Jumatatu tutakuwa na mambo mengi mengi mengi sana. Lakini tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha labda robo saa hivi halafu Waziri mwenyewe kama nusu saa, halafu tutaanza kupiga kura. Kura ile muhimu sana ya Bajeti, ningeliwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuwepo siku ya Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi tuwe hapa tuweze kuanza kwa pamoja.

Niwakumbushe kwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, hii ni *three line weep* usipokuwepo Jumatatu na unatarajia kugombea safari hii, sidhani kama jina lako litakuwa kwenye orodha. Kwasababu utakuwa umefanya *capital offence* kwa hiyo, sishauri usafiri halafu sijui gari limekuharibiklia huko, sijui imekuwaje, sijui mimi nilikuwa hilvi kikazi, sijui Waziri nilienda wapi hakuna hiyo.

Jumatatu, saa tatu, mje hapa mtekeleze takwa la kikatiba kwanza mengine yote yatafuata baada ya hapo. Niwatangazie tangazo la Mheshimiwa Mama Sitta wale wa *TWPG* wenye zoezi lao maalum ambalo litafanyika kesho basi leo wakutane pale Msekwa D baadaye kidogo baada ya kuahirisha hapa wanajifahamu wenyewe.

Lakini kuhusu zoezi la kesho, Jumapili mchana la kukabidhi ile shule ya wasichana ambayo tumeijenga kwa Serikali. Mgeni wetu rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nawakaribisha Waheshimiwa Mawaziri wote, Waheshimiwa Manaibu, Wabunge wote tuweze kuwa pale saa nane kamili. Na kwa wale ambao wanahitaji usafiri tutakuwa na mabasi ya kutosha hapa. Lakini mabasi haya hataondoka saa saba kamili kuelekea Kikombo.

Wale wenye usafiri wao wenyewe, tumeandaa eneo la kutosha tu la *parking* wala hakuna tatizo. Kwa hiyo, tuungane sote na niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge kwa zoezi la kesho basi asiyekuwepo na lake halipo. Nafikiri

mnanielewa kuhusu utaratibu uko vizuri ni kamili kabisa. Utaratibu ni kamili kabisa yaani uko vizuri.

Katika dakika hizi za mwisho huwezi juu inaweza kusaidia saidia kidogo, kujaza *full tank* ya *petrol* au *diesel*. Kwa hiyo, kwa kuwa muda sasa hauko upande wetu niwashukuruni sasa nyote. Niahirishe Shughuli za Bunge hadi keshokutwa siku ya Jumatatu saa tatu kamili juu ya alama tunaanza shughuli.

*(Saa 08.10 Mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu,  
Tarehe 15 Juni, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*